# NGUVU ILIYOPO KATIKA

# SADAKA

# ISIYO YA KAWAIDA

**CPA Mbogo Nyakangara Kerenge**

**Mawasiliano ya Mwandishi**

Simu: 0763547281/0714 611669

Barua pepe: mbogokn@gmail.com

Facebook: Mbogo Kerenge

Tovuti: **www.nguvuyasadaka.com**

You Tube: **nguvuyasadaka**

**Toleo la kwanza: 2022**

Haki zote zimehifadhiwa.

Hauruhusiwi kunakiri maandishi ya kitabu hiki bila idhini ya mwandishi.

**ISBN**: **978-9912-40-871-5**

**Designed by:**
Truth printing – Dar es Salaam

**Printed by:**

R&J Stationery

+255 754 862 677/+255 715 862 677
judyntupwa@yahoo.com
Dar es Salaam-Tanzania

# YALIYOMO


SHUKRANI.......................................................v

UTANGULIZI.....................................................7

*Sura Ya Kwanza:* SADAKA.......................................9

Maana ya Neno Sadaka...........................................9

Historia ya Sadaka............................................10

Usipende Kutoa Sadaka za Kupewa...............................11

Sadaka za Watoto..............................................12

*Sura Ya Pili:* SADAKA ISIYO YA KAWAIDA.......................14

Matukio ya Laana katika Utoaji wa Sadaka......................14

Matukio ya Baraka katika Utoaji wa Sadaka.....................15

Maana ya Sadaka isiyo ya Kawaida..............................21

Mwanzo wa Sadaka Isiyo ya Kawaida.............................22

Shuhuda.......................................................28

Utajuaje kama Sadaka Yako Siyo ya Kawaida?....................36

Je, Sadaka Isiyo ya Kawaida Lazima iwe Fungu Kubwa?...........37

Kitu Gani Husaidia Utoaji wa Sadaka Isiyo ya Kawaida?.........39

*Sura Ya Tatu:* AINA ZA SADAKA................................44

a) Aina za sadaka wakati wa agano la kale:....................44

(b) Aina za Sadaka wakati wa Agano Jipya.......................46

1. Sadaka ya Upendo (*2Korintho 8:3; 9:7*)....................46

Kiwango cha Sadaka ya Upendo..................................47

Mahali pa Kutoa Sadaka ya Upendo..............................50

Kujitoa kwa Ajili ya Watu Wengine.............................51

Mungu Mtoaji wa Mavuno:.......................................56

Mbegu ya Kupanda na Mbegu ya Mavuno:........................56
Shetani Hung'oa Mapando...........................................57
Mbegu ya Mavuno:..................................................59
Kila Apandaye Huvuna:.............................................59
2. Zaka au Fungu la Kumi.........................................60
Zaka Katika Sheria ya Musa........................................61
Zaka Katika Agano Jipya...........................................62
3. Malimbuko (Mithali 3:9-10).....................................66
4. Sadaka ya Nadhiri..............................................68
5. Sadaka ya Shukrani.............................................68
Maandalizi ya Sadaka ya Shukrani..................................69
Jinsi ya Kushiriki Katika Ibada ya Sadaka ya Shukrani.........71
Faida ya Sadaka ya Shukrani.......................................72
Upinzani Katika Kutoa Sadaka ya Shukrani.......................74
*Sura Ya Nne:* KAZI ZA SADAKA.......................................75
*Sura Ya Tano:* MSUKUMO WA KUTOA SADAKA.................79
Kwa nini Tunatoa Sadaka?..............................................81
*Sura Ya Sita:* KANUNI ZA UTOAJI SADAKA.......................89
Kwa Nini Tunatoa Lakini Hatupokei?................................89
Baadhi ya Njia za Utoaji Mzuri........................................101
HITIMISHO...........................................................110

---

## SHUKRANI

---

Kwanza kabisa kwa namna isiyoelezeka, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifanikisha kuandika kitabu hiki.

Naona kupendelewa kipekee sana kwa kupata fursa ya kutumiwa na Roho Mtakatifu katika kuandika habari za uponyaji kwa njia ya sadaka.

Pia napenda kuwashukuru wachungaji wote ambao walinipa nafasi katika makusanyiko yao hata kuniwezesha kupata nafasi ya kufundisha semina na vipindi mbalimbali katika ibada kuhusu somo la utoaji wa sadaka. Kupitia nafasi walizonipa, Roho Mtakatifu alinifunulia ufahamu wa tofauti sana kuhusu somo la utoaji. Kuna wakati nilikuwa najiandaa kufundisha mada fulani lakini nilipokuwa nasimama madhabahuni Roho Mtakatifu alikuwa ananifunulia ufahamu tofauti wa kufundisha somo la utoaji kisha baada ya kufundisha nilikuwa naandika yale ambayo Roho wa Bwana alinionesha.

Hivyo basi, kwa nafasi ya kipekee napenda kumshukuru Mchungaji wangu na baba wa kiroho, **Kundael Matee (**Mchungaji kiongozi wa kanisa la *Jesus Celebration Centre, Tanzania Assemblies of God (T.A.G)* Kimara Kilungule**)** kwa kunilea kiroho na kuniamini kwa kunipa nafasi ya kufundisha somo la utoaji kila mara nilipoomba nafasi ya kufanya hivyo. Mchungaji huyu pia amehusika kuhariri kitabu hiki pamoja na kuongeza ufafanuzi wake juu ya somo hili la utoaji. Mbali na Kundael Matee, shukrani zangu za dhati pia ziwafikie Mchungaji **Ibrahim Sabuni** wa *Jesus Ark International Ministry - Kigamboni* na Mchungaji **Zacharia Daudi** wa T.A.G *Salama Kati* ambao pia kwa nyakati tofautofauti walinilea kiroho na wamekuwa wakinipa nafasi ya kufundisha somo la utoaji kwenye makusanyiko yao.

Vilevile, napenda kuishukuru familia yangu kwa kunivumilia, kuniombea na kunitia moyo wakati wote nilipokuwa nikijibidisha katika kuandaa masomo ya utoaji kwani nilitumia muda mwingi kuandika badala ya kufurahi pamoja nao. Kipekee namshukuru mke wangu **Salome** kwa kunitia moyo na kuniombea katika huduma yangu. Kwa nyakati tofauti nimekuwa nikijitoa kwa njia ya mali za familia ili kusaidia watu

wenye mahitaji mbalimbali ilihali wao kama familia wakibaki bila kitu lakini mke wangu hakuwahi kunizuia kufanya hivyo. Pia nawashukuru watoto wangu: **Sarah**, **Sandra**, **Jayden** na **Eliana** na wadogo zangu: **Frank**, **Mbogo, Suzana** na **Dennis** Malcery kwa kunitia moyo na kuniombea katika huduma yangu. **Denis** pia alihusika katika kuhariri kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili.

Mwisho lakini siyo kwa umuhimu, nawashukuru viongozi wenzangu wa Idara ya Uanafunzi na Maandiko ambao ni ndugu **Magreth** Stephano, Elias **Mushi** na Simoni **Mshana** pamoja na washirika wenzangu wa JCC Kimara Kilungule ambao huwa wananiombea na kunitia moyo katika kuifanya kazi ya Bwana. Naamini kuwa maombi yao siyo bure kwani yamekuwa sababu kwangu mimi kufikia hatua hii kubwa ya kuandika kitabu hiki. Mbali na kitabu hiki, pia nimeweza kuandika machapisho mbalimbali ya neno la Mungu yakiwemo: Karama za Roho Mtakatifu, Ubatizo wa Maji Mengi, Kusifu na Kuabudu na Historia yenye Nguvu ya Ushindi. .

Machapisho hayo pamoja na kitabu hiki vinapatika kwenye tovuti yetu ya **www.nguvuyasadaka.com.**

# UTANGULIZI

Msukumo wa kuandika kitabu hiki ulianza mwaka 2018 baada ya kuhitimu elimu yangu ya shahada ya Umahiri ya Fedha na Uhasibu katika fani ya Mafuta na Gesi. Wakati nikifikiria kujiunga na masomo ya Shahada ya Uzamivu (PhD) ndipo Roho Mtakatifu aliponipa mzigo wa kuandika habari ya neno lake badala ya kuendelea na elimu dunia. Roho Mtakatifu alinikumbusha vitu vingi sana ambavyo Mungu amenitendea toka utotoni hadi sasa ukilinganisha na jinsi ambavyo nimejitoa kwake. Hivyo, nikapata msukumo wa kutoa sadaka ya muda wangu na elimu yangu kwa kuandika habari za Ufalme wa mbinguni ambazo zitaleta uponyaji kwa njia ya neno la Mungu.

Pamoja na kitabu hiki, pia nimeweza kuandika machapisho mbalimbali ya neno la Mungu yakiwemo: Karama za Roho Mtakatifu, Ubatizo wa Maji Mengi, Kusifu na Kuabudu na Historia yenye Nguvu ya Ushindi ambayo yanapatikana kwenye tovuti yetu ya **www.nguvuyasadaka.com**. Pamoja na kuandika vitabu hivyo, pia nimefungua tovuti hiyo na ukurasa wa You Tube ili zote kwa pamoja zisaidie kutangaza habari njema kwa njia ya mtandao ili kufikia watu wengi ulimwenguni kote.

Baraka za utoaji wa sadaka ni za kudumu na zinafuata vizazi vyako vyote. Zipo baraka utakazoziona ukiwa hai lakini zaidi sana baraka hizo zitavifuata vizazi vyako wakati wewe haupo hapa duniani. Mimi ni shuhuda wa yote haya niliyoyaandika katika kitabu hiki, nimemuona BWANA akijidhihirisha kwangu kwa jinsi ya tofauti sana kupitia huduma hii ya utoaji wa sadaka. ***Hali hii imenisukuma kutoa ushuhuda huu kwa njia ya maandishi ili na wewe upone na uweze kumwona Bwana kupitia sadaka***.

Wakati wa kutoa sadaka shetani anaweza kukuaminisha uone kuwa unapoteza mali zako, lakini naomba utambue kuwa kupitia

utoaji wa sadaka kamili mbele za Mungu, hutaishiwa, hutalala njaa, hutaaibika; **utapendeza tu**, **utang'ara tu**, **utastawi tu**, **utaongezeka sana** katika kila jambo utakalogusa mkono wako.

Hivyo basi, katika kitabu hiki utasoma shuhuda zangu binafsi na za watu wengine pia ambazo Mungu kwa nyakati tofauti aliwatendea watu wake ili iwe ushuhuda na kwako pia. Kisha Roho Mtakatifu alinipa msukumo wa kuandika yote haya ili yalete uponyaji kamili kwako kwa msaada wa Roho Mtakatifu. Naomba Mungu akuponye kwa kusoma kitabu hiki na nakuomba utoe ushuhuda kwa wengine ili nao wapone.

Ndani ya kitabu hiki nimeelezea utoaji wa sadaka **Isiyo ya Kawaida** pamoja na nguvu iliyomo ndani ya sadaka ya aina hiyo. Roho Mtakatifu alinisukuma kuandika habari za sadaka isiyo ya kawaida ili kuponya watu waliozoea kutoa sadaka ya kawaida ambayo haijaleta matokeo kwao na wamefikia hatua ya kukata tamaa na kuona kuwa utoaji wa sadaka ni hasara kwao.

Utoaji wa sadaka isiyo ya kawaida utakutoa mahali ulipo na ***kukupeleka mahali ambapo utapata matokeo halisi ya utoaji wa sadaka.*** Mungu ameahidi kutubariki kupitia sadaka lakini watu wengi bado hawajaona matunda ya utoaji wao kwa sababu wengi wao hutoa sadaka ya kawaida. Utakaposoma kitabu hiki utapata uelewa mpana juu ya utoaji wa sadaka isiyo ya kawaida na matokeo ya utoaji wa aina hiyo.

Mbali na sadaka isiyo ya kawaida, ndani ya kitabu hiki pia nimeelezea aina za sadaka na utaratibu unaofaa katika utoaji wa sadaka. Nimeelezea nafasi ya Roho Mtakatifu katika utoaji wa sadaka maana yeye ndiye kiongozi wetu katika kufanya kazi za kiroho. Utasoma pia misukumo mbalimbali inayoongoza watu katika kutoa sadaka pamoja na faida za kumtolea Mungu sadaka.

# *Sura Ya Kwanza*
# SADAKA

---

**Maana ya Neno Sadaka**

Sadaka ni kitu au fedha ambazo hutolewa na mtu kwa kuwapa wale aliowakusudia ***kama ishara ya kuwathamini na kuwapenda***. Neno **sadaka** kwa Wayahudi huitwa ***minchah,*** kiingereza huitwa ***offering.*** Neno hili la Kiyahudi linatoa maana nzuri zaidi ya neno sadaka, neno hilo limeweza kutofautisha kati ya sadaka na dhabihu (***zebah*** ni dhabihu katika lugha ya kiyahudi, katika kiingereza ni ***sacrifice***).

Tofauti hiyo inaeleza kwamba **sadaka** (minchah) ni matoleo kwa Bwana yasiyohusisha damu lakini **dhabihu** ni matoleo kwa Bwana yanayohusisha **damu**. Ndiyo maana huwezi kusema "Yesu alifanyika sadaka ya dhambi kwa ajili yetu" ingawa wengi tunasema hivyo, lakini usahihi wake ni kusema kwamba "Yesu alifanyika dhabihu ya dhambi kwa ajili yetu". Hii ni kwa sababu kujitoa kwa Yesu pale msalabani kulihusisha damu (ingawa sadaka na dhabihu ina maana moja ya matoleo na ndiyo tunayoitumia). Hivyo, **Sadaka ni kitu cha thamani kinachotolewa kwa Bwana Mungu**, ni muhimu kusema kitu cha **"thamani**" kitolewacho kwa Mungu. Yaani kwa thamani ya ulinzi, nguvu, rehema, upendo wa Mungu kwetu n.k. Bila shaka hatuwezi kutaja vitu vyote ambavyo Mungu anatutendea, hivyo basi, sadaka haitakiwi kuwa kitu dhaifu, masalia au kitu cha ziada tu bali lazima liwe fungu jema kwa sababu sadaka yenyewe hueleza mbele za Mungu jinsi tunavyompenda upitia utoaji wetu.

Sadaka inaweza kuwa kitu chochote cha thamani kama vile pesa, nguo, vyakula na vitu vingine vyovyote vile vilivyo na thamani mbele za Mungu na wanadamu pia. ***Hivyo siyo vyema kusema sadaka ni kitu chochote tu*** bali lazima kiwe chochote cha thamani kwa maana ya aina ya sadaka; kwamba ni pesa, mavazi,

mazao, vyombo vya kupazia sauti n.k. Yaani kitu chochote tu kile ambacho unaweza kukutana nacho bila kujali thamani yake hakifai kutolewa kama sadaka kwa Mungu. Kwani tunaowapenda huwa tunawapa vitu vya thamani.

**Historia ya Sadaka**

Kwa mujibu wa neno la Mungu, sadaka imebeba historia ndefu kulingana na matukio pamoja na muda. Tangu mwanzo kabla ya Torati watu walionyesha shukrani zao na kujitoa kwao kwa Mungu kwa njia ya kumtolea sadaka. Kutokana na mfumo wa zamani wa kufanya biashara nyingi bila pesa, watu wengi walitoa nafaka au mifugo yao iliyo bora zaidi kama matoleo yao kwa Mungu (***Mwanzo 4:4***). Wengine walionesha uhusiano mwema na Mungu na wanadamu wenzao ambapo mtoaji alikula sehemu ya sadaka yake katika sherehe pamoja na ndugu, rafiki na jamaa zake (***Mwanzo 31:54***).

Tukio la kwanza la utoaji wa matoleo ya hiyari mbele za Mungu tunaliona kutoka kwa *Kaini* na *Habili* **(*Mwanzo 4:3-4***); matoleo yao yalikuwa katika mfumo wa sadaka za hiyari mbele za **BWANA**. Kabla ya kuwepo kwa hekalu, kulikuwa na mahali tofautitofauti pa kutolea sadaka. Baadaye ilikuwa ni sheria kwamba sadaka zote zinapaswa kutolewa katika hekalu mjini Yerusalemu kama sehemu pekee iliyoruhusiwa na Mungu kwa ajili ya kutolea sadaka. ***Maana yake ni kuwa, sadaka haitakiwi kutolewa mahali popote tu ambapo mtu anataka bali aongozwe na Roho Mtakatifu ili atoe mahali ambapo Mungu amepachagua*** (***Kumbukumbu 12:5-7, 10-14*****).**

Katika kanisa la Mungu waumini huwa hawaendi mikono mitupu kwenye ibada, bali huenda na sadaka kama ishara ya kunyenyekea, kuthamini na kumpenda Mungu.

**Katika utoaji wa sadaka: kabla ya torati, wakati wa torati hadi wakati huu wa sasa, moyo wa mtoaji huwa ni muhimu**

**sana kuliko kiasi cha sadaka kinachotolewa.** Maana yake ni kwamba, kama mtu atatoa sadaka kubwa lakini moyoni mwake hana upendo basi sadaka hiyo inaweza isiwe na matokeo kutoka kwa Mungu. Hivyo, ni muhimu kutoa sadaka kwa upendo ndipo mtoaji atapata thawabu kwa Mungu.

Wakati wa Torati, watu waliotekeleza sherehe za sadaka za kuteketezwa kama desturi tu bila kuingiza imani na unyoofu wa mioyo yao, manabii walilaumu sadaka zao wakisema kuwa hazina maana yoyote mbele za Mungu (***Isaya 1:11-13; Amosi 5:21-22; Mika 6:6-8)***. Tunaona pia toka mwanzo Mungu hakuweka kusudi la sadaka kuwa mzigo mkubwa kwa mtoaji ili watoaji wasitoe kwa manung'uniko bali Mungu aliruhusu sadaka za aina tofautitofauti na zenye thamani tofauti ili kila mtu atoe kadri awezavyo bila kumfilisi au kuwa mzigo kwake (***Mambo ya Walawi 1:3, 10, 14; 5:6-7, 11)***. ***Hata hivyo, kwa kuwa Mungu ndiye mtoaji mkuu wa vyote, hakuna mtu anayeweza kufirisika kwa kutoa sadaka nyingi.***

**Usipende Kutoa Sadaka za Kupewa**

Sadaka inatakiwa iwe mali yako wewe mwenyewe ili iambatane na moyo wako pia ili kuonesha uthamani wa kile unachokitoa kwa Mungu ***(Kumbukumbu la Torati 12:6-7, 16:10; 2Samweli 24:21-25)***. Ukweli ni kwamba kitu cha kupewa huwa hakiumi, hivyo kinaweza kisiambatane na moyo wa mtoaji. Tukisoma katika ***Kumbukumbu la Torati 16:10,*** neno la Mungu linaeleza utoaji wa sadaka inayotokana na kuinuliwa kwa mikono yako na pia baraka nazo zitaambatana na kazi za mikono yako, hakuna habari za baraka kupitia kazi ya mikono ya mtu mwingine.

Katika ***2Samweli 24:24*** tunasoma habari za Mfalme Daudi kukataa ofa ya sadaka isiyogharimiwa kutoka kwa Arauna. Arauna alijitolea kutoa kiwanja na ng'ombe kwa ajili ya sadaka lakini Daudi alikataa kwa sababu alitambua kuwa kama angelikubali kupokea hicho kiwanja cha bure na huyo ng'ombe

basi zile baraka za kutolewa vitu hivyo, zingelienda kwa *Arauna* aliyevitoa na wala siyo kwa Daudi. Daudi alilielewa hilo na akatambua kuwa yeye ndiye mwenye maono, na Mungu alisema naye hivyo, ni lazima ahusike moja kwa moja kutii sauti ya Mungu na siyo vinginevyo.

***Wapo watu ambao Mungu amewapa nguvu na uzima, tena amewabariki katika mali lakini linapokuja suala la sadaka linaonekana kama siyo suala la mtu mmojammoja kadri ya kubarikiwa kwake bali huonekana kama la kifamilia kwa ujumla.*** Kwamba mke ambaye Mungu amempa kazi na kipato lakini kwenye sadaka anajificha kwenye koti la mume wake au mume kwenye kivuli cha mke wake. Ni kweli kuwa yapo mambo ambayo yatafanyika kwa ngazi ya familia lakini ikumbukwe kuwa kujitoa mbele za Mungu kunamhusu mtu mmojammoja. Usikae ukisubiri kuishi kwa mgongo wa baraka za mtu mwingine, kama kuna suala la kuchangia kama familia kuhusu kazi ya Mungu hakikisheni kuwa kila mtu ameweka nguvu yake katika hilo changizo sawasawa na kubarikiwa kwake.

## Sadaka za Watoto

Watoto wetu ambao bado hawajatambua jema na baya tuendelee kuwapa sadaka nzuri ili kuwajengea tabia ya kumtolea Mungu sadaka. Tuwasisitize na kuhakikisha kuwa wanafikisha sadaka yote wanayopewa na kuwasisitiza kuwa asiwepo yeyote anayepunguza sadaka kwa kununua vitu kama vile pipi na vitu vingine vinavyopendwa na watoto.

Tuwaambie kuwa sadaka ni mali takatifu ya Mungu na hivyo haitakiwi kupunguzwa kwa sababu zozote zile; na wakipunguza watakuwa wanamwibia Mungu ***(Matendo 5:1, Malaki 3:8-10)***. Zipo baraka zinazoambatana na uaminifu wao pale wanapokuwa waaminifu kufikisha sadaka yote waliyopewa na wazazi wao. Mungu anaanza kuwahesabia haki ya uaminifu toka wakiwa wadogo na hivyo kuwafanikisha katika hatua zote za maisha yao.

Vijana wanaojitambua lakini bado hawajaanza kufanya kazi za kujitegemea na ambao bado kwa kiasi kikubwa wanategemea wazazi wao, lipo jukumu la kuwaeleza kuhusu kujitegemea wenyewe kwenye suala la sadaka. Wanapopewa pesa za kujikimu katika mambo yao binafsi kwa jina maarufu '*pocket money*' au hata pesa za kula shuleni wakumbuke pia kupanga bajeti inayomhusu Mungu katika kiwango hicho cha pesa wanachopewa. Tuwasisitize kuwa wasitumie pesa yote kwenye mambo yao binafsi kisha wakaomba tena kupewa sadaka kutoka kwa wazazi wao, ***waanze kujifunza kujinyima kwa ajili ya Mungu***. Tuwaambie kuwa kwenye bajeti zao wakumbuke kuweka fungu kwa ajili ya Mungu. Hii haitahusisha pesa wanazopewa kwa matumizi ya moja kwa moja kama vile ada ya shule, nauli na matumizi mengine ya moja kwa moja kama hayo. Pesa za matumizi ya moja kwa moja wazitumie kma walivyopangiwa na wazazi wao.

## *Sura Ya Pili*
## SADAKA ISIYO YA KAWAIDA

Tokea nyakati za kale hata sasa, maandiko matakatifu yanaonesha matukio tofautitofauti ambayo yanadhihirisha kuwa suala la utoaji wa sadaka siyo la kawaida kama ambavyo imezoeleka kwa watu wengi. Waamini wengi hudhani kuwa suala la utoaji wa sadaka kamili kuwa ni la ziada tu katika safari ya wokovu. Kuwaza kwa jinsi hii siyo sahihi hata kidogo kwani wokovu wetu unapimwa pamoja na mambo mengine, jinsi tunavyojitoa kwa njia ya mali zetu kwa ajili ya kazi ya Bwana. Neno la Mungu linaonesha mambo tofautitofauti yanayodhihirisha kuwa utoaji wa sadaka unatakiwa kuchukuliwa kwa umuhimu wa pekee sana katika maisha ya watakatifu wa Bwana.

Yapo matukio katika Biblia yanayoonesha laana ambazo zilitokana na kutoa kwa udhaifu au kutotoa kabisa sadaka sawa sawa na maagizo ya Mungu. Maandiko pia yanatuonesha matukio ya uponyaji, ufufuo, maagano na pia ahadi za baraka na ustawi wa maisha ya watakatifu pale walipotoa sadaka sawa sawa na maagizo ya Mungu. Uwepo wa matukio haya ya pande mbili yanatosha kututhibitishia kuwa suala la utoaji wa sadaka siyo la kawaida tu na wala siyo la mazoea tu bali ni suala linalohitaji maandalizi pamoja na kupewa uzito unaostahili.

### Matukio ya Laana katika Utoaji wa Sadaka

Katika kitabu cha **Malaki 3:7-9,** tunaona Mungu kupitia nabii Malaki analiambia taifa la Israel kuwa limeyaacha maagizo yake kwa kutotoa zaka na sadaka iliyo kamili na kwa kufanya hivyo Mungu aliachilia laana juu ya taifa zima. Kumbe kutotoa sadaka kamili ni kuasi maagizo ya Mungu na hivyo kunasababisha mtu kupoteza mahusiano yake na Mungu. Kupata laana ni kusema kuwa mambo yako mbalimbali yakiwemo ya kiuchumi yataenda ndivyo sivyo kwa sababu ya kukosa ulinzi wa Mungu.

Katika kitabu cha **Matendo ya Mitume 5:1-11,** tunasoma habari za Anania na mkewe Safira, ambao walipatwa na mauti baada ya kumdanganya Roho Mtakatifu kwa njia ya sadaka. Kumbe tunapoahidi kutoa mbele za Bwana kisha tusipotekeleza ahadi zetu huwa hatukosei kwa wanadamu tu bali kwa Mungu na hivyo kwa kutotimiza ahadi zetu za sadaka humuhuzunisha Roho Mtakatifu kiasi cha kufa.

Katika kitabu cha **Hagai 1:2-11**, tunasoma habari za wana wa Israel waliposimama kuendelea na kazi ya ujenzi wa Hekalu la Bwana na kugeukia mambo yao binafsi. Hali hii ilisababisha Bwana Mungu kusimamisha Baraka juu ya maisha yao kiasi kwamba hakuna mtu kati yao aliyefanikiwa katika nchi mpaka wakati ule Mungu aliposema nao kupitia unabii wa Hagai.

Katika kitabu cha **Mathayo Mtakatifu 25:41-44,** tunasoma habari za wakati wa hukumu kuwa, wapo watu watakaoambiwa waende katika jehanamu ya moto kwa sababu tu hawakusaidia watu wengine walipokuja kwao wakiwa na mahitaji. Kumbe tunaposhindwa kufanyika Baraka kwa watu ambao Mungu anawaleta kwetu ni kukosa kutii maagizo ya Mungu na hivyo ipo hukumu juu yake.

Mambo yote haya yanatuonesha jinsi ambavyo kutoa sadaka katika hali ya udhaifu au kupuuza suala la utoaji wa sadaka ni sawasawa na kukosa magizo ya Mungu. Hivyo tunapata picha kuwa sadaka siyo jambo la kawaida lakini pia tunaona kuwa ipo nguvu ya kiroho ndani ya utoaji wa sadaka iliyo kamili mbele za Bwana.

**Matukio ya Baraka katika Utoaji wa Sadaka**

Hapo awali tumeona laana zinazoambatana na utoaji hafifu wa sadaka. Sasa tuangalie upande mwingine ambapo tutaona baadhi ya maandiko ambayo yanatudhihirishia kuwa utoaji ulio kamili ni chanzo cha Baraka zisizo za kawaida.

Katika kitabu cha **Malaki 3:10-12,** Mungu anatuonesha jinsi ambavyo anaweza kutubariki kupitia utoaji wa sadaka kamili mbele zake, anataja siyo tu Baraka lakini pia anataja aina za ulinzi anaoachilia juu yetu tunapotoa kwa ukamilifu. Hakuna mtu kati yetu anayeweza kujua wala kutabiri mambo mabaya ambayo adui amepanga juu ya kazi zetu, afya zetu n.k bila msaada wa Mungu. Lakini kupitia sadaka Mungu anaahidi ulinzi wa kila namna juu yetu na mali zetu. Ni kweli kuwa, kupitia maombi tunaweza kukemea sana hila za adui juu ya maisha yetu, lakini kupitia utoaji sahihi wa sadaka Mungu yeye mwenyewe anaahidi kukemea kwa niaba yetu.

Katika kitabu cha **Mathayo 25:34-40**, tunasoma habari za watu waliotenda wema kupitia utoaji wa sadaka kwa watu wengine. Tunajifunza kwamba, tunapofanyika Baraka kwa watu ambao Mungu huwaleta kwetu huwa tunamfanyia Mungu na hivyo tunahesabiwa haki ya kuurithi ufalme wa mbinguni. Maandiko yanaonesha itakuwa mshangao mkubwa sana pale Yesu atakaposema njoo kwangu maana wakati nilipokuwa na njaa ulinilisha na nilipokosa mavazi ulinivalisha. Kumbe yote tuyafanyayo kupitia utoaji ulio kamili huwa tunafanya kwa Bwana naye ametuandalia taji la uzima.

Katika kitabu cha **Matendo ya Mitume 10:31-31**, tunsoma habari za Kornelio ambaye kupitia sadaka alizokuwa anatoa, Mungu alimtuma malaika kuja kwake kwanza kumthibitishia kuwa utoaji wake unakumbukwa mbele za Mungu lakini pia kupitia kumbukumbu hiyo Mungu akamwelekeza njia sahihi ya kuurithi ufalme wa mbinguni. Tunajifunza kuwa sadaka tuzitoazo kwa uaminifu zina nguvu ya kutuombea rehema kwa Bwana, Kornelio alipata rehema hii kupitia utoaji wake.

Katika kitabu cha **Matendo ya Mitume 9:36-39,** tunasoma habari za Dorkasi amabaye alipata rehema ya ufufuo kupitia utoaji mzuri wa sadaka. Yeye alikuwa anatoa kwa wajane na baada ya kifo chake wajane walisimama wakionesha sadaka za Dorkasi juu ya

maisha yao. Hapa ni kusema kwamba sadaka za Dorkasi zilisimama kupinga kifo chake na hatimaye Dorkasi alifufuliwa.

Katika kitabu cha **Mwanzo 8:20-22,** tunaona nguvu ya sadaka aliyotoa Nuhu baada ya gharika. Hivyo Mungu kutokana na uzuri wa sadaka ile aliahidi kutoipiga tena dunia kwa gharika.

Katika kitabu cha **Mwanzo 22:16-18**, hapa tusoma jinsi ambavyo Mungu anamwapia Ibrahimu juu ya Baraka zisizo na kipimo ambazo Ibrahimu anaapiwa na Mungu kupitia utoaji ambao haukuwa wa kawaida pale Ibrahimu alipokubali kumtoa mwanae wa pekee awe sadaka ya kuteketezwa sawasawa na maagizo ya Mungu.

Katika kitabu cha **1Wafalme 17:12-16**, tunasoma habari za mama mjane wa Shunemu ambaye alijitoa kwa mtumishi wa Mungu Eliya. Baada ya mama yule kujitoa tunaona anapona katika njaa kali ya kipindi cha miaka mitatu na nusu. Utoaji wa huyu mama haukuwa wa kawaida maana alikuwa anapita katika kipindi kigumu sana lakini hakusita kutii sauti ya Mungu ilipomtaka amlishe Eliya. Naye Mungu hakubaki kimya baada ya sadaka ile.

Katika kitabu cha **2Wafalme 4:8-17,** tunasoma habari ya mama ambaye alikaa muda mrefu bila kupata mtoto lakini akapata mtoto baada ya kutoa sadaka iliyompendeza Mungu. Tunaona jinsi ambavyo huyu mama alivyojitolea kumtambulisha Elisha mbele za mume wake, siyo jambo rahisi mtu mke kumpeleka mtu wa jinsi tofauti kwa mume wake lakini huyu mama aliweza. Kujitoa kwake hakukupita bure. Tunajifunza kuwa yapo majibu ya maombi yetu yanayosubiri tujitoe kwa Bwana kikamilifu kisha tutapokea mahitaji yetu.

Katika kitabu cha **Marko 14:9,** tunasoma utoaji wa sadaka yenye thamani nyingi sana ambayo Mariamu alitoa kwa Yesu. Sadaka hii inaonekana kumpedeza Yesu na akatamka neno juu ya Mariamu. Tunajinza kuwa kumbe sadaka inaweza kusababisha

Mungu kusema jambo juu ya maisha yako**. *Watu wengi leo hii huenda kwa manabii ili watamkiwe neno la Baraka juu ya maisha yao, siyo vibaya kutamkiwa neno la Baraka kutoka kwa watumishi wa Mungu. Lakini kumbe kupitia sadaka yako, Mungu mwenyewe atatamka neno la Baraka juu ya maisha yako*.**

Katika kitabu cha **Mithali 3:9-10,** tunasoma kuwa kutoa sadaka ni ishara ya kumheshimu Mungu. Mali zetu zinaweza kutumika kumheshimisha Mungu. Watu hutamka katika midomo yao kuwa wanamheshimu Mungu lakini kumbe ipo heshima kupitia mali zetu na heshima hii imebeba ahadi za Baraka kutoka kwa Bwana.

Katika kitabu cha **Marko 12:42-44,** tunaona Yesu anavyoifurahia sadaka ya mama mjane ambaye alitoa sadaka ndogo sana machoni pa wanadamu lakini ilikuwa kamilifu machoni pa Bwana. Hapa tunajifunza kuwa, kumbe wakati wa utoaji wa sadaka Yesu huwa yupo na huwa anachunguza sadaka zetu. Kila mmoja wetu naamini angetamani Yesu aifurahie sadaka yake na ni hakika kwamba, kama sadaka ikitolewa kwa ukamilifu Mungu huwa anaifurahia na kutamka neno juu ya hiyo sadaka.

Katika kitabu cha **2Mambo ya Nyakati 31:10,** tunaona habari za Azaria kuhani akieleza jinsi ambavyo watu wa Mungu walivyobarikiwa pale walipoanza kutoa sadaka nyumbani mwa Bwana. Inawezekana hapo awali watu hao hawakutoa kikamilifu lakini walipoanza kutoa kikamilifu waliziona Baraka za Bwana. ***Wapo watu siku hizi wanajisikia wivu kutoa sadaka nzuri eti kwamba zitaliwa na wachungaji***. Kupitia kusoma kitabu hiki naomba utambue kuwa kama mchungaji wako anaishi kwa taabu kwa sababu unaona vibaya kufanyika Baraka kwake, uwe na uhakika kuwa Baraka zako zitachelewa sana mpaka pale utakapofunguka kama hawa wana wa Israel walivyofunguka wakajitoa kwa watumishi wa Mungu kisha Baraka zikamiminika kwao.

Hiyo ni baadhi tu ya mifano inayoonesha ni jinsi gani sadaka imebeba nguvu na hivyo utoaji wa sadaka hautakiwi kuchukuliwa kama jambo la kawaida tu. Tumeona uthibitisho wa jinsi ambavyo sadaka isivyo jambo la kawaida mbele za Mungu tofauti kabisa na hali ya watu kutoa sadaka ama kitu chochote tu tena kwa mazoea katika ibada. ***Kutokana na mazoea ya kuchukulia utoaji wa sadaka katika hali ya kawaida, hali hii imesababisha sadaka inayotolewa kanisani nyakati hizi kuitwa sadaka ya kawaida badala ya sadaka ya upendo kwa Mungu.*** Kwa bahati mbaya sana hilo neno la ukawaida limeenda hadi likazama mioyoni mwa watoaji hatimaye wanatoa sadaka ya kawaida kabisa madhabahuni pa Bwana bila hofu yoyote.

Watoaji wengi huonekana kujitoa kwa kiasi kikubwa kama kuna tukio fulani kanisani hususani matukio ambayo yanaonekana machoni pa watu. Matukio hayo yanaweza kuwa ni pamoja na msiba, sherehe za harusi au ahadi za ujenzi. Ni jambo jema tena lenye baraka kwa washirika wa mahali pamoja kujitoa kwa ajili ya mambo ya misiba, magonjwa, ujenzi, sherehe na mambo kama hayo yanapotokea maana tumeagizwa kupendana sisi kwa sisi **(Yohana 13:34-35; Galatia 6:9-10**).

Hata hivyo, bado swali linabaki kuwa kwa nini watu wengi hujitoa kwa baadhi ya mambo tu, hasa yale yanayoonekana machoni pa watu wakati watu haohao wanapotoa sirini hutoa sadaka dhaifu? Je, pengine hali hii hutokea kwa sababu michango ya aina hii huwa ni ya wazi ndio maana watu huahidi kiasi kikubwa ili waonekane machoni pa watu? Bila shaka jibu la maswali haya yote utalipata kwa msaada wa Roho Mtakatifu baada ya kusoma kitabu hiki chote.

Haina maana kuwa kila siku ya ibada watu watoe kama wanavyoahidi kwenye michango mingine bali ni vizuri kuzingatia siku zote kuwa na uwiano mzuri wa sadaka zitolewazo madhabahuni kulingana na jinsi ambavyo Mungu alivyokubariki tena katika hali ya kujitoa kusiko kwa kawaida na bila kuhesabu

umetoa mara ngapi. Huduma ya madhabahuni haina matukio maalumu kwani kinatakiwa kiwepo chakula ghalani mwa Bwana siku zote.

Nyakati hizi ni mara chache sana kusikia sadaka inayotolewa Kanisani kuitwa sadaka ya upendo kwa sababu ama ya mazoea au kwamba wakiita hivyo itawachoma mioyoni mwao. Ikiitwa sadaka ya upendo itakuwa rahisi kutambua kuwa sadaka waliyoandaa mikononi mwao ni duni na wala haiendani na upendo wa Kristo maishani mwao kwani inajulikana kuwa kitu kinachobeba upendo hakiwezi kuwa cha kawaida tu. Hivyo, nyakati hizi utasikia watumishi wengi mara nyingi wanasema "sasa tunaenda kutoa sadaka ya kawaida".

Mfano mzuri wa ishara ya vitu vya kuonesha upendo ni pete ya uchumba ama pete ya ndoa itolewayo na mwoaji. Hivi vitu vimekuwa vikioneshwa madhabahuni kuwa ni kweli vinafanana na kuwa ***ishara ya upendo kwa mwenza kwa sababu ya thamani yake.*** Lakini kwa bahati mbaya sana siku hiyo ya uchumba au ndoa ukihesabu sadaka iliyotolewa kwa Mungu ambaye ndiye atakayelinda hiyo ndoa au uchumba, utaona kuwa ni sadaka ya kawaida kabisa. ***Wanadamu wanafanya maandalizi ya mambo yao binafsi ili yapendeze lakini hawafanyi maandalizi yoyote kwa ajili ya kazi ya Bwana.***

Tunaonesha unafiki wa upendo machoni pa wanadamu tunaposimama na kumshukuru Mungu kwa midomo tu lakini mioyo yetu ipo mbali na Mungu **(*Mathayo 15:7-9)***. Tumebaki kutamka upendo wetu kwa Mungu kwa midomo tu lakini mioyo yetu ipo mbali kabisa. ***Hii haimaanishi kuwa mtu atoe sadaka sawa au zaidi ya thamani ya pete ya ndoa au uchumba lakini kama kwa wanadamu tunaweza kutoa vitu vizuri zaidi, ugumu unapatikana wapi kutoa vitu vyema kwa Mungu wetu***. Kama vile tunavyokuwa na mzigo kusimamia na kuandaa mambo yetu kwa ufanisi, vivyo hivyo tunatakiwa kufanya kwa ajili ya Mungu. Hivyo sadaka zetu zinatakiwa kuwa na maandalizi ya kutosha ili

zipate matokeo sahihi. ***Maharusi wengi huwa wanajiandaa kwenda kanisani kufunga ndoa lakini huwa hawaandai sadaka ya kutoa siku ya harusi.***

Kutokana na hali hii dhaifu katika utoaji wa sadaka, ndipo Roho wa Bwana akanipa mzigo moyoni mwangu kuandika habari za utoaji wa sadaka isiyo ya kawaida. Kwa ujumla, katika sehemu hii ya sadaka isiyo ya kawaida nitaongelea utoaji wa sadaka ya upendo ambayo inapotolewa kwa uaminifu inakuwa siyo sadaka ya kawaida mbele za Mungu na hivyo kusababisha Mungu aseme jambo juu yako.

**Maana ya Sadaka isiyo ya Kawaida**

Neno kawaida lina maana ya kufanya jambo kwa mazoea. Kitu kisicho cha kawaida ni kitu kinachofanyika katika hali isiyo na mazoea, yaani katika hali ya tahadhari na kwa uangalifu unaostahili. Hivyo sadaka isiyo ya kawaida ni sadaka inayoambatana na mguso kutoka moyoni mwa mtoaji mwenyewe kwa kutambua ukuu wa Mungu anayemtolea sadaka. Siyo sadaka inayotolewa katika hali ya mazoea na isitoshe sadaka hii inagusa moyo wa anayeipokea pia. Hii ni sadaka isiyotolewa katika hali ya mazoea au kutimiza wajibu tu bali hutolewa katika hali ya ***maandalizi yanayozingatia ukuu wa Mungu aliye mbinguni***. Inatolewa katika hali ya kumtambua na kumthamini Mungu unayemtolea.

**Mfano wa sadaka isiyo ya kawaida**: Je, umewahi kumsaidia mtu jambo fulani kisha huyo mtu akashindwa aseme maneno yapi ya kushukuru, badala yake akaanza kutoa machozi hata wewe uliyetoa msaada huo ukaguswa kiasi kwamba wote mkajikuta mnalia badala ya kufurahi? huo ndiyo mfano mzuri sana wa sadaka isiyo ya kawaida, ***kujitoa kusiko kwa kawaida mbali ya kugusa moyo wa aliyepokea lakini pia ni lazima itagusa moyo wa mtoaji pia***. Ni sadaka inayomgusa Mungu kiasi cha kusababisha aseme jambo la kipekee juu ya maisha ya mtoaji wa

sadaka hiyo. Hivyo, tunasema ni sadaka isiyo ya kawaida kwa sababu wakati mwingine utajikuta unatakiwa kutoa sadaka katika mazingira ambayo kibinadamu siyo rahisi na hayaruhusu kabisa. Kuna wakati unaweza kuwa unapitia hali ya kuishiwa kabisa lakini wakati huohuo Mungu anaweza kusema na wewe kujitoa kwa ajili ya kazi yake au watu wengine.

**Mwanzo wa Sadaka Isiyo ya Kawaida**

Chimbuko la utoaji wa sadaka isiyo ya kawaida ni Mungu mwenyewe pale alipomtoa Yesu Kristo mwana wa pekee ili aje duniani na kufa kwa ajili ya kubeba dhambi zetu (***Yohana 3:16***). Jaribu kubwa la sadaka ya namna hii kwa mwanadamu alipewa mtumishi wa Mungu Ibrahimu pale alipoambiwa na Mungu amtoe Isaka mwanaye wa pekee kuwa sadaka ya kuteketezwa (***Mwanzo 22:1-2***). ***Utoaji wa jinsi hii ambao Mungu kumtoa Yesu Kristo na Ibrahimu kumtoa Isaka unaonesha kuwa suala la utoaji wa sadaka ni lazima litoke moyoni tena katika hali ya upendo mkuu sana***.

Hapa tunapata maana ya utoaji wa sadaka isiyo ya kawaida tofauti na utoaji wa sadaka ya kawaida ambapo mtoaji anakuwa hajafungamanisha moyo wake katika sadaka anayotoa. Yaani mtoaji anatoa ili aonekane ameshiriki tu lakini siyo katika mzigo wa utoaji. Haina maana kuwa ili tutoe sadaka isiyo ya kawaida mbele za Bwana inatubidi tutoe watoto wetu ili wawe sadaka za kuteketeza, bali tunaweza kujitoa kwa jinsi hiyo kupitia mali zetu.

Katika utoaji wa kawaida mtu hutoa kama kutimiza jukumu fulani tu lakini hakuna moyo wa ibada unaoambatana na utoaji huo. Hali hii hutokana na sababu kadha wa kadha zikiwemo:

(i) Pengine mtoaji hajui sababu za kumtolea Mungu sadaka nzuri (kukosa uelewa sahihi wa utoaji hasa kutokana na watu wengi kuzoea kusema toa chochote ulichonacho)

(ii) Mtoaji anajua sababu za kumtolea Mungu lakini amezoea kutoa kwa mazoea tu (kukosa msukumo wa ndani ya moyo kuhusu sadaka).

(iii) Hali ya mtu kupungukiwa moyo wa ibada kamili mbele za Mungu na hivyo kusababisha mtu kutoa bila kujali. Moyo wa ibada siyo tu kuhudhuria kanisani lakini pia ni muhimu zaidi kwenye maandalizi ya kuhudhuria katika ibada. Maandalizi yako katika ibada yanahusisha kujitakasa wewe mwenyewe pamoja na kuandaa sadaka utakayomtolea Mungu. Maandalizi ya sadaka ni muhimu sana kwa sababu sadaka yako imebeba upendo wa moyo wako mbele za Bwana. kwa hiyo, lazima iwe na maandalizi mazuri. Ibilisi naye anajua baraka za mtoaji zinaambatana na utoaji ulio kamili mbele za Bwana, hivyo ni rahisi kumfumba macho mtoaji ili asitoe ipasavyo na hivyo kukosa baraka zitokanazo na utoaji.

Yapo makundi mawili ambayo mtu anaweza kutoa sadaka isiyo ya kawaida:

A. **Kundi la Kwanza: Sadaka inayotolewa kutokana na kusikia na kutii maelekezo (sauti) ya moja kwa moja kutoka kwa Mungu (kufuata mwongozo wa Roho Mtakatifu)**.

Katika kutoa sadaka ya kumpendeza Mungu, mara nyingi Roho Mtakatifu huwa ananena na mtoaji kumwelekeza kuhusu aina fulani ya sadaka na aitoe sehemu gani. Kusikiliza na kutii sauti hiyo huwa kunampendeza Mungu kwa sababu mtoaji hutoa kama Mungu alivyokusudia. Hali hii husababisha Mungu kuachilia baraka zisizo za kawaida kwa mtoaji kwa sababu ya kutimiza kusudi la Mungu. ***Ipo nguvu kubwa ndani ya utoaji wa sadaka ya namna hii kwa maana Mungu huwa hanyamazi juu ya mtu anayetoa kwa jinsi hii.***

Katika kundi hili ipo mifano mbalimbali ya utoaji kama vile:

1. ***Ibrahimu ambaye alisikiliza na kutii sauti ya Mungu ya kumtoa dhabihu mtoto wake wa pekee aitwaye Isaka (Mwanzo 22:1-18)***. Mahali hapa tunaona kuwa Mungu anambariki Ibrahimu si tu kwa sababu alikubali kutoa sadaka ya mwanaye lakini pia katika mstari wa **18** tunaoneshwa kuwa Mungu anamfurahia Ibrahimu kwa kutii sauti yake.

   Naamini umewahi kusikia sauti ya Mungu akikuelekeza kufanya jambo fulani la utoaji iwe ni kanisani kwako, kwa watumishi wa Mungu au kwa wahitaji mbalimbali. ***Hata hivyo ni wachache tu huwa wanatii sauti kama hizo na watu hawa ndio wanaoziteka baraka za Mungu, hawa ndio wanaoshudia nguvu iliyomo ndani ya sadaka***. Mara nyingi pale unaposikia sauti kama hiyo Shetani huja mara moja na kuiondoa (***Marko 4:15***) hata kukufanya ushindwe kuiona nguvu ya sadaka.

   Shetani anajua kuwa kama ungetii sauti ya Mungu ungebarikiwa isivyo kawaida hivyo utasikia sauti inayokwambia: ***'kila mtu apambane na hali yake, nitasaidia wangapi, kila mtu atakula kwa jasho lake n.k.***

   Utoaji ni sehemu ya ibada takatifu ya Mungu, hivyo mtoaji anatakiwa kuongozwa na Roho Mtakatifu ili utoaji wake umpendeze Mungu. Mtumishi wa Mungu aitwaye Musa, anawakumbusha wana wa Israel kuhusu baraka zinazoambatana na kusikia na kutii sauti ya Mungu **(*Kumbukumbu 28:1-13).*** *Kati yetu yupo Roho Mtakatifu ambaye moja ya kazi yake ni kutukumbusha kuyashika maagizo yote ya Mungu. Hivyo atatukumbusha ili utoaji wetu uwe wa kupendeza mbele zake*. **Tukitoa kwa mwongozo wa akili zetu tu itakuwa**

***vigumu kumpendeza Mungu kwa sababu mara nyingi tutajikuta tunatoa kwa rafiki au ndugu zetu tu ili watusifu na kutupa heshima za kibinadamu.***

2. ***Mwanamke mjane wa Sarepta ambaye aliandaliwa na Mungu kumpokea na kumlisha Eliya***. Huu haukuwa utoaji wa kawaida, kama umewahi kupitia katika vipindi mbalimbali vya ukame na njaa utakubaliana na mimi kuwa watu huwa hawataki hata kutembelewa na ndugu au wageni. Wakitembelewa na wageni huwa wanadiriki hata kuficha chakula uvunguni wakisubiri kula baada ya wageni kuondoka.

   Lakini huyu mwanamke alikubali, akatii na kuamua kumlisha Eliya huku akijua kabisa kufanya hivyo kungesababisha yeye na watoto wake kufa njaa. *Mwanamke huyu aliona nguvu ya sadaka aliyotoa kwani kujitoa kwake ndiyo ilikuwa sababu iliyompelekea kula na kusaza katika kipindi chote ambacho kulikuwa na njaa kali katika Nchi ile* ***(1Wafalme 17:9-16).*** Fikiria kama huyu mwanamke asingetii sauti ya Mungu, bila shaka angekufa katika janga lile la njaa.

   Watu wangapi mambo yao yamekufa kwa sababu hawakuwa waaminifu katika kutii sauti ya Mungu? Watu wangapi wamekuja kwako kwa maelekezo ya Mungu ili uwasaidie lakini walipofika kwako ukatoa sababu kadha wa kadha wakarudi mikono mitupu? Haimaanishi kwamba kila mtu anayekuja kwako kuomba msaada huwa ametumwa na Mungu lakini ujue kwamba wapo watu wanaokuja kwako kwa maelekezo ya Mungu.

Hivyo, ni vyema kumuomba Mungu ili upate roho ya utambuzi wa maelekezo au sauti ya Mungu ili utoaji wako umpendeze Mungu.

Mtume Paulo anawaombea watu wa Efeso kupata utambuzi wa Rohoni ili wazione baraka za Mungu. Ni lazima tuwe na utambuzi wa Rohoni ili tujue na kuyatenda mapenzi ya Mungu (***Waefeso 1:17-18***). *Kama umempokea Yesu kuwa ni Bwana na mwokozi wa maisha yako na pengine bado hujajazwa Roho Mtakatifu inabidi usikae ukaona ni kawaida tu. Jenga shauku na uhakikishe umejazwa Roho Mtakatifu. Kama tayari umejazwa Roho Mtakatifu lakini huna utambuzi wa jinsi ambavyo Mungu husema na wewe kupitia Roho Mtakatifu basi jitahidi kutafuta uso wa Bwana kwa kumwomba akupe uwezo wa kutambua sauti yake*.

3. **Mariamu ndugu yake Lazaro**: Sadaka ya Mariamu haisemwi moja kwa moja kama ni kuitii sauti ya Mungu lakini ukisoma vizuri unaona Yesu anaifurahia sadaka ile kwamba imetangulia ili itumike katika maziko yake (***Yohana 12:1-9)***. Hii inaonesha kuwa huyu mwanamke pengine alipewa ufunuo wa kufanya jambo ambalo lilitakiwa kufanyika wakati wa maziko ya Yesu Kristo. Kwa utii wake tunaona Yesu Kristo anasema sadaka yake itakumbukwa wakati wote Injili itakapokuwa inahubiriwa.

   Hapa tunaona kuwa utoaji wa sadaka isiyo ya kawaida lazima usababishe jambo la baraka kwa mtoaji ***(Marko 14:3-9*****).** Mariamu alitoa sadaka yenye thamani kubwa sana ambayo ilisababisha watu kama vile Yuda kunung'unika.

   Hata leo wapo watu wanaonung'unika kwa nia ya kuwakatisha tamaa watoaji pale wanapoona watu

wanajitoa mbele za Mungu kwa matoleo yasiyo ya kawaida. Ikiwa kama umesikia sauti ya Mungu inayokutaka ufanye hivyo usiruhusu kusikia tena sauti za wanadamu kwa sababu wao hawajui Mungu amesema nini moyoni mwako. ***Pia hii inaonesha kuwa Mungu wakati mwingine anaweza kukujaribu katika hali isiyo ya kawaida kwa kukutaka utoe vitu vikubwa japo haiwezi kuwa nje ya uwezo wako***. Utoaji huu unaweza kutokea mara moja au Mungu akawa anasema na wewe mara kwa mara katika kumtolea sadaka isiyo ya kawaida.

**Ushuhuda**: *Yupo mtu mmoja ambaye alijenga nyumba kadhaa kwa ajili ya kupangisha, nyumba zilipokamilika zilikaa kwa kipindi cha zaidi ya miezi mitatu (3) bila wapangaji, baadaye Mungu alimpa mwenye nyumba mzigo wa kufanya jambo fulani kanisani kwao. Alipotafakari aliona kama vile ile kazi ingelimgharimu pesa nyingi, hivyo akaamua kushirikisha baadhi ya watu pale kanisani ili wasaidiane katika gharama. Kila mtu alitoa sababu zake za kukosa pesa na wengine wakasema labda hilo jambo lifanyike miezi kadhaa ijayo. Yule mtu akaendelea kupata msukumo wa kufanya ile kazi, hivyo akaamua kutafuta pesa na kuanza kufanya ile kazi kwa gharama zake peke yake. Siku tu kazi aliyoagizwa na Mungu ilipokamilika, anasema wapangaji wa zile nyumba walipatikana siku hiyohiyo na anasema waliendelea kuja watu wengi wakihitaji kulipia ili waishi pale. Jambo lililomshangaza ni kwamba zile nyumba zilikuwa zimekaa muda mrefu bila wapangaji, iweje baada ya kufanya ile kazi kanisani watu waje kwa wingi kiasi kile!!*

***Naomba utambue kuwa yapo majibu ya maombi yako ambayo yanahitaji wewe kusikia na kutii sauti ya Mungu katika kumtoleo sadaka***. Yapo mambo ambayo Mungu anaposema na wewe ni kwamba anataka ufanye peke yako ndiyo maana unaona huyu mtu Mungu alikusudia kumwinua yeye mwenyewe hata aliposhirikisha watu wengine hawakuwa tayari kushiriki.

Haimaanishi kwamba kila jambo utafanya peke yako lakini yapo mambo ya kushirikisha watu wengine na yapo ambayo Mungu anataka ufanye wewe mwenyewe.

***Roho Mtakatifu atakuelekeza mambo ya kufanya peke yako na ya kushirikisha watu wengine. Kama atataka kushirikisha watu wengine, uwe na uhakika kuwa yeye mwenyewe atakuchagulia watu wa kushirikiana nao na siyo wale utakaowachagua wewe kwa akili zako***. Tukiangalia habari za Nehemia katika ***Nehemia (2:7-8)*** na Ezra katika ***Ezra (1:3-4)*** tunapata mpango wa Mungu wa kushirikisha watu wengine kwa ajili ya kazi yake.

**Shuhuda**

**Pitia ushuhuda wangu binafsi, naamini kuna kitu utajifunza**

Safari yangu ya elimu ilikuwa ngumu mno lakini kuna wakati Mungu aliniandalia njia kupitia utoaji wa sadaka bila mimi kujua. Kibinadamu lilikuwa ni jaribu gumu sana kwangu kutokana na mazingira niliyokuwa napitia kuamini kwamba ningeweza kufanyika baraka kwa mtu mwingine, haikuwa rahisi kabisa. ***Baada ya kupitia ushuhuda huu utaelewa kuwa bila kujali hali ya mtu kiuchumi, kila mtu ana nafasi sawa na mwingine katika kumpendeza Mungu kwa njia ya sadaka isiyo ya kawaida.***

Mara baada ya kuhitimu masomo yangu ya kidato cha nne, nilipata nafasi ya kufundisha katika shule ya Sekondari ya Salama kama mwalimu wa kujitolea, pale shuleni nilimkuta mwalimu mmoja ambaye alikuwa anaishi na kijana mmoja (jina la huyo kijana aliitwa DAUDI) aliyekuwa hajiwezi kiuchumi. Yule kijana alikuwa ni yatima, alikuwa analelewa na bibi yake katika kijiji kimoja huko wilayani Bunda mkoani Mara. Bibi yake alikuwa akisaidiwa na mjomba wake ambaye alikuwa anaishi Musoma mjini. ***Jambo la kushangaza ni kwamba yule mwalimu alikuwa ni jirani yake na huyo kijana huko kijijini kwao, pia alikuwa na uwezo zaidi yangu wa kukaa naye na kumsaidia kuliko mimi***

***badala yake akaniomba na kunisihi sana nimchukue yule kijana ili niishi naye.***

Nakumbuka nilimwambia yule mwalimu kuwa mimi nitamsaidia vipi ukizingatia hali niliyokuwa nayo lakini yeye akaona mimi naweza kumsaidia yule kijana kuliko yeye. Wakati bado najiuliza nitamsaidiaje, yule mwalimu akawa tayari amemrudisha yule kijana nyumbani kwao, hali hiyo ilipelekea mahudhurio ya yule kijana kuwa hafifu sana shuleni kutokana na umbali kati ya nyumbani kwao na shuleni lakini pia, mazingira magumu ya nyumbani kwao.

Nilichukua uamuzi wa kwenda kuomba ruhusa kwa bibi yangu ili aruhusu yule kijana aje aishi pale nyumbani, nilijaribu kumshawishi bibi yangu naye akaweza kukubali. Hivyo, yule kijana akaanza kuishi pale nyumbani kwetu katika chumba kimoja, kitanda kimoja na mimi. Ukitazama haya mazingira utaona kuwa nilikuwa na kila sababu ya kukataa kuishi na huyo kijana, Kwanza mimi mwenyewe nilikuwa naishi kwa wazazi siyo kwangu, mazingira ya nyumbani yalikuwa ni magumu isitoshe mimi nilikuwa mwalimu ambapo ilikuwa siyo heshima mwalimu kuishi katika chumba kimoja na mwanafunzi wake hata kama alikuwa wa kiume. Hata hivyo, sikuyatazama yote hayo nikaamua kuishi naye tu.

Baada ya yule kijana kuanza kuishi pale nyumbani taarifa zilimfikia mjomba wake ambaye alikuwa anaishi Musoma mjini, kwamba mpwa wake anaishi na mwalimu. Mjomba wake alishangaa sana kuona mtu mwenye upendo kiasi gani wa kuamua kuishi na mtu asiyemjua. Hivyo, akapanga safari ya kuja mpaka hapo nyumbani kwetu, alipofika alifurahi sana na kushangaa pia. Alinikaribisha nyumbani kwake Musoma, nakumbuka nilimwambia kuwa kwa sasa sina ratiba ya kuja huko lakini katika uchaguzi wa shule za kidato cha Tano, miongoni mwa shule nilizochagua ni shule za huko Musoma hivyo endapo nitafaulu na kufanikiwa kuchaguliwa kujiunga na shule mojawapo huko

Musoma basi yeye atakuwa mwenyeji wangu. Tukaachana na mjomba wake Daudi akarudi Musoma.

Muda mfupi baadaye matokeo ya kidato cha nne yakatoka na baadaye nikachaguliwa kujiunga na shule ya sekondari ya Musoma. Kusema kweli ule ulikuwa ni muujiza kwangu, nilipata sehemu ya kufikia mimi na rafiki yangu. Wakati wote tuliishi pale kama watoto wa familia moja, nikiugua nilikuwa naenda kutibiwa bure (huyo mjomba alikuwa na maabara na duka la dawa), tukichoka kula maharage shuleni tunaenda pale tunapewa dagaa na samaki, tukiishiwa maji ya kunywa (pale shuleni maji yalikuwa machafu sana hivyo tulikuwa tunaenda na maji masafi ya kunywa kutoka nyumbani) tunaenda pale tunajaza vigaloni vya maji, wakati wa likizo fupi au sikukuu nilikuwa sihitaji kusafiri kurudi nyumbani nilikuwa nabaki hapo. ***Yaani Mungu aliniandalia sehemu ambayo ilikuwa ni nzuri zaidi ya nyumbani kwani nyumbani kwetu hakukuwa na vitu vizuri kama pale. Katika hali ya kawaida usingeweza kuamini kuwa yule kijana na hali ya umaskini aliyokuwa nayo, alikuwa amebeba baraka zangu kiasi kile.*** Hivyo, tutambue kuwa ipo nguvu ndani ya sadaka isiyo ya kawaida. Kwangu binafsi, kwa wakati ule kuamua kuishi na yule kijana ilikuwa ni kujitoa kusiko kwa kawaida na mavuno yake hayakuwa ya kawaida katika maisha yangu.

## KISA KINGINE

***Huu ni mwendelezo wa ushuhuda kuwa tunaweza kumpendeza Mungu kwa njia ya sadaka bila kujali hali zetu kiuchumi.***

Wakati nakakaribia kumaliza mitihani ya kidato cha sita nilipigiwa simu na binamu yangu akaniomba na kunisihi sana nitakaporudi nyumbani nimsaidie kuishi na kijana mmoja anaitwaye Lukas Christopher. Binamu yangu aliniambia kuwa “kijana huyo alikuwa anaishi na baba yake (mama yake ni marehemu) lakini baba yake hakuwa tayari kumsomesha”. Huyo binamu yangu alikuwa ameolewa; hivyo, walikuwa wanaishi

nyumba moja na Lukas, muda wa pango ulipoisha Lukas akashindwa kulipia pango, baba mwenye nyumba akamfukuza. Binamu yangu alijaribu kumkaribisha aishi naye lakini mume wake hakutaka, hivyo Lukas akawa analala nje kwenye varanda ya nyumba, hakuwa na godoro wala shuka la kujifunika, wakati wa kulala alikuwa anajifunika jaketi ambalo lilikuwa limechanika.

Wakati huohuo nilikuwa nimepigiwa simu na mwalimu mkuu wa shule ya Sekondari ambayo Lukasi alikuwa anasoma. Niliwahi kufundisha shuleni hapo kipindi nimehitimu masomo ya sekondari kidato cha nne. Mwalimu mkuu aliniomba kuwa nikimaliza mitihani yangu nisiende sehemu nyingine kufundisha bali nirudi pale pale kufundisha.

**Nilikutana na Lukas kwa Muujiza**

Mara tu niliporejea kijijini kwetu nilianza kazi ya kufundisha, ilikuwa ni siku chache tu tangu nifike hapo kijijini na nilikuwa hata sijaenda kumtembelea huyo binamu yangu ili nifahamu vizuri ombi lake la kutaka nimsaidie Lukas. Siku moja nilikuwa natoka mahali fulani, nikiwa njiani nikakutana na kijana fulani aliyekuwa amechoka sana, amekata tamaa na hata mavazi yake na mwonekano wake ulitosha kueleza kuwa kijana yule alikuwa anapitia wakati magumu sana.  Nilimsimamisha kijana yule na kumsalimia, nikamuuliza jina lake na kutaka kujua kama anasoma.

Akajitambulisha jina lake anaitwa Lukas na anasoma Salama sekondari na akanieleza kuwa yeye ndiye anayeishi kwa binamu yangu. Nilishangaa sana kuona jinsi ambavyo Mungu ameona nachelewa kumfuata Lukas hivyo, akaamua kunikutanisha naye. Nilimweleza kuwa nilipata ombi kutoka kwa binamu yangu kuniomba niishi naye nyumbani kwetu.

Basi nikamwambia asiende tena huko alikokuwa anaenda kwa sababu kesho yake atakapotoka masomoni atahamia nyumbani

kwetu na nitaishi naye. Lukas alipata faraja kubwa sana kwa sababu wakati ule alikuwa njiani kwenda sehemu ya mbali sana kutafuta msaada na kwa kweli alikuwa hana uhakika kama angepata msaada aliokuwa anahitaji.

Kesho yake baada ya masomo alihamia nyumbani kwetu na kuanza kuishi naye kama ilivyokuwa kwa yule kijana wa kwanza.

Kwa ufupi Lukas alikuwa anahitaji kila aina ya msaada ili aweze kuendelea na masomo yake. Mavazi yake yalikuwa yamechakaa sana na hakuwa na msaada wa fedha wala chakula. Nilimgawia nguo zangu zile zilizokuwa angalau zinamwenea na zingine alipeleka kwa fundi akazipunguza hatimaye akapendeza na akaonekana nadhifu mbele za watu. Nikaanza kumsaidia ada ya shule, michango na mahitaji mengine ya shuleni.

Hata nilipojiunga na elimu ya Chuo kikuu nilikuwa nagawana naye pesa yangu ya kujikimu mpaka akahitimu elimu ya sekondari. Alipochaguliwa kujiunga na chuo cha Ualimu kwa bahati nzuri nilikuwa nimeishapata kazi, hivyo, ikawa rahisi kumgharamia mahitaji yote ya chuo na hatimaye mpaka sasa Lukas ni mwalimu anaendelea na maisha yake.

Kwa haraka haraka huwezi kujua Mungu alinilipa nini kwa tendo langu jema la kumtunza Lukas lakini huwa naamini pengine ilikuwa ndio sababu pekee kwangu ya kupata mkopo kwa 100% nilipojiunga na elimu ya Chuo kikuu. Nilijiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Mwezi Oktoba, 2008 kusomea masomo ya Shahada ya awali ya Biashara katika fani ya Uhasibu. Wakati huo Shahada hiyo haikuwa na kipaumbele cha kukopeshwa kwa 100%. Kumbuka wakati huo kipaumbele kilikuwa kwenye fani za Sayansi na Ualimu, nilipokopeshwa mkopo kwa 100% nilitumia mkopo huo kufanya mambo mbalimbali binafsi pamoja nakumsaidia Lukas katika mahitaji yake mpaka akahitimu elimu ya Sekondari.

Kukopeshwa mkopo wa elimu ya juu halikuwa jambo la kawaida kwa sababu pale chuoni walikuwepo wanafunzi wengi sana waliokuwa na shida hata Zaidi yangu lakini hawakupata mkopo kiasi change. Pia kulikuwa na rafiki yangu ambaye pia tulisoma wote katika mazingira ya shida, mfadhili wetu alikuwa mmoja wakati tunasoma sekondari na tuliambatanisha kila kitu sawa kwenye maombi ya mkopo lakini yeye alipata 80% ya mkopo. Nakumbuka alikuja kuniuliza iweje tusome wote kidato cha nne na sita katika shule moja, tuweke viambatanisho sawa na tumechaguliwa kozi zinazofanana lakini mimi nikopeshwe zaidi yake? sikua na jibu, ila jibu alikuwa nalo Mungu pekee. Hivyo basi, kupitia shuhuda hizi napenda utambue kuwa***"Ipo nguvu katika sadaka isiyo ya kawaida".***

B. **Kundi la pili la utoaji wa sadaka isiyo ya kawaida ni sadaka inayotolewa kutokana na mahusiano ya mtu na Mungu**.

Yaani inakuwa ni sehemu ya maisha ya mtoaji kutoa bila kuona kuwa anapoteza mali zake au muda wake katika kujitoa mbele za Mungu. ***Wapo watu ambao wametengeneza urafiki na Mungu kiasi kwamba wanajitoa bila kiwango na wanajisikia raha kujitoa kwa ajili ya Bwana***. Utoaji huu unapokuwa ni endelevu na kwa uaminifu mbele za Mungu bila kujali hali waliyo nayo kiuchumi ndipo tunaona kuwa Mungu anaguswa na hata kunena jambo la kipekee kwa mtoaji wa sadaka.

Utoaji huu unakuwa ni tofauti na ule wa kawaida ambapo mtoaji hujaribu kutoa mara moja au mara kadhaa ili aone kama Mungu anajibu na akiona hapokei kama alivyotarajia anakoma kutoa au anatoa kwa malalamiko**.** Hapa tunaona mifano ya utoaji wa *Dorkasi* pamoja na *Kornelio* ambao maandiko matakatifu yanaonesha kuwa utoaji wao ulikuwa ni endelevu na ulikuwa ni sehemu ya maisha yao. Lakini pia tunaona kuwa maandiko matakatifu hayadokezi iwapo utoaji wa watu hawa ulitokana na maelekezo ya moja kwa moja kutoka kwa Mungu ila walijitoa

wenyewe kwa jinsi walivyokuwa wanampenda Mungu. Walifanya utoaji kuwa sehemu ya utumishi wao kwa Mungu. ***Hii inatufundisha kuwa hata kama Mungu hatasema na wewe moja kwa moja kuhusu utoaji, bado unayo nafasi ya kutoa sadaka ya kupendeza mbele zake.***

Katika utoaji wa Kornelio, yeye alikuwa akitoa sadaka nyingi kwa watu na tunaona jinsi ambavyo Mungu alivyoguswa na utoaji wake hata ikawa ndiyo sababu ya yeye kupata wokovu kamili **(*Matendo 10:1-4*).**

Pia tunaona utoaji wa mwanamke mmoja aitwaye Dorkasi ambaye maisha yake yalikuwa yamejaa utoaji, yaani utoaji ulikuwa ni sehemu ya maisha yake na ndiyo ikawa sababu mojawapo ya kufufuliwa kwake. Wakati wa kifo chake wajane wakasimama na kuonesha mavazi ambayo walikuwa wanavalishwa na Dorkasi, wakatoa machozi yao mbele za Mungu wakati ambapo Dorkasi hawezi kujiombea **(*Matendo 9:36-41*). *Kuna wakati ambao maneno yako hayataweza kufanya kitu au kuwa na nguvu mbele za Mungu bali kitakachokuwa na nguvu ya kusema au kupiga kelele mbele za Mungu ni yale uliyofanya kabla ya wakati huo unaokuwa unapitia.***

Hivyo, tujifunze kitu kwa hawa watumishi wa Mungu Kornelio na Dorkasi, sadaka na matoleo yao walioyafanya hapo nyuma ndiyo yaliyopaza sauti mbele za Mungu kwa ajili yao kumweleza na kumkumbusha Mungu juu ya wakati waliokuwa wanapitia.

Mbali na *Dorkasi* na *Kornelio*, pia tunaona utoaji wa mwanamke wa huko Shunemu ambaye anatimiza wajibu wake kama mama anayemjua Mungu kwa kuchukua jukumu la kumtunza mtumishi wa Mungu ***Elisha***. Mungu hakubaki kimya katika kujitoa kwake hata kumuwezesha kupata mtoto ambaye inasemekana kuwa alikuwa ameomba kwa miaka mingi bila majibu, hivyo utoaji wake ukawa sababu ya majibu ya maombi yake **(*2Wafalme 4:8-17*).** Halikuwa jambo dogo kwa mwanamke tena aliyeolewa

kwenda kumshawishi mume wake kumtunza mtu asiyemjua na ambaye ni mwanamume, ndiyo maana utaona utoaji huu haukuwa wa kawaida kwa sababu siyo tu huyu mama alimshawishi mume wake kumkaribisha Elisha lakini pia, walimjengea sehemu ya kulala na wakachukua jukumu la kumlisha.

***Kuna muda tunakuwa tunaomba tukitegemea majibu kupitia maombi yetu tu lakini kuna wakati ambapo utoaji wetu unakuwa ni mlango wa majibu ya maombi yetu.*** Katika ***Mathayo 10:42,*** Yesu Kristo anatoa ahadi kwa yeyote atakayejitoa kwa ajili ya watumishi wa Mungu kwamba hatakosa thawabu yake**.** Hicho ndicho kilichotokea kwa huyo mama wa Shunemu baada ya kujitoa kwa ajili ya mtumishi wa Mungu**.**

Utoaji mwingine wa sadaka isiyo ya kawaida tunauona katika makanisa ya Makedonia (***2Korintho 8:1-15***). Mtume Paulo anaguswa na kujitoa juu ya makanisa hayo, japo tunajua kuwa makanisa yale yalikuwa bado machanga kiroho na walikuwa katika hali ngumu kiuchumi lakini wakajitoa katika kiwango kikubwa bila kujali hali zao za kiuchumi. ***Hii inatuonesha kuwa moyo wa utoaji hautazami mali ambazo mtoaji anazo au muda mrefu ambao mtu amekaa katika wokovu bali ni upendo katika kujitoa kwa kujua ukuu wa Mungu.***

Katika ***Marko 12:41-44,*** tunasoma utoaji wa mwanamke mjane ambaye japo alitoa sadaka ndogo sana ukilinganisha na wale wengine waliotoa mapesa mengi lakini Yesu Kristo anafurahia utoaji wa mwanamke mjane. ***Hii inaturudisha kwenye hoja ya kwamba utoaji wa sadaka isiyo ya kawaida (sadaka inayo mpendeza Mungu) unahusiana zaidi na moyo wa mtoaji kuliko kiasi anachotoa.***

***Yesu anapomzungumzia huyu mama mjane anasema kuwa ametia vyote alivyokuwa navyo, ndiyo riziki yake pekee aliyokuwanayo.*** Maana yake si tu kwamba Yesu anataka tutoe kila kitu tulichonacho bila kujali chochote kitakachotokea bali

alichotaka kutundisha ni kuwa tunampenda kiasi gani yule tunayemtolea sadaka zetu yaani Mungu. Lakini pia, tunamtanguliza nani wakati wa utoaji wetu? je utoaji wetu umejaa imani? Kwa sababu, huyu mwanamke mjane hakuwa na senti yoyote aliyobaki nayo na wala hakujali itakuwaje juu ya maisha yake baada ya kutoka kwenye hiyo ibada.

***Hapa tunaweza kuona imani ya huyu mwanamke mjane juu ya Mungu aliyemtolea sadaka kwamba angeshughulika na mahitaji yake ya baadaye. Hii ndiyo aina ya imani katika utoaji wa sadaka ambayo Mungu hupendezwa nayo.***

Pia, mtumishi wa Mungu aitwaye Nuhu, baada ya ule msiba mkubwa wa gharika **(*Mwanzo 8:20-22*),** alimtolea Mungu sadaka nzuri kabisa ambayo ilikuwa sababu ya Mungu kutoa agano la kutotokea tena gharika katika nchi. Kumbuka katika gharika ile waliokoka watu 8 tu. Hii ni kusema kwamba, mbali na watoto na mke wa Nuhu, ndugu zake Nuhu wote walikufa katika ile gharika. Kama umewahi kufiwa na ndugu zako wa karibu utaelewa maumivu aliyokuwa nayo Nuhu kabla ya kutoa ile sadaka. Kwa hiyo ule moyo wa kutoa sadaka nzuri mbele za Mungu mara baada msiba kama ule halikuwa jambo la kawaida. Ingekuwa ni mimi na wewe labda tungekuwa na moyo mzito uliojaa manung'uniko badala ya shukrani. Utoaji wa jinsi hii unaonekana kumgusa Mungu na hivyo, kusababisha aseme jambo juu ya Nuhu.

Tumeona kuwa utoaji unaomgusa Mungu siyo lazima iwe mali nyingi sana japo kuna wakati anaweza kutaka ujitoe kwa hali isiyo ya kawaida. Jitahidi kujenga mahusiano yako na Mungu, wapo watu ambao wameokoka lakini wamewekeza mahusiano yao kwa wanadamu kuliko kwa Mungu. Unapookoka unafanyika kuwa mwana (mtoto) wa Mungu (***Yohana 1:12***) hivyo, ni vyema kuwekeza maisha yako, mali na akili zako kwa Mungu ili uone matunda ya wokovu ulioupokea.

**Utajuaje kama Sadaka Yako Siyo ya Kawaida?**

Sadaka hiyo lazima itaanza kukugusa wewe mwenyewe, yaani ni lazima itabeba moyo wako. Angalia mifano ya utoaji wa watu waliotajwa katika maandiko matakatifu; *Kornelio*, mwanamke mjane wa *Sarepta*, *mama Mshunemu*, *Dorkas*, *Ibrahimu*, *Nuhu*, *Mariam* ndugu yake na *Lazaro* na kadhalika. Bila shaka unaona wazi kuwa lazima kila mmoja aliguswa na utoaji wake na hivyo alitambua kujitoa kwake mwenyewe mbele za Mungu.

Lakini pia, tunajua kuwa neno la Mungu linasema kuwa pale hazina yako ilipo ndipo moyo wako utakapokuwepo, hivyo utoaji wa jinsi hii kwa sababu hugusa hazina yako ni lazima moyo wako ujue (***Mathayo 6:21***).

Kumbuka mfano wa kufanyika baraka kwa muhitaji kiasi cha wote mtoaji na mpokeaji kububujika machozi ya mguso kutokana na kitu kilichofanyika kuwa siyo cha kawaida. Kwa hiyo, inaonesha dhahiri kuwa mtu akifanya maandalizi mazuri ya utoaji wa sadaka ni lazima yeye mwenyewe moyo wake utamshuhudia. Lakini pia, kati yetu yupo Roho Mtakatifu ambaye hutushuhudia mambo yote, kwa hiyo yeye atasema na wewe kuhusu utoaji wako.

**Je, Sadaka Isiyo ya Kawaida Lazima iwe Fungu Kubwa?**

Jibu ni hapana. Siyo lazima sadaka isiyo ya kawaida iwe fungu kubwa japokuwa wakati mwingine linaweza kuwa fungu kubwa. Mtu mwenye kipato kidogo na mwingine mwenye kipato kikubwa wote wana nafasi sawa ya kutoa sadaka isiyo ya kawaida mbele za Mungu. Jambo kubwa hapa ni mtu kujitoa bil kujali hli nayopitia.

Jambo la muhimu katika utoaji wa sadaka isiyo ya kawaida ni uaminifu, utayari pamoja na upendo unaobeba moyo wa mtoaji. Mtoaji lazima awe anamjua Mungu anayemtolea lakini pia awe

tayari kutoa. Utambuzi huu utamsaidia kufanya maandalizi mazuri katika utoaji na hivyo mtoaji hatatoa chochote tu. Lakini pia, ili utoaji wako uwe na matokeo makubwa ni muhimu kuzingatia maelekezo ya Roho Mtakatifu katika utoaji wako. ***Huyu Roho Mtakatifu hutuongoza kuhusu nini tutoe, wapi tutoe na tutoe kiasi gani?*** Kama hufahamu jinsi gani Mungu anawasiliana na wewe ni bora kabisa utafute ufahamu wa rohoni ili ujue mawasiliano kati yako na Mungu.

Usifanye mazoea ya kutoa kwa akili zako tu, tegemea mwongozo wa Roho Mtakatifu yeye atakuongoza kutoa sadaka inayompendeza Mungu. Katika mifano ya watu waliotoa sadaka isiyo ya kawaida nimemtaja *Dorkasi* **(*Matendo 9:36-41*).** Maandiko matakatifu hayaoneshi kama Dorkasi alikuwa ni mtu tajiri kama yanavyomtaja ***Kornelio***, bali yeye katika fungu dogo hilo hilo aliweza kujitoa kwa ajili ya wajane na sadaka yake ikampendeza Mungu. Pengine Dorkasi alikuwa ni fundi cherehani tu na akatumia ufundi wake kuwavalisha nguo wajane na sadaka yake ikakumbukwa mbele za Mungu**.**

Pia, tumeona utoaji wa mwanamke mjane wa Sarepta **(*1Wafalme 17:9-16*)** ambaye hakuwa tajiri. Alikuwa amebaki na chakula kidogo tu lakini alikubali kujitoa kwa ajili ya mtumishi wa Mungu Eliya na utoaji ule ukawa wa maana kubwa mbele za Mungu hata akamponya katika ile njaa. Ukiangalia utoaji wa mjane ambaye tunaona Bwana Yesu Kristo anaguswa na sadaka yake, ile sadaka ilikuwa ni pesa ndogo sana ukilinganisha na wale waliotoa pesa nyingi **(*Marko 12:41-44*)**. Mifano hii michache inatosha kuonesha jinsi ambavyo kila mtu anayo nafasi ya kumpendeza Mungu kwa njia ya matoleo bila kujali kipato chake. ***Pia, umesoma shuhuda zangu jinsi nilivyojitoa kwa ajili ya vijana Daudi na Lucas bila kujali kuwa hata mimi nilikuwa napita katika hali ngumu kiuchumi na nilikuwa mhitaji pia, lakini nilikubali kutoa kile nilichokuwa nacho kwa ajili ya hao vijana***.

Kwa wale wanaotoa pesa au mali nyingi siyo wote wanaomfurahisha Mungu katika utoaji wao lakini pia siyo kwamba Mungu hapendi matoleo makubwa. Angalia mfano wa hao waliotoa pesa nyingi ukilinganisha na mwanamke mjane ambaye Yesu Kristo anafurahia sadaka yake. ***Japo tunaona pia utoaji wa pesa nyingi walizotoa Kornelio na Mariamu, utoaji wao ulikubalika mbele za Mungu***. Hivyo basi, suala siyo tu kiasi unachotoa bali ni jinsi ambavyo mtu anavyomtolea Mungu.

**Kitu Gani Husaidia Utoaji wa Sadaka Isiyo ya Kawaida?**

1. **Mahusiano ya mtoaji na Mungu (imani na upendo)**

   Asili ya utoaji ni upendo ambao tunauona kwa Mungu mwenyewe alipomtoa Yesu Kristo afe kwa ajili yetu sisi wenye dhambi. Hivyo, kwa mtu ambaye anatoa kama wajibu au kama sehemu ya kutii maagizo tu, kwake siyo rahisi kutoa sadaka isiyo ya kawaida mbele za Mungu. Suala la utoaji limebebwa na upendo **(*Kutoka 35:5, 22, 29; 36:3*).**

   Kuhusu suala la imani, tunaona mfano wa utoaji wa *Habili* ambaye kwa imani alitoa sadaka ambayo ilimpendeza Mungu. Maandiko matakatifu yanatueleza kuwa tendo lolote tulifanyalo bila imani haliwezi kumpendeza Mungu, kwa hiyo, kama mtu atatoa tu bila kuwa na imani juu ya mbegu anayopanda, utoaji huo hauwezi kumpendeza Mungu. ***Wapo watu wanaotoa sadaka huku hawana uhakika kabisa kama Mungu ameiona sadaka yao ndio maana wengine wanalazimika kujionesha kwa watu ili wajulikane kuwa wanajitoa sana.*** Yote hayo yanatokea kwa sababu ya upungufu wa imani, hawaamini kuwa Mungu ameona na amepokea sadaka zao. Kwa hiyo, ni vyema tuamini kuwa Mungu anaona kila tunachofanya katika utoaji wetu ndipo itakuwa rahisi kwetu kujitoa kusiko kwa kawaida.

2. **Kudumu katika Uwepo wa Msaada wa Nguvu za Roho Mtakatifu**

   Msaada pekee ambao watumishi wa Mungu wameachiwa ni nguvu za Roho Mtakatifu katika kutimiza mapenzi ya Mungu. Bila msaada huu ni vigumu sana kutimiza azima zetu za kumpendeza Mungu kwa njia ya sadaka.

   Katika utoaji wa sadaka isiyo ya kawaida tumeona kuwa wakati mwingine tunahitaji kutumia mali zetu au muda mwingi sana kwa ajili ya Bwana au kuwasaidia watu wengine. Hivyo, bila msaada wa nguvu za Roho Mtakatifu ni rahisi kukatishwa tamaa katikati ya safari. Fikiria kwamba umejitoa kusomesha watoto wasio na uwezo kiuchumi, umejitoa kujenga kanisa au kujitoa kwa jinsi yoyote ile kadri Roho wa Bwana atakavyokuwa amekuongoza, bila shaka kujitoa huko kutakugharimu pesa nyingi na kwa muda mrefu.

   **Pasipo msaada wa Roho Mtakatifu ni rahisi sana shetani kukuinulia watu watakao kukatisha tamaa na hatimaye ukaanza kufikiria kwamba unajipa hasara au unapoteza muda kwa kufanya hivyo vitu**. *Tunao mfano wa Anania na Safira, ambao waliahidi kutoa sadaka ya kiwanja chao kwa hiari lakini ghafla wakabadili nia yao na kujikuta wanamdanganya Roho Mtakatifu kisha wanaingia katika hukumu kubwa sana **(Matendo 5:1-5)**.*

   Je, hujawahi kukutana na mtu anayesema ***'laiti ningejua nisingemsaidia au nisingefanya hivi na vile.*** Mtu wa jinsi hii huwa tayari ameshavurugwa kiasi kwamba kwa sasa anaona hasara katika kujitoa kwake wakati mwanzoni aliona kuwa ulikuwa ni utumishi mbele za Bwana.

Fikiria kipindi Ibrahimu anaenda kutoa sadaka ya kumteketeza mwanae, kama isingelikuwepo msaada wa nguvu ya Mungu ndani yake bila shaka angerudia njiani. Kumbuka kuna wakati Isaka alimwuliza Ibrahimu “babangu! moto upo na kuni zipo, lakini hakuna mwana-kondoo” **(Mwanzo 22:7).** Hilo swali halikuwa jepesi kwa mzazi wa mtoto. Fikiria wakati Mariamu anapeleka sadaka ya mafuta yenye thamani kubwa mbele za Yesu kisha akina Yuda wakaanza kumkatisha tamaa, pasipo Yesu kumtia moyo bila shaka huyu Mariamu angevunjika moyo na kuona hasara juu ya sadaka yake. Kumbuka wakati Eliya anamwomba chakula yule mama mjane wa Sarepta bila shaka pasipo nguvu za Bwana isingekuwa rahisi kwa yule mama kukubali kutoa akiba yake ya mwisho kabisa kwa ajili ya Eliya.

Wakati huu ambapo Yesu hayupo nasi kimwili msaada pekee tulio nao ni kuendelea kuwepo katika usaidizi wa nguvu za Roho Mtakatifu ili kutusaidia katika kufanikisha azima ya kutoa sadaka isiyo ya kawaida mbele za Mungu.

**Nafasi ya Roho Mtakatifu katika Utoaji wa Sadaka:**

***i.*** *Roho Mtakatifu hutupa ujasiri wa kufanya mambo ambayo kwa macho ya mwili hayawezekani.* Katika maandiko matakatifu tunaona mifano ya wajane wawili ambao walitoa sadaka zao wakati ambapo akili za kibinadamu zinakataa lakini waliweza kufanya hivyo kwa msaada wa nguvu ya Mungu iliyofanya kazi ndani ya mioyo yao ***(Marko 12:41-44; 1Wafalme 17:9-16).***

***ii.*** *Hutusaidia kututia moyo hata kama shetani atajiinua kutukatisha tamaa.* Tunaona wakati Mariamu amenunua mafuta ya gharama kubwa ili kumpaka Yesu, waliinuka watu walionung’unika sana juu ya jambo lile, kisha Yesu akamtia moyo

Mariamu. Wakati huu ambao Yesu hayupo nasi kimwili, ni Roho Mtakatifu ambaye hututia moyo wakati wa kuvunjwa moyo ***(Marko 14:3-9*).**

***iii.*** *Hutusaidia kutuinulia watu ambao hufanyika Baraka katika kukamilisha kazi ya Bwana au watakaokufaa wakati wa shida.* Ukisoma habari za Nehemia na Ezra katika kujenga ukuta wa Yerusalemu pamoja na hekalu, utaona jinsi ambavyo Mungu alivyoinua watu mbalimbali katika ujenzi ule ***(Nehemia 2:7-9; Ezra 1:3-4).*** Pia tunaona wakati Eliya akiwa katika njaa, Mungu alimwinulia mtu aliyemlisha wakati wote wa njaa ***(1Wafalme 17:9-16).***

***iv.*** *Hutusaidia kutuelekeza mahali sahihi pa kutoa sadaka***.** Neno la Mungu linatuzuia kutoa sadaka mahali tunapoamua kwa akili zetu bali sadaka itolewe mahali ambapo Bwana amechagua. Kwa hiyo kwa akili zetu hatuwezi kujua sehemu sahihi ya kutoa sadaka zetu bila msaada wa Roho Mtakatifu ***(Kumbukumbu la Torati 14:13-14)***

3. **Usikivu na Utii wa Sauti ya Mungu**

Usikivu na utii wa sauti ya Mungu unaambatana sana na suala la imani. Siyo rahisi mtu kutii sauti ya Mungu bila kuamini kuwa hiyo sauti inatoka kwa Mungu na kwamba Mungu yupo. Rejea utoaji wa kundi la kwanza utaona kuwa utoaji wao uliambatana na utii wa sauti ya Mungu.

Ili kufanikisha utoaji kwa kusikia na kutii sauti ya Mungu ni lazima ujue milango ambayo kwayo Mungu huwa anaongea na wewe, vinginevyo itakuwa vigumu sana kufanikisha utoaji wako.

Milango hiyo inaweza ikawa ni watumishi wa Mungu (kupitia mahubiri na mafundisho mbalimbali ambayo

Mungu anakusudia kuongea na wewe kupitia ujumbe wa somo husika), ndoto, Malaika, sauti ya ndani ya moyo wako, maono, maombi, kusoma neno la Mungu, watu mbalimbali (siyo lazima wawe watumishi wa Mungu maana Mungu hutumia mtu yeyote kutimiza makusudi yake) n.k. Malaika wanaweza kukujia kwa njia mbalimbali kama vile mtu anayeomba msaada n.k siyo lazima wawe wamevaa mavazi meupe kama wengi wadhaniavyo (**Waebrania 13:2; Mwanzo 18:1-3**). ***Ni vigumu kufanikisha utoaji kwa njia hii kama wewe mwenyewe huwezi kutofautisha kati ya sauti ya Mungu na hisia zako au sauti ya shetani.***

Hivyo, tambua kuwa usipokuwa mwangalifu unaweza kudanganywa na matapeli wa injili kwamba wamesemeshwa na Mungu labda uuze mali yako ya thamani au utoe mshahara wako wote ili umtolee Mungu sadaka. Wengi wametapeliwa kwa njia hii na matokeo yake wamekataa wokovu. Jitahidi kumkaribia Mungu wewe mwenyewe ili aseme na wewe moja kwa moja, hakikisha unatambua sauti ya Mungu wewe mwenyewe. Usisubiri kusemewa na watu kwamba Mungu amesema nao kuhusu utoaji wako, mtafute Mungu naye atajidhihirisha kwako binafsi (***Isaya 55:6, 2, Nyakati 26:5).***

Jitie nia ya kumtafuta Bwana, yeye hayupo mbali kabisa, atasema na wewe tena atakuongoza katika kumtolea sadaka nzuri na hatimaye utaona matokeo ya matoleo yako. Hii haimanishi kuwa usisikie maonyo ya mchungaji wako au watumishi wengine wa Mungu kuhusu utoaji, hapo awali nimedokeza kuwa Mungu anaweza kusema na wewe kupitia huduma zao pia. Jambo la kusisitiza hapa ni kwamba hata wewe una nafasi ya kusikia sauti ya Mungu kwani Mungu anaweza kusema na wewe moja kwa moja bila kutegemea watu wengine.

*Je, unaonaje hali ya utoaji wako? ya kawaida au siyo ya kawaida? Je, unaamuaje baada ya somo hili? Je, kama ukirudishiwa sadaka uliyoandaa kutoa kanisani itakubariki wewe binafsi? au utaona kuwa haiwezi kufanya jambo lolote la maana kwako? je, umetambua nguvu iliyopo katika utoaji wa sadaka isiyo ya kawaida?*

## *Sura Ya Tatu*
## AINA ZA SADAKA

Yapo makundi makuu mawili ya matoleo ambayo ni **Fungu la kumi** (Zaka) na **sadaka ya upendo**. Sadaka ya upendo nayo imegawanyika katika makundi mbalimbali kulingana na ***kusudio la mtoaji.*** Wakati wa Torati kulikuwa na aina tano za sadaka nazo vilevile zilitofautiana kulingana na makusudio ya mtoaji wa sadaka husika.

### a) Aina za sadaka wakati wa agano la kale:

**1. Sadaka za kuteketezwa**: sadaka hii ilifanyika ambapo nyama ya mnyama fulani inateketezwa juu ya madhabahu kama ishara ya mtu ama taifa zima kujitoa kwa Mungu bila kukoma (***Mambo ya Walawi 1:9; Mwanzo 8:20; 22:2; Kutoka 10:25; 29:38-42, Warumi 12:1***)

**2. Sadaka ya shukrani:** mtoaji alitoa unga pamoja na divai au kinywaji; sadaka hizi zilionesha shukrani kwa Mungu kwa ajili ya chakula cha kila siku kilichotoka kwake. Kumbuka sadaka hii humuonyesha Mungu na kumfunulia uelewa wa moyo wako kuwa umetambua ya kuwa ni yeye amesababisha kupata hayo uliyopokea kwa sababu yeye ndiye atupaye nguvu ya kujipatia utajiri au baraka tulizonazo. Kwa hiyo, pale unapoenda mbele zake kushukuru huku ukisindikizwa na sadaka yako basi inasababisha Mungu aendelee kufungua milango na nguvu zaidi za wewe kubarikiwa. (***Kumbukumbu 8:17-18***, ***Mambo ya Walawi 2:4-10; 23:13,18; Hesabu 15:1-10***).

**3. Sadaka ya Amani:** sadaka hii ilionesha ushirika na uhusiano mwema ambapo mtoaji alishirikiana na familia yake, marafiki zake na watu wenye dhiki kula mabaki ya mnyama aliyetolewa katika sadaka ya kuteketezwa katika sherehe ya furaha (***Mambo ya Walawi 7:11-18; Kumbukumbu la Torati 12:7, 12; 1Samweli 9:12-13).***

***4.*** **Sadaka ya dhambi**: Hii ilitolewa pale ambapo mtu alipotambua kuwa amevunja sheria mojawapo ya Mungu kwa hivyo, alitoa sadaka hii ili ifanyike kama ishara ya toba mbele za Mungu. Sadaka hii kwenye agano la kale ilitumika kama kifuniko cha kumfunika mtoaji ili aweze kumkaribia Mungu aliye mtakatifu. Kwa hiyo, kifuniko hiki hakikuwa na uwezo wa kumbadilisha mwanadamu ili asiendelee kutenda dhambi, bali ilifanya kazi ya muda mfupi pale mtoaji anapotaka kwenda mbele za Mungu.

Sadaka ya damu ya Kristo msalabani ilitosha kumaliza kila kitu pale tunapokubali na kumruhusu aingie ndani yetu. Damu ya Yesu hutusafisha dhambi zetu zote na kutupatia msamaha wa dhambi. Sadaka za fedha au vitu baada ya kifo cha Yesu Kristo msalabani haina uwezo wa kusababisha mtoaji kusamehewa bali jibu la dhambi ni toba kupitia jina la Yesu. (***Mambo ya Walawi 4:27-30; 6:26, 30 Ebrania 7:24-25; 10:10*****)**

**5. Sadaka ya hatia:** sadaka hii ilitolewa kwa kosa la mtu kupimwa kwa thamani ya pesa au vitu. Mfano wa hayo makosa ni kusahau kutotoa zaka, kufanya uharibifu katika mali fulani, kusahau kulipa deni n.k **(*Mambo ya Walawi 5:15; 6:1-5*).** Aliyekosa alilipa hasara pamoja na fidia ya **asilimia 20** ya thamani ya kitu husika **(*Mambo ya Walawi 5:16; 6:5*).**

**Upungufu wa Sadaka Wakati wa Torati**

Sadaka za wanyama hazikuweza kuondoa dhambi (***Waebrania 10:4***), japo zilisaidia kuonesha kuwa sadaka ya kifo (**dhabihu**)

ilikuwa lazima kwa kuondoa dhambi (***Waebrania 9:22***). Kifo pekee cha sadaka kilichotimiza mambo yote ambayo sadaka za Agano la Kale hazikuweza kuyatimiza ni sadaka ya Yesu Kristo kama nilivyotangulia kuelezea hapo juu (dhabihu ya Yesu Kristo), (***Waebrania 10:11-14, 17-18)***.

Tofauti na sadaka za wanyama, sadaka ya Kristo inaondoa dhambi, inasafisha dhamiri, inaleta msamaha kamili na inahakikisha ukombozi wa milele (***Waebrania 9:6-7, 11-12, 25-26). Sadaka hii ilikuwa ya hiari na tendo la utii na upendo***. Hivyo, sisi leo tunapoenda kutoa sadaka, hatuendi kutengeneza **upatanisho kati yetu na Mungu**, kazi hii ilishafanywa na Yesu Kristo pale msalabani**.**

**(b) Aina za Sadaka wakati wa Agano Jipya.**

1. **Sadaka ya Upendo (*2Korintho 8:3; 9:7*)**

Hii ni aina ya sadaka tunayotoa kwa hiari mara kwa mara wakati wa matoleo ya ibada au hata tunapotoa kwa ajili ya kusaidia watu wengine wenye uhitaji. Sadaka ya upendo ni pamoja na utoaji wa kufanikisha shughuli mbalimbali za kanisani ikiwemo ujenzi, ununuzi wa vyombo, kupeleka injili, kutia moyo na kupongeza watumishi wa Mungu katika huduma mbalimbali.

Toka mwanzo Mungu huwafurahia watu wanaotoa kwa upendo tena kwa hiari yao wenyewe ndiyo maana inaitwa sadaka ya upendo mbele za Mungu. Mungu anamwelekeza Musa kuwa watu wenye moyo wa kupenda ndio wamtolee sadaka kwa ajili ya kazi yake (***Kutoka 25:1-8)***. Mungu ametubariki kwa utajiri wa wanyama, mazao na tunazo pesa pia kwa ajili ya kumtolea Bwana sadaka ya upendo.

Lakini ni muhimu kujua kuwa sadaka ni suala la moyoni, linalofanywa kwa moyo wa kupenda na kutii bila kushurutishwa. Upendo katika utoaji umeasisiwa na Mungu mwenyewe pale alipomtoa mwanawe wa pekee ili kufa kwa ajili ya dhambi zetu (***Yohana 3:16***). ***Hivi leo sisi tunaendeleza upendo huo kwa kujitoa kwake kwa baraka za mali alizotubariki yeye mwenyewe.***

**Kiwango cha Sadaka ya Upendo**

Tofauti na fungu la kumi ambalo maandiko matakatifu yametaja kiwango cha kumtolea Mungu, sadaka ya upendo haikuamuliwa kiwango cha kutoa bali inatolewa kwa hiari yako na kwa kupenda *(**Kumbukumbu la Torati 16:10; 2Korintho 9:7**)*. *Maandiko yanatufundisha kutoa kulingana na mapato yetu* ***(toa kulingana na mapato yako bila kulazimishwa, 1Korintho 16:2; 2Korintho 8:11-14)***. Utakavyoamua kupanda ndivyo utakavyovuna, ukitoa kidogo utavuna au utapimiwa kidogo pia, ukitoa kwa wingi utapimiwa vingi. ***Ni vyema pia ifahamike kuwa udogo au ukubwa wa sadaka hutegemea sehemu uliyotoa kama sadaka katika wingi wa vitu au mali ambazo Mungu amekupa.***

Ukubwa au udogo wa sadaka ya mtu haupimwi kwa kutumia thamani ya pesa ya sokoni (yaani kusema TSh. 500; 1,000; 5,000; 10,000/= n.k) bali kwa kadri ya uwezo wa mtoaji sawasawa na nafasi ya mali yake **(*Marko 12:43-44; 2Korintho 8:2*).** Kwa sababu hii mtu anaweza kutoa TSh 10,000/= kama matoleo yake katika ibada na kiasi hiki kikawa ama kikubwa au kidogo kabisa kulingana na jinsi ambavyo Mungu amemjalia mtu huyo. Mtu mwingine katika ibada akatoa TSh.1,000/= ikawa sadaka kubwa ukilinganisha na huyo wa kwanza kutokana na fungu ambalo Mungu amembariki.

Mungu anaahidi kuwa mtu asiogope kutoa kiasi kikubwa cha sadaka kwa kuogopa umasikini au hali aliyonayo kwa sababu Mungu ndiye mtoaji wa vyote. ***Kwa sababu utoaji huambatana***

***na Imani, wengi wamefungiwa kwenye eneo moja la maisha kwa sababu ya kutazama hali au walichonacho kwa wakati huo badala ya kutumaini kupata vingi kutoka kwa Mungu***. Wanashindwa kumtolea Mungu kwa viwango vya ukuu na utukufu wake kwa kutokuelewa kuwa huo ndio mlango pekee ambao Mungu anautumia kupima moyo wa mwanadamu juu ya uaminifu wake katika uwakala wa mali za dunia alizobarikiwa nazo.

**Ushuhuda:**

Wakati kaka yangu alipofariki tarehe **20 Octoba, 2021**, na hivyo kuniachia majukumu ya kuhudumia familia yake, swali langu kubwa lilikuwa ni kwa jinsi gani nitahudumia hiyo familia pamoja na ya kwangu. Nilijihisi kuwa na mzigo mkubwa sana wa kuhudumia familia mbili. Swali langu na mawazo yangu hayakuwa mazuri mbele za Mungu kwani nilifikiria kuwa ni kwa uwezo wangu na akili zangu naweza kuhudumia hizo familia.

Mara baada ya mawazo yale mabaya mbele za Mungu, nilipata ufumbuzi wa Rohoni kwamba hata watoto wangu wanahudumiwa siyo kwa sababu nipo hai bali kwa sababu Mungu ananiwezesha kuwahudumia. Hivyo, hata hiyo familia ya kaka yangu ni Mungu atakayeihudumia na siyo mimi kama nilivyowaza.

***Wengi tunadhani kuwa tunafanikisha mambo yetu kwa akili na uwezo wetu kiasi kwamba hata tunafikia hatua ya kuogopa kujitoa kwa ajili ya kazi ya Mungu kwa kuhofia kuwa mambo yetu yataendaje mara baada ya kutumia mali zetu kwa Mungu.***

Asiye na Imani na kutofahamu fadhili za Mungu vizuri hufikiri kuwa utoaji ni sababu ya kufirisika. Kama mtu atashindwa kumuelewa Mungu vizuri na kutambua sauti yake basi inasababisha kufunga milango yake yote ya kutoka mahali alipo na kushindwa kukua na kuongezeka kwa kila namna.

Ni dhahili kwamba, endapo yule mama mjane wa Sarepta ambaye Eliya alimwomba chakula angebaki kuiamini sauti ya mahubiri ya mwili na hali yake ya upungufu wa chakula, bila shaka angeishia kufa kama wengine walivyokufa katika kipindi kile cha ukame na njaa kali. ***Kamwe usijilinganishe na mtu katika utoaji wako mbele za Mungu. Utoaji siku zote hutegemea mtu mwenyewe jinsi anavyomjua Mungu na Upendo wake kwa Mungu***.

Utoaji wako kwa uaminifu na kwa ukarimu mbele za Mungu ndio unaofungua milango yako ya kupokea kwa wingi kutoka kwa Mungu aliye chanzo cha uhai na baraka zako. ***Sio wingi wa vitu utakaowaongoza wenye imani kumtolea Mungu bali watu hawa huongozwa na imani na upendo***. Wapo watu wenye vitu vingi lakini utoaji wao mbele za Mungu hauko sawasawa kwa sababu ya kukosa Imani na upendo juu ya chanzo cha wao kuzidishiwa walivyo navyo ***(2Korintho 9:8-10; Filipi 4:19).*** Biblia inaeleza mambo mawili muhimu sana katika kila sadaka unayoitoa kwa Bwana, yaani **upendo** kisha **kutoa** kunafuata. '**Mungu *aliupenda ulimwengu* kisha *akatoa*'**. Siri ya utoaji mzuri ni hiyo, kwamba ukihitaji sadaka yako iwe na nguvu basi huna budi "*kupenda*" kutoka moyoni, ndipo "*utoe*".

Tunaona pia, Yesu Kristo anaikubali sadaka ya mama mjane kwa sababu alitoa kwa moyo wa upendo. Yesu hakupenda sadaka ya wale wengine kwa sababu pamoja na kwamba walitoa mapesa mengi lakini hayakuonekana ya thamani mbele za Mungu kwa sababu pengine hawakutoa kwa upendo au unyenyekevu mbele za Bwana (***Luka 21:1-4).***

Ukisoma vizuri ***Luka 21:1-4,*** utagundua kuwa utoaji wa wale matajiri haukufanywa kwa moyo wa kupenda na kwa moyo wote maana walitoa yale yaliyowazidia. Kitu kilichozidi ni kile ambacho hata wewe mwenyewe hukihitaji yaani unatafuta sehemu ya kukipeleka ili kikuondoke machoni pako. Mtu ambaye kabati lake la nguo limejaa au nguo zimembana au zimepitwa na wakati ndiyo baadhi ya mifano ya vitu vilivyozidi. ***Wapo watu***

***ambao utoaji wao unasubiri pale watakapoona mahitaji yao binafsi yametimia, yaani kwao haipo bajeti ya sadaka wala msaada kwa watu wengine***.

Siyo vibaya kumpa mwenzio nguo zilizokubana au ambazo kwako zimepitwa na wakati au zimekuwa nyingi kwako kiasi kwamba unaamua kuzipunguza kwa kugawia wenzio. Jambo la muhimu ni kuwa ipo tofauti ya kutoa vilivyozidi na kutoa visivyozidi kwako yaani vile ambavyo bado unavipenda. Hivyo, sadaka za hao wengine pengine Yesu aliona kuwa hazikubeba mioyo yao na zilikuwa si kamilifu ingawa walitoa pesa nyingi kuliko yule mwanamke mjane. Hivyo, ***tunajifunza kuwa suala sio kiasi tu bali suala lingine la muhimu lipo katika moyo wa mtoaji.*** Moyo ukipenda utatoa vilivyo vya thamani na hiyo sadaka yako itaambatanishwa na moyo wako na hivyo kuwa ya maana mbele za Mungu. Katika andiko hilo, tunaona jinsi ambavyo sadaka ya yule mwanamke mjane ilivyo ambatanishwa na moyo wake na hivyo kuwa ya thamani mbele za Mungu**.**

**Mahali pa Kutoa Sadaka ya Upendo**

Kwa sababu ya upendo wa kujitoa kwa Yesu Kristo msalabani, sisi leo tunatakiwa kutoa sadaka kama ishara ya utii na upendo wetu kwa Mungu.

Mungu anataka watu wake waoneshe utii na upendo wao kwa njia ya kujitoa kwa hiari kwa ajili ya watu wengine pia ***(Efeso 5:2,25; Yohana 15:12-13; Rumi 5:8; Waebrania 10:7-10***). ***Yesu Kristo alibeba msalaba siyo kwa ajili yake mwenyewe, yeye hakuwa na hatia bali alifanya hivyo kwa ajili ya watu wengine.*** Hivyo, utoaji wetu usiishie madhabahuni pekee au kwa watu tunaowafahamu tu bali kwa kadri Roho wa Bwana atakavyokuongoza, unaweza pia kutoa sadaka yako ya upendo kwa watu wengine wenye uhitaji ili ifanyike kama ishara ya upendo wa Mungu kwao.

Sehemu nyingine ya sadaka utoe kanisani (madhabahuni) kwa ajili ya kufanikisha mahitaji ya madhabahuni. ***Wakati mwingine pia andaa sadaka ya kuwatia moyo watumishi wa Mungu moja kwa moja bila kujali kwamba umetoa sadaka kanisani.*** Usiache kwenda na sadaka madhabahuni (usiende mikono mitupu) kwa kisingizio kwamba umetumia sadaka yako nyingi kusaidia masikini (***Kumbukumbu la Torati 16:16-17***). Ukumbuke kuwa sadaka zetu ni za upendo na kawaida ya upendo huwa hauna kipimo **(*1Korintho 13:3*)**. ***Kama vile ambavyo huwezi kuhesabu idadi ya baraka za Mungu anazoachilia juu yetu, vivyo hivyo utoaji hautakiwi kuwa na kipimo bali kwa kadri Mungu atakavyoendelea kukuwezesha na wewe endelea kujitoa***.

Sadaka zetu ni sadaka za kiroho zitolewazo kama shukrani kwa Mungu kwa sababu ya upendo na neema yake kwetu. Mbali na sadaka za mali zetu pia tunatakiwa kumtolea Mungu sadaka za ibada, sifa na huduma ***(Rumi 15:16; Waebrania 13:15-16).*** Tunaweza kutoa sadaka za kumpendeza Mungu ikiwa tumejitoa wenyewe kwanza kuwa dhabihu au sadaka hai kwa Mungu ***(Rumi 12:1; 2Korintho 8:1-5).***

## Kujitoa kwa Ajili ya Watu Wengine

Kama ilivyodokezwa hapo awali usiishie kutoa madhabahuni tu bali kadri Roho wa Bwana atakavyokuongoza, unaweza kutoa sadaka yako ya upendo kwa watu wengine wenye uhitaji ili ifanyike kama ishara ya upendo wa Mungu kwao. Sehemu nyingine ya sadaka utoe kanisani (madhabahuni) kwa ajili ya kufanikisha mahitaji mbalimbali ya madhabahuni. Kujitoa kwa mambo yote haya kwa pamoja kunahitaji mwongozo thabiti wa Roho Mtakatifu. Wapo watu ambao wanapokuwa na mahitaji yao binafsi basi watajiona kuwa wao pekee ndio wanastahili kusaidiwa na hivyo wao hawastahili kusaidia wengine. ***Watu wengine wameshajichukulia kuwa wao ndio watu pekee wa kusaidiwa hivyo wamefunga kabisa milango ya kujitoa kwa ajili ya watu wengine.*** Utoaji wa jinsi hiyo hautakutoa mahali ulipo.

Kumbuka shuhuda zangu jinsi nilivyokuwa katika hali ya uhitaji lakini bado nilijitoa kwa ajili ya watu wengine.

*Ni vyema sasa utambue kuwa wakati ukiwa unasubiri kujibiwa haja zako au wakati watu wengine wanapofanyika baraka kwako hata kama wewe unajiona kuwa mahitaji yako ni muhimu sana, na wewe una nafasi ya kugusa maisha ya wengine wenye uhitaji* (***Mathayo 7:7-12*****)**. Katika **Mathayo 7:7** neno la Mungu linatuhakikishia kuwa tukiomba tutapokea, tukitafuta tutaona na tubishapo tutafunguliwa.

Uhakika wa neno hili unatolea mfano wa sisi wenyewe kama wanadamu kwamba hatupeani vitu vibaya na kama ni hivyo basi, ni hakika kuwa Mungu wetu atatupatia vitu vilivyo vyema sana. Tutambue kuwa ni kawaida sana kupita kipindi kirefu kabla hatujapata yale tunayoomba kwa Mungu. Wakati huu wa mpito siyo wa kukunja mikono kwa wengine wenye shida kama au tofauti na za kwetu kwa kisingizio kwamba na sisi tuna shida kama zao au tuna shida zaidi yao.

Katika ***Mathayo 7:12*** neno la Mungu linasema kuwa, yoyote tutakayotendewa au kuyapokea basi hatuna budi kuyatenda kwa wengine pia. Bila shaka hayo tunayotaka kutendewa wakati mwingine huwa bado hatujayapokea lakini neno la Mungu linatuelekeza kuyatenda kwa wengine na hata tukishapokea haja zetu bado lipo agizo la kufanya wema kwa wengine pia.

Hata tunapokuwa tunapitia wakati mgumu kiasi gani, hiyo isiwe sababu ya kutuzuia kujitoa kwa wengine, lazima tuguse maisha ya wengine wakati tukisubiri majibu yetu. Kwa jinsi wanadamu walivyo kila mmoja angetamani kutendewa wema aidha kutoka kwa Mungu au kwa wanadamu wenzake, lakini mwanadamu huyo huyo huwa anasahau kwamba naye ana nafasi ya kuleta furaha katika maisha ya wanadamu wengine. ***Neno hili linatukumbusha wajibu wetu wa kiroho wa kuleta furaha katika maisha ya wengine***. Hata majibu ya Mungu hupita kwa

mwanadamu mmoja kwenda kwa mwanadamu mwingine (***Marko 3:35; 2Korintho 8:1-5***).

Katika ***2Korintho 9:6,*** mtume Paulo anatukumbusha kuwa apandaye haba atavuna haba, hivyo jinsi tunavyojitoa kwa udhaifu kwa ajili ya wengine ndivyo hivyo tutegemee kupokea vichache kutoka kwa Mungu. Pia katika ***2Korintho 9:9,*** mtume Paulo anatukumbusha habari ya kujitoa kwa ajili ya watu wengine ambako ndiko kunasababisha haki zetu za kupokea baraka kutoka kwa Mungu kukaa milele**.** Kukaa milele hapa ni pamoja na vizazi vyetu kubarikiwa hata kama sisi wenyewe wakati huo tutakuwa tumeshakufa**.**

Katika ***Zaburi 37:22, 25,*** Daudi anasema kuwa waliobarikiwa na Bwana hurithi nchi na wala watoto wao hawawezi kuomba mkate barabarani**.** Kwa hiyo ni hakika kwamba baraka za kujitoa kwako kwa wengine kutakuletea baraka zinazodumu milele katika vizazi vyako**.** Tunapojitoa kwa ajili ya wengine tunapata haki ya kuzidishiwa baraka zetu kutoka kwa Mungu katika kutekelezewa mahitaji yetu katika utajiri wa kila namna ***(2Korintho 9:8,11*****)**. Tunaona kuwa kujitoa kwetu kwa ajili ya watu wengine kunampa Mungu shukrani na utukufu. Yaani wewe unapogusa maisha ya watu wengine Mungu hutupa riziki zetu lakini pia Mungu huwa anasifiwa na kupewa utukufu **(*2Korintho 9: 11-13*)**.

Katika maandiko matakatifu, ipo mifano kadha wa kadha ambayo inaonesha watu waliojitoa kwa wengine kisha nao kwa wakati wao wakapokea haja zao. Katika ***1Wafalme 17:9-16*** tunaona utoaji wa mama mjane wa Sarepta ambaye hakuwa na chakula cha ziada lakini alikubali kujitoa kwa ajili ya Eliya. Katika hali ya kawaida ya akili za kibinadamu huyu mama alikuwa na sababu halali ya kukataa kumsaidia Eliya.

Kujitoa kwake kwa ajili ya Eliya kulikuwa na maana kubwa sana mbele za Mungu hata akamponya katika kile kipindi cha njaa. *Wapo watu wanaosema huyu mama alijitoa kwa Eliya kwa*

*sababu tayari Mungu alikuwa amesema naye. Ni kweli kabisa, Mungu alikuwa amesema naye lakini je, ni kweli kwamba Mungu hajawahi kusema na wewe**? Mungu anafanya kazi na wanaosikia na kutii sauti yake. Mungu anafanya kazi na watu walio tayari kutumika. Watu wengi hawapo tayari kutumika Mungu hasa kwa mali zao na ndiyo maana Mungu hawatumii na wala hawezi kuwasemesha juu ya utoaji.***

Fikiria kama huyu mama asingetii sauti ya Mungu kwa kisingizio kwamba hakuwa na chakula cha kutosha kugawana na mtumishi wa Mungu Eliya. Bila shaka angekufa katika ile njaa na asingeliona majibu ya maombi yake ya kuponywa katika njaa. Watu wangapi ambao mambo yao yamekufa kwa sababu hawakuwa waaminifu katika kutii sauti ya Mungu? ***Watu wangapi wamekuja kwako kwa maelekezo ya Mungu ili uwasaidie na iwe sababu yako kupokea majibu ya maombi yako lakini walipofika kwako ukatoa sababu kadha wa kadha wakarudi mikono mitupu?*** Hii haimaanishi kwamba kila mtu anayekuja kwako kuomba msaada huwa ametumwa na Mungu ili kuwa mlango wa majibu ya maombi yako lakini ujue kwamba wapo watu wanaokuja kwako kwa maelekezo ya Mungu.

Hivyo, ni vyema kumuomba Mungu ili upate roho ya utambuzi wa maelekezo au sauti ya Mungu ili utoaji wako umpendeze Mungu. Mtume Paulo anawaombea watu wa Efeso kupata utambuzi wa Rohoni ili wazione Baraka za Mungu. Lazima tuwe na utambuzi wa Rohoni ili tujue na kuyatenda mapenzi ya Mungu (***Waefeso 1:17-18***). Ukiangalia utoaji wa mama mjane ambaye tunaona Bwana Yesu Kristo anaguswa na sadaka yake, ile sadaka ilikuwa ni pesa ndogo sana na hivyo kuonesha kuwa huyo naye alikuwa ni muhitaji lakini pamoja na uhitaji wake bado alikuwa anajitoa **(*Marko 12:41-44*)**.

Tunaona utoaji wa Dorkasi ambaye maisha yake yalikuwa yamejaa utoaji, yaani kujitoa kwa ajili ya watu wengine kulikuwa ni sehemu ya maisha yake na ndiyo ikawa sababu ya kufufuliwa

kwake. Dorkasi aligusa sana maisha ya wajane na tunaona kuwa wajane wanasimama na kuonesha mavazi ambayo walikuwa wanavalishwa na Dorkasi, wanatoa machozi yao mbele za Mungu wakati ambapo Dorkasi hawezi kujiombea **(*Matendo 9:36-41*).**

Mbali na Dorkasi, pia tunaona utoaji wa Mwanamke wa huko Shunemu ambaye anatimiza wajibu wake kama mama anayemjua Mungu kwa kuchukua jukumu la kumtunza mtumishi wa Mungu Elisha. Mungu hakukaa kimya katika kujitoa kwake, hivyo akampatia mtoto ambaye alikuwa ameomba kwa miaka mingi bila majibu lakini alipogusa maisha ya mtumishi wa Mungu ikawa sababu ya majibu ya maombi yake **(*2Wafalme 4:8-17*).** Katika ***Mathayo 10:42*,** Yesu Kristo anatoa ahadi kuwa kwa yeyote atakayejitoa kwa ajili ya watumishi wa Mungu hatakosa thawabu yake**.** Hicho ndicho kilichotokea kwa huyo mama wa Shunemu baada ya kujitoa kwa ajili ya mtumishi wa Mungu**.**

Utoaji mwingine wa kujitoa kwa wengine tunauona kutoka katika makanisa ya Makedonia (***2Korintho 8:1-15***). Mtume Paulo anaguswa na kujitoa kwa makanisa yale japo tunajua kuwa makanisa yale yalikuwa bado machanga kiroho lakini walijitoa katika kiwango kikubwa bila kujali hali zao za kiuchumi. Hii inatuonesha kuwa moyo wa utoaji hautazami mali ambazo mtoaji anazo au muda mrefu aliokaa katika wokovu bali ni upendo katika kujitoa kwa kujua ukuu wa Mungu. Pia tunaona utoaji wa Kornelio, yeye alikuwa akitoa sadaka nyingi kwa watu na tunaona jinsi ambavyo Mungu alivyoguswa na utoaji wake hata ikawa sababu yake kupata wokovu kamili **(*Matendo 10:1-4*).**

Hii ni mifano michache tu, lakini inatosha kuonesha jinsi ambavyo kila mtu anayo nafasi ya kumpendeza Mungu kwa njia ya matoleo bila kujali hali anayopitia na Mungu kwa wakati wake atatenda jambo juu yako katika mahitaji yako. ***Hivyo katika kupambania mahitaji yako jitahidi kushiriki kwenye mahitaji ya wengine pia***. Usisubiri mpaka umalize haja zako ndipo uhusike na maisha ya wengine. Wakati mwingine unaweza kusubiri na

haitatokea wakati ambapo haja zako zitatimia. Wakati mwingine mimi binafsi huwa nasaidia kulipa ada za watoto wa watu wengine wenye uhitaji bila kujali kuwa nitapata wapi ada kwa ajili ya watoto wangu lakini Mungu kwa wakati wake huwa anafungua milango na siyo mlango mmoja kwa ajili ya watoto wangu pia.

Mara nyingine huwa napanga bajeti ya kufanya mambo yangu fulani lakini ghafla anatokea mtu anaeleza jinsi ambavyo ametingwa na wakati mgumu anaopitia, hivyo najikuta naahirisha mambo yangu kwa ajili ya mtu kama huyo kwa imani kwamba Mungu atatenda kwangu pia. Lakini nikwambie jambo, mipango yangu huwa inachelewa kwa muda tu kwani ninapojitoa kwa ajili ya watu wengine, Mungu kwa wakati wake huwa analeta baraka zisizo za kawaida na ninajikuta nafanikiwa zaidi ya nilivyokusudia.

Kama nilivyodokeza hapo awali, sadaka zetu zitolewe mahali ambapo Mungu amepachagua, hivyo siyo kila atakayekuja kuomba msaada kwako atakuwa ameelekezwa na Mungu bali kadri ya mwongozo wa Roho Mtakatifu utajua ni wapi pa kupanda mbegu zako.

**Mungu Mtoaji wa Mavuno:**

Ukisoma maandiko katika ***Mathayo 7:11-12*** na ***Luka 6:32***, katika hali ya kawaida utaona kama vile yanamaanisha kuwa tutapokea fadhila za wema wetu kutoka kwa wale tunaowasaidia. Ukweli ni kwamba hazina za wema wetu zinahifadhiwa mbinguni na wala si kwa wanadamu. Mungu yeye mwenyewe huwainua wanadamu ambao watatufaa wakati wa mahitaji yetu. Katika ***Mathayo 6:1*** na ***Luka 6:35,*** tunaona zuio la kutenda wema huku tukitumai kupata kitu kwa wale tunaowasaidia. Haizuii kudai pesa au vitu ambavyo tumewakopesha wanadamu wenzetu bali tunazuiwa kuwasaidia kwa lengo la kulipwa wema huohuo kutoka kwao **(*Mithali 19:17*)**. Wengi waliosaidia kwa lengo la kulipwa fadhila kutoka

kwa wanadamu wamevunjwa moyo kwa sababu wengi hawakupata kile walichotarajia.

**Mbegu ya Kupanda na Mbegu ya Mavuno:**

Mbegu ya kupanda ni hali ya kujitoa kwetu kwa kazi ya Mungu au kwa ajili ya mahitaji ya watu wengine bila kupata malipo ya moja kwa moja huku tukitarajia kuvuna kwa wakati wake Mungu **(*Galatia 6:9; Mathayo 6:19-20*).** Katika ***Galatia 6:7*** tunapata uhakika kuwa mavuno hutokana na tunachopanda tena katika ***Galatia 6:10*** tunapata himizo la kuendelea kupanda bila kuchoka. Maandiko matakatifu yanadokeza habari ya watu ambao walipanda lakini kwa wakati wake Mungu walivuna.

Angalia mfano wa utoaji wa **Kornelio** katika ***Matendo ya Mitume 10:1- 4,*** **Dorkas** katika ***Matendo ya Mitume 9:36- 40,*** pamoja na utoaji wa makanisa ya Makedonia katika ***2Korintho 9:6-11.*** Hivyo, na sisi wakati wote tupande tukitegemea mavuno ni wakati wa Bwana.

Katika ***2Korintho 9:6*** tunaona habari ya mtu apandaye haba atavuna haba lakini pia katika ***2Korintho 9:10*** tunaona habari ya kupewa mbegu za kupanda na kuzizidisha. ***Hapa tunapata picha kwamba siyo kila Baraka tupatazo kutoka kwa Mungu huwa ni kwa ajili yetu tu bali Baraka zingine huwa ni mbegu ambazo Mungu hutupatia ili tuziongeze kwa kuzipanda na baada ya kuzipanda yeye mwenyewe atazizidisha na kuzifanya ziongezeke kwa wingi na kutufanya tuwe na riziki za kila namna.***

Wengi tunapenda kuvuna tu, hatupendi kupanda**.**Tukipewa mbegu za kupanda tunakula kisha tunabaki bila mavuno kwa sababu tulikula mbegu zetu. Mbegu zinazoongelewa hapa ni utoaji wa kila jinsi ambavyo Mungu atakuelekeza kupitia msaada wa Roho Mtakatifu iwe ni kutoa kwa watu wengine au madhabahuni pa Bwana. Omba Mungu akupe utambuzi wa kujua mbegu ya kupanda.

**Shetani Hung’oa Mapando**

Utoaji ulio kamili huambatana na kufuata mwongozo wa neno la Mungu. Kinachotokea ni kwamba, shetani huliondoa neno la Mungu katika moyo wa mtu anayepanda mbegu **(*Marko 4:15*)** ili afikirie kwamba anapopanda mbegu ama anapoteza au atalipwa na mwanadamu na wala siyo kuweka hazina mbinguni. Hali hii husababisha mpanda mbegu kuchukia na kupata majuto ya kujitoa kwa watu na kwa kufanya hivyo Shetani anakuwa amefanikiwa kung’oa mbegu uliyopanda. Utasikia mtu anasema kwa uchungu kabisa ***“najuta kukusaidia, yaani haya ndiyo malipo ya wema niliokufanyia?***

Watu wengi wanapenda kuwa wapandapo mbegu basi wavune hapohapo. Yaani kwa mfano, ukimlipia mtu ada ya shule basi naye akifanikiwa alipe kwa wanao au afanyike msaada kwako. Katika mbegu ya kupanda haipo hivyo, kwani utajitoa kwa wengine na kuvuna kutoka kwa watu wengine tofauti kabisa na wale uliojitoa kwao. Kuna wakati utasikia mtu anasema ***“mimi nimeshaapa kuwa sisaidii mtu tena”*** hapo unaelewa kwamba shetani ameshang’oa mapando yake yote si tu kwa yule aliyemkwaza lakini pia hata kwa wahitaji wa baadaye.

Ipo mifano kadha wa kadha katika maandiko matakatifu yanayoonesha jinsi ambavyo Shetani huharibu mapando ya watu. Angalia mfano wa Anania na mke wake ***Matendo ya Mitume 5:1-5,*** ambapo tunaona watu hawa ghafla wanabadili azima yao ya kutoa sadaka kamili na kujikuta wanaingia katika hukumu kali ya Roho Mtakatifu**.** Pia unaweza kukumbuka jinsi wana wa Israel walivyokuwa wamedhamilia kujenga hekalu la Bwana baada ya kutoka utumwani Babeli ghafla Shetani akaharibu nia zao na wakawa wamegeukia mambo yao binafsi mpaka wakati wa unabii wa **Hagai.** Watu wamekuwa wakianza na Mungu katika mambo yao labda kwa maombi ya kufunga lakini mwishoni Shetani anaingilia maombi yao na wanajikuta wanatenda dhambi au wanaharibu nadhiri za maombi yao.

Mtu anaweza kuwa katika maombi ili Mungu amsaidie afaulu mtihani wake lakini dakika za mwisho atajikuta anashawishika kumhonga mwalimu au msimamizi wa mtihani ili amsaidie. Mtu mwingine anakuwa katika maombi akiomba Mungu amsaidie ili apate kazi au apande cheo, ghafla anajikuta kushawishika kutoa hongo au kutumia hila ili kupata nafasi anayotaka. Siyo vibaya kuomba watu watusaidie lakini tusitafute msaada kwa kutumia mbinu ambazo zinatupelekea kutenda dhambi katika kufanikisha azima zetu.

**Mbegu ya Mavuno:**

Hii ni mbegu ambayo inahitaji uipande lakini tayari ipo na mavuno (***Waebrania 13:2***). Tofauti na mbegu ya kupanda, mbegu ya mavuno huwa tayari ina matokeo. Wapo watu ambao walipotoa sadaka kwa ajili ya jambo fulani, wakati huo huo Mungu akafungua milango ya baraka kwao. Wengi wangependa kukutana na mbegu kama hii lakini mbegu hii inakuja kutokana na mbegu ya kupanda. Kornelio alipojenga tabia ya kutoa kwa watu ndipo ulipowadia wakati wa kuvuna pale malaika alipomshukia na kumwambia sadaka zake zimekuwa ukumbusho mbele za Mungu ***(Matendo 10:30-31).***

Hivyo basi, ipo mifano ya watu mbalimbali katika maandiko matakatifu inayoonesha watu waliokutana na mbegu ya mavuno kwa wakati ambao Mungu mwenyewe alipenda: Ibrahim katika ***Mwanzo 18:2-10;*** mjane wa Sarepta***, 1Wafalme 17:10-16;*** mama wa Shunemu***, 2Wafalme* 4:8-17;** Akida***, Luka 7:2-5*;** Dorkas***i, Matendo 9:36-39*.** Huyu Dorkasi alitumika kwa watu ambao baadaye walifanyika baraka kwake. Wengi tungetamani iwe hivyo lakini hazina zetu kutoka mbinguni ni Mungu mwenyewe hupanga jinsi tutakavyozivuna.

**Kila Apandaye Huvuna:**

Katika ***2Korintho 9:6b,*** tunapata uhakika wa kuvuna kutokana na jinsi tulivyopanda na katika ***2Korintho 9:8,*** tunaona aina ya mavuno ambayo pia yanakuja na mbegu na kututaka kuendelea kupanda, tena tunaelekezwa kuzidi sana katika kutenda kila lililo jema. Katika ***2Korintho 9:10*** tunapewa mavuno ambayo ni mkate kuwa chakula kisha tunaona habari ya kuongeza mazao ambayo ni matunda ya mbegu tulizopanda.

Unaweza ukaona kama vile utoaji wako haujakulipa lakini nataka nikwambie kuwa hakuna apandaye bila kuvuna. Yapo mambo ambayo Mungu huyafunua waziwazi, moja kwa moja kwa mpanzi kwa ajili ya kumjengea imani lakini ukweli ni kwamba, yapo mambo mengi sana ambayo Mungu hutenda kwetu bila sisi kujua, hali hii inapelekea watu wengi kudhani kuwa hakuna matunda ya utoaji.

***Yale yanayofunuliwa kwetu huwa ni machache sana lakini tunahitaji kuwa na macho ya Rohoni kuyajua yote haya. Wapo watu ambao wamebarikiwa kupitia ndugu zao wa karibu kama vile mjomba, mwenza wa ndoa n.k lakini huwa hatuyaoni hayo.*** Kila mtu angetaka yeye mwenyewe awe na kazi au biashara nzuri lakini hatuoni ndugu zetu ambao Mungu amewainua kwa ajili yetu.

## 2. Zaka au Fungu la Kumi

Zaka au wengine huita sadaka ya fungu la kumi ina maana ya kuwa, kile kitolewacho ni sehemu ya kumi ya mapato yako yote. Hivyo basi, zaka ni aina ya sadaka inayotolewa kutoka katika sehemu ya kumi ya pato lako lote. Sadaka hii ni ya kipekee kuliko sadaka nyingine, upekee wake ni kwamba sadaka nyingine ***unatoa*** bali hii ***unalipa***. Kwa maana kitendo cha kutoa ni kitendo cha ***hiyari*** ya mtu bali kitendo cha kulipa ni kitendo cha ***lazima*.** Katika vile vitu ambavyo Mungu ametoa kwetu hututaka tutoe

asilimia kumi si kwamba Mungu ni muhitaji au ni masikini hivyo anataka tumpe vitu vyetu, la hasha anapima upendo wetu kwake. Biblia inatuambia wazi ya kuwa dunia na vyote vijazavyo ni mali yake, fedha na dhahabu vyote ni vyake.

Mungu anachotaka kuona kwangu na kwako ni ule uelewa na uaminifu wetu kwake kwa vyote alivyotupa. Je? Tunafahamu ya kuwa tulivyo navyo vyote ni mali yake? je kuwepo hivyo vitu mikononi mwetu tunaelewa ya kuwa Mungu anahusika? Ndiyo maana amedai au ametaka sehemu ndogo sana turejeshe kwake katika sehemu kubwa aliyotupatia na kwa sababu hiyo anachotafuta Mungu hapa ni upendo na uaminifu wetu kwake. Ndiyo maana fungu la kumi halihusiki tu katika agano la kale bali hata agano jipya kwa sababu upendo na uaminifu ndiyo maisha ya mtakatifu wa agano la kale na jipya.

*Tangu mwanzo hata kabla ya wakati wa Torati ya Musa, watu walikuwa na desturi ya kutoa zaka ya mapato yao kwa Mungu kama tendo la ibada na shukrani. Walitambua kuwa Mungu ndiye mtoaji mkuu wa Baraka na nguvu maishani mwao*. Ilikuwa ni desturi ya kujitoa kwa hiari bila kulazimishwa kabla ya kuwa jambo la lazima katika sheria ya Musa.

Katika Biblia kuna mifano ya watu wawili ambao walitoa zaka kabla ya sheria ya Musa na kufanya jambo hili kuwa la lazima. Ibrahimu, baada ya kupata ushindi mkubwa katika nchi aliyoahidiwa na Mungu alimtolea Mungu zaka (***Mwanzo 14:17-24; Waebrania 7:4-10***). Naye Yakobo, alipokimbia kwa usalama wake katika nchi ya mbali aliahidi kumpa Mungu zaka (***Mwanzo 28:20-22***).

**Zaka Katika Sheria ya Musa**

Waisrael walipaswa kumtolea Mungu zaka ya nafaka, matunda na mifugo. Zaka iliyotolewa ilipaswa kuwa ***mfano wa uaminifu*** wa mtoaji katika mali yake wala si sehemu ***duni au dhaifu*** ambayo

hakuwa na haja nayo (***Mambo ya Walawi 27:30,*** *32-33*). Kama mtu hakutoa zaka yake kwa wakati, alitakiwa kutoa nyongeza ya ***asilimia 20*** ikiwa kama faini ya kushikilia kitu ambacho alitakiwa kukitoa kwa Mungu (***Mambo ya Walawi 27:31*****).** *H**ii inaonesha kuwa mpango wa Mungu ni kuwa kila mtu apeleke fungu la kumi kwa wakati muafaka, bila kuchelewesha.***

Tusilimbikize fungu la kumi kwa sababu yoyote ile, kwa sababu fungu la kumi ni mali ya Mungu tangia ilipoingia mikononi mwako**.** Wapo watu wanaolimbikiza fungu la kumi na matokeo yake fungu linaongezeka na kuwa kubwa na hatimaye wanashindwa kulitoa au wanatoa sehemu ndogo kabisa ya kile kilichotakiwa kutolewa**.** ***Sadaka anayostahili Mungu inabidi kutolewa kwa muda mwafaka vinginevyo inaleta hukumu*****.**

Katika kitabu cha ***Hagai 1:2,*** wana wa Israel waliotoka utumwani Babeli walitakiwa kujenga upya hekalu la Bwana, walipokutana na vipingamizi katika ujenzi waliacha kazi ya ujenzi na kusema wakati wa Bwana haujafika, waliendelea na maisha yao huku hekalu la Bwana likichakaa**.** Tunaona hukumu ya Bwana juu yao ikawashukia (***Hagai 1:6*****).**

Hata kama ni jukumu ambalo Mungu amenena na wewe kulifanya, ni muhimu kufanyika ndani ya wakati wa Bwana na siyo unavyoona inafaa. Utoaji wa fungu la kumi pungufu ya kiwango sahihi ni kuvuna laana mbele za Mungu ***kwa sababu utoaji ni kipimo cha imani, upendo na uaminifu wa mwanadamu kwa Mungu*** **(*****Malaki 3:8-9*****)**. *Utoaji wa zaka kwa Waisrael ulipangwa na kuratibiwa kama sheria ya Musa ilivyoelekeza, lakini pamoja na hayo utoaji huo uliweza kuwa ishara ya mtoaji jinsi alivyojitoa kwa Mungu. Pia utoaji ule ulionesha jinsi ambavyo Mungu alivyokusudia utoaji wetu uwe wa namna gani kwake hadi wakati huu.*

**Zaka Katika Agano Jipya**

Miaka ya baadaye baada ya kifo cha Musa, walimu wa kiyahudi waliongeza sheria zao juu ya zile zilizotolewa na Musa katika utoaji wa zaka**.** Walifanya zaka iwe mzigo mzito sana kwa Wayahudi wa kawaida. Walimu wale walikuwa hawatekelezi yale waliyokuwa wakifundisha, pia hawakufundisha wala wao hawakufanya mambo muhimu kama vile **Imani, upendo na haki (*Mathayo 23:4, 23; Luka 11:42, 46; 18:12*).**

Hivyo, katika Agano Jipya, Yesu anasisitiza utoaji unaoambatana na upendo, amani na haki **(*Mathayo 23:23*)** na anawaonya watumishi wanaowatwika mizigo ya sadaka waumini wao, huku wenyewe wakijiweka kando katika utoaji. Neno la Mungu linatufundisha kuwa, viongozi wa kanisa wanatakiwa kuwa mfano wa yale wanayofundisha (**utoaji**) na siyo kuwa, wasemaji tu na kuwatwisha wamini mizigo ambayo wao wenyewe hawapo tayari kuibeba.

Mungu hapendi kuwapeleka watu katika umaskini kwa sababu ya sadaka **(*2Korintho 8:12-14*),** ingawa anawasifu wale wanaotoa kupita kiasi ambacho wangeweza kutoa kwa kawaida (***2Korintho 8:3***). Neno la Mungu linatuelekeza kuwa utoaji wa sadaka hautakiwi kuwa sababu ya kufanya waumini kuwa masikini kwa kuwalazimishwa kutoa zaidi ya uwezo wao, japo wenyewe wanaweza kufanya hivyo kama wakiamua bila kulazimishwa.

Tangu mwanzo Bwana Mungu alipanga utaratibu mzuri wa kulipa zaka kama sehemu ya kumi ya kila pato (***Walawi 27:32****)*. Kwa sababu kila kitu ukipatacho chatoka kwa Bwana, Bwana anataka **usile vyote** bali sehemu ya kumi **umrudishie yeye** kwa ajili kuujenga **ufalme wake (*Malaki 3:10-11*)**. Lakini ni lazima ujue kwamba sasa hatupo chini ya sheria bali tunaongozwa na Roho Mtakatifu. Hivyo, chochote ukifanyacho katika ufalme wa Mungu ni lazima kitoke moyoni na siyo utoaji kwa sababu ya kutimiza wajibu tu.

Hivyo basi, fungu lako la kumi hutakiwi kulipa kwa sababu tu ya kutii sheria bali ulipe ukiongozwa na upendo wa Mungu. Mfano: mtu akiwa na kipato cha TSh 532,000/= basi siyo lazima atoe TSh **53,200/**= kama sehemu ya kumi ya kipato hicho bila kuongeza chochote (**wengi hufanya hivyo ila hufungwi kufanya hivyo**). Bali badala ya kulipa TSh 53,200/= unaweza kutoa zaidi, kwa mfano: **53,500** au **54,000** kama sehemu ya kumi ya kipato hicho.

Yeye asiyefungwa na sheria atafikiria zaidi upendo wake kwa Mungu bila kujali kwamba anachotoa ni zaidi ya kilichoamuliwa. Ikumbukwe kuwa kiasi chochote kinachozidi kiasi halisi cha fungu la kumi kitachukuliwa kama sadaka yako ya upendo mbele za Bwana. Hata hivyo, yeye atakeyetoa TSh **53,200** na yule atakayetoa zaidi ya TSh **53,200** wote watahesabiwa haki mbele za Mungu.

Jambo la kuzingatia ni ***kutotoa chini ya kiwango kilichoamuliwa***, wapo watu ambao siku ya kutoa fungu la kumi huwa hawatoi sadaka nyingine ya upendo, hii siyo sahihi. Usahihi ni kwamba fungu la kumi katika kipato chako huwa tayari ni sehemu ya Mungu moja kwa moja ndiyo maana tunalipa fungu la kumi. Hivyo, ni vyema uandae sadaka yako ya upendo pembeni ya sadaka yako ya fungu la kumi.

**Bwana Yesu Anasemaje Kuhusu Zaka (*Mathayo 23:23; Waebrania 7:5-10)***. Katika ***Mathayo 23:23,*** Yesu Kristo anazungumzia suala la zaka kwamba linapaswa kuendelezwa kuwepo kama kawaida. Ndio maana anasema hayo mambo ya zaka wala msiyaache. Waandishi na mafarisayo walikuwa wakijitahidi kulipa zaka kama kutimiza sheria na lakini si kama Bwana atakavyo. Ndivyo ilivyo hata leo, wapo watumishi wenye jitihada nyingi za kulipa zaka kama kutimiza tu sheria na siyo suala linaloanzia mioyoni mwao. Waandishi na mafarisayo, waliyaacha mambo muhimu ya imani ndipo Bwana akawaambia "*ole wenu*" kwa sababu wokovu ni zaidi ya zaka na sadaka, bali ni jumla ya maisha yote tunayoishi.

**Je, Fungu la Kumi Linatoka Wapi?**

Fungu la kumi linatoka katika kipato chako, iwe ni faida katika biashara au mshahara au chanzo chochote cha kipato ambacho ni halali mbele za Mungu. Hupaswi kulimbikiza sadaka yako ya fungu la kumi kwa kigezo kwamba utalipa mwisho wa mwaka au baada ya miezi Fulani. Zaka au fungu la kumi linatakiwa lilipwe haraka upatapo pato lako **(*Walawi 27:31*)**, wengi wao wanaolimbikiza fungu la kumi mwishowe huwa linawaelemea kisha kushindwa kutoa fungu kamili.

**Je, naweza kulipa michango ya kanisani kwa kutumia fungu la kumi?**

***Jibu ni hapana.*** *Fikiria mfano huu: mtu anakudai pesa yake lakini pia mtu huyo ana sherehe nyumbani kwake na umeahidi kumchangia pesa ya sherehe. Je? unaweza kumpa pesa anayokudai au sehemu ya pesa anayokudai kisha ukasema umechanga kwa ajili ya sherehe? Bila shaka utakuwa umelipa pesa uliyokuwa unadaiwa na wala siyo mchango.*

***Ndivyo ilivyo katika fungu la kumi, huwezi kutumia pesa ambayo tayari ni mali ya Mungu kisha ukasema umechanga kwa ajili ya kazi ya Mungu, Fungu la kumi tayari ni mali ya Mungu, hivyo Mungu hawezi kujichangia mwenyewe kwa mali yake.***

**Je, Naweza Kutoa Zaidi ya 10% kama Fungu la Kumi?**

Fungu la kumi linabaki kuwa ni sehemu ya kumi ya kipato cha mtoaji ila tunapotoa fungu la kumi ni vizuri tuambatanishe na sadaka ya upendo tunayotoa kila siku ya ibada. Katika ***Luka 11:42,*** utaona kuwa msisitizo wa Yesu Kristo unabaki kuwa ni utoaji wa zaka kama Agano la Kale lilivyoelekeza.

Tunafahamu kuwa utoaji huo ulielekezwa kuwa ni sehemu ya kumi ya pato lote la mtoaji (***Walawi 27:32; Mwanzo 14:17-24; 28:20-22***). Lakini katika Agano Jipya, utoaji wa fungu la kumi unabaki vile vile isipokuwa suala la upendo linaongezeka katika utoaji wa sasa. Kutokana na mahusiano (upendo) kati ya mtoaji na Mungu, mtu anaweza kutoa zaidi ya 10% kama matoleo yake kwa Mungu lakini fungu la kumi litabaki kuwa ni 10% ya pato la mtoaji. Hicho kinachozidi kinakuwa ni sadaka ya hiyari mbele za Mungu, kutokana na jinsi ambavyo mtoaji mwenyewe anavyoguswa na utoaji. Wapo watu ambao wanatoa mishahara yao yote kanisani wakiita kuwa fungu la kumi na wapo wengine wanatoa 10% kisha sehemu ya kiasi kinachobaki wanatoa sehemu tofauti tofauti kama vile: michango kanisani, sadaka kwenye ibada, kusaidia wahitaji mbalimbali n.k.

Wote hawa wapo sawa katika kumtolea Mungu yaani wote wanamtolea Mungu. kutokana na utoaji huo ambao pengine unazidi kiwango cha kawaida katika utoaji, wapo wachungaji na wahubiri mbalimbali ambao wanataka utoaji huo uwe kama utaratibu mpya wa utoaji wa fungu la kumi. Utasikia mtu anasema watu watoe 20% n.k, hii si sawa kwa sababu hakuna sehemu katika maandiko matakatifu inayodokeza ulipaji wa fungu la kumi kuwa fungu la 11 au zaidi. Utoaji wa fungu la kumi utabaki kuwa 10% na zaidi ya hapo ni sadaka ya upendo tena ya hiyari kabisa kwa Mungu ambapo hata mtu asipozidisha 10% hawezi kulaaniwa kwamba amemuibia Mungu ila akipunguza akatoa chini ya 10% atalaaniwa sawa sawa na maandiko matakatifu (***Malaki 3:8-9***), zaka kamili ni sehemu ya kumi ya mapato yako yote.

### 3. Malimbuko (Mithali 3:9-10)

Limbuko ni zao la kwanza la kazi ya mikono yako (**First Fruits**). Sadaka ya limbuko ni ishara ya kumheshimu Mungu kuwa ndiye chanzo cha baraka zetu na mtoaji mkuu wa mali zetu. Ukimtambua Mungu kwa namna hiyo***; kwamba yeye ndiye***

***chanzo cha baraka zetu atakubariki zaidi na kukuzidishia katika yote unayoyatarajia au unayofanya.***

Kutokana na Torati ya Musa, Wanaisrael walipaswa kumpa Mungu vitu vya kwanza katika mavuno yao. Hivi vitu vilikuwa matunda au nafaka, vilitolewa ili kuonesha shukrani kwa Mungu kwa mavuno yote (***Kutoka 22:29; 23:19; 2Nyakati 31:5, 6-11).*** Waliweza kutoa ama mikate au Keki iliyotengenezwa kwa unga au kutoa kikapu chenye unga ama matunda (***Hesabu 15:17-21; Kumbukumbu la Torati 26:2*****).**

Sadaka za malimbuko zilikuwa mali ya makuhani kama sehemu ya riziki yao **(*Hesabu 18:8, 12-13*).**

***Malimbuko yalikuwa ni ishara ya matumaini au dhamana ya vitu vikubwa zaidi vilivyotazamiwa kutoka kwa Mungu***. Kwa hiyo, hii ni sadaka inayotolewa kwa Imani kwamba Mungu ametenda na atatenda Zaidi.

Kristo aliyefufuka anaitwa limbuko la waamini waliokufa kwa sababu kufufuka kwake ni dhamana na uhakika wa ufufuo wa waumini wote (***1Korintho 15:20, 23***). Kama vile malimbuko ya Waisrael yalivyokuwa matunda bora ya mavuno yao, vivyo hivyo Mungu anataka Wakristo wa leo wawe viumbe bora katika uumbaji wake bora, hata wao ni mali ya Mungu kwa namna ya kipekee **(*Ufunuo 14:4*).** Unapoona kuwa watu wamekosa moyo wa kumtolea Mungu malimbuko ya kazi zao, tambua kuwa aidha hawana uelewa wa aina hii ya sadaka au imani (matumaini) yao kwa Mungu ni madogo sana (Yaani hawaamini kuwa wakitoa kwa Mungu watapokea zaidi). Hivyo kwao hata hicho kidogo walichopata wakitoa watapata hasara kwa sababu hawana uhakika wa kupata kingine.

Lakini anayelijua neno, anampenda, anamheshimu na anamwamini Mungu hawezi kuona shida katika kumtolea Mungu malimbuko kwa sababu anajua kuwa kwa kufanya hivyo

matumaini yake ya kupata vitu vingi zaidi yatafunguliwa. Asiye na imani na Mungu kila mara anapofikiria kutoa huona zaidi nafasi ya kupoteza kuliko kupokea. Yaani yeye kutoa anaona ni kama kucheza kamali au kupoteza kabisa hivyo hawezi kutoa kikubwa wakati hana imani ya kupokea zaidi. Lipo tumaini tukimtolea Mungu kwa uaminifu, jenga tumaini lako kwa Mungu kwa kumtolea Malimbuko ya kazi zote za mikono yako.

### 4. Sadaka ya Nadhiri

Nadhiri ni matoleo ya hiyari ambayo mtu anajifunga mwenyewe kwa Mungu kwa kutaka Mungu amtendee jambo fulani analolihitaji. Mara zote mtu hutoa bila kulazimishwa na mtu yeyote. Ukitoa nadhiri ni **lazima uiondoe kwa vyovyote vile, vinginevyo inakuwa dhambi mbele za Mungu.** Watu wengi wana matatizo katika maisha yao ambayo wao wenyewe hawajui yametokana na nini, lakini ni kweli kwamba baadhi ya matatizo yanatokana na kutokuwa mwaminifu mbele za Bwana katika nadhiri **(*Walawi 7:16; Hes 15:1-3; Kumbukumbu la Torati 23:21-23*).**

### 5. Sadaka ya Shukrani

Kama zilivyo aina zingine za sadaka, sadaka ya shukrani ni sehemu ya kumwabudu na kumtukuza Mungu kwa ukuu wake (***Zaburi 50:23*).** Sadaka hii hutolewa bila kujali kwamba Mungu amejibu au hajajibu maombi ya mtoaji kwani kupata au kukosa yote yaweza kuwa ni mapenzi ya Mungu. Wakati mwingine mtu anaweza kuona kuwa hajajibiwa maombi yake kumbe kwa sababu ameomba vibaya **(*Yakobo 4:3*)** au wakati wa Mungu haujafika kwani Mungu hutupatia vilivyo vyema zaidi yetu sisi tufanyavyo kwa wanadamu wenzetu (***Mathayo 7:9-11*)**.

Neno la Mungu linatutaka tushukuru kwa kila jambo (***1Thesalonike 5:18, Wafilipi 4:6)***. Maelekezo ya utoaji wa sadaka ya shukrani yalikuwepo hata wakati wa Torati ya Musa

(***Walawi 7:11-13***). Pia tunaona wakati wa Agano Jipya, Yesu Kristo anafurahia karamu aliyoandaliwa na Martha kama sherehe ya kumshukuru baada ya kumfufua Lazaro ***(Yohana 12:1-3; Marko 14:3-9*****).**

Mungu anapenda watu walio na mioyo ya shukrani, hivyo tunapotendewa matendo makuu na Bwana tunapaswa kushukuru siyo tu kwa mema bali hata kwa yale tunayoona machoni petu kuwa yana maumivu kwetu. Ukisoma katika ***Luka 17:12-19,*** utaona utakaso wa ukoma unatokea kwa wakoma kumi lakini ni mkoma mmoja tu aliyekumbuka kurudi kumshukuru Mungu kwa utakaso alioupata**.** Katika andiko hili tunaona kuwa watu wengi huwa wanapoteza baraka zao au majibu ya mahitaji yao kwa kushindwa kurudi kumpa Mungu utukufu kwa njia ya shukrani baada ya kuwatendea matendo makuu.

Yaani huwa tunaacha sehemu kubwa ya majibu ya maombi yetu baada ya kupokea sehemu ndogo tu ya majibu kwa kutokuwa waaminifu katika kushukuru. Kila mtu anayo sababu ya kumshukuru Mungu, iwe ni kwa kulinda kazi yake, ndoa, afya, watoto, wazazi, huduma yake, riziki ya kila siku, kufaulu mitihani n.k

Baada ya Nuhu kuokoka katika ile gharika, akamtolea Bwana sadaka nzuri ya shukrani ambayo ilikuwa sababu ya Mungu kutoa agano la kutoangamiza tena dunia kwa gharika (***Mwanzo 8;21-22*****).** Kumbuka katika gharika ile waliokoka watu 8 tu. Hii ni kusema kwamba mbali na watoto na mke wa Nuhu, ndugu zake Nuhu wote walikufa katika ile gharika. Kama umewahi kufiwa na ndugu zako wa karibu utaelewa maumivu aliyokuwa nayo Nuhu kabla ya kutoa ile sadaka. Kwa hiyo ule moyo wa kutoa sadaka nzuri mbele za Mungu mara baada msiba kama ule halikuwa jambo la kawaida. Ingekuwa ni mimi na wewe labda tungekuwa na moyo mzito uliojaa manung’uniko badala ya shukrani. Utoaji wa jinsi hii unaonekana kumgusa Mungu na hivyo kusababisha aseme jambo juu ya Nuhu.

**Maandalizi ya Sadaka ya Shukrani**

Ni kawaida kwa mwanadamu anayejitambua kufanya maandalizi endapo kuna jambo lolote la muhimu analoenda kulikabili siku za usoni. Maandalizi husaidia mtu kufanya jambo hilo kwa ufanisi zaidi kuliko ambavyo angelifanya bila maandalizi. Ndivyo ilivyo hata lilipokuja suala la utoaji wa sadaka ya shukrani **(*Mithali 16:1*)**. Kwa kuzingatia umuhimu wa sadaka hii mbele za Mungu, mtoaji hana budi kufanya maandalizi yafuatayo:

a) **Utakaso wa Moyo**: Izingatiwe kuwa, moyo unaobeba sadaka ya shukrani ni wa muhimu sana pengine kuliko sadaka yenyewe. Hivyo tunapojiandaa kutoa sadaka ya shukrani tuanze na maandalizi ya mioyo yetu mbele za Mungu. Mara nyingi tunapomwendea Mungu kwa ajili ya mahitaji yetu huwa tunajinyenyekeza hata kwa maombi ya kufunga lakini Mungu anapotujibu huwa tuaenda na sadaka tu bila maandalizi ya moyo. Wengine wanadhani kuwa hiyo sadaka ya shukrani ni kubwa sana kiasi cha kulinganishwa na wema wa Mungu aliotenda maishani mwao.

   Hakuna kitu ambacho mwanadamu anaweza kufanya kikalingana au hata kukaribiana na upendo wa Mungu juu yetu. Hivyo kabla ya kutoa sadaka ya shukrani anza na maandalizi ya moyo wako ikiwa ni pamoja na maombi ya kufunga kisha andaa sadaka yako ya shukrani kwani sadaka huwa ni hitimisho la kitokacho katika moyo wa mtoaji. Katika ***1Wafalme 8:1-11*** na ***Nehemia 12:30*** tunaona utoaji wa sadaka ya shukrani unaoanza na maandalio ya moyo ili kumkaribisha Mungu ahusike na utoaji wa sadaka ya shukrani. Pia tunaona Nuhu katika ***Mwanzo 8:20,*** ambapo anaanza na kutengeneza mazingira ya uwepo wa Mungu kabla ya utoaji wa sadaka. Hivyo maandalizi ya moyo wako ni muhimu ili kuleta uwepo wa Mungu juu ya sadaka unayoenda kutoa.

b) **Kusogeza mbele za Bwana yale ambayo unaona kuwa una sababu ya kumtolea Mungu sadaka ya shukrani (*1Wafalme 8:22-25*)**. Hapa unamweleza Mungu kwa njia ya maombi yale ambayo Mungu ametenda kwa ajili yako. Unamwendea Mungu kwa njia ya maombi ili akutane na moyo wako wa shukrani. Jambo hili linaweza kufanyika siku ya ibada ya sadaka ya shukrani au siku kadhaa kabla ya siku ya utoaji wa sadaka husika. Ukiwa na muda wa maombi utapata wakati ambao Mungu atasema na wewe kuhusu aina ya sadaka utakayotoa, mahali utakapotoa na kiasi cha sadaka utakachotoa.

c) **Sadaka:** Moja ya maandalizi ya ibada ya shukrani ni sadaka yenyewe ambayo itatolewa kama hitimisho la ibada hiyo. Utoaji wa sadaka katika ibada ya shukrani huwa ni hitimisho la maandalizi ya ibada hiyo. ***Majibu ya kiasi gani cha sadaka, aina gani ya sadaka na wapi utatoa sadaka, huwa yanapatikana wakati wa maombi ya kujiandaa na sadaka ya shukrani.*** Wakati huu wa maombi huwa unakutana na Roho Mtakatifu na atasema na wewe kuhusu sadaka utakayotoa. Watu wengi huandaa sadaka kabla ya kuongea na Mungu kwa njia ya maombi. Hali hii husababisha mtu kutoa sadaka aliyopanga mwenyewe pengine tofauti na sadaka ambayo Mungu angemsemesha kuitoa. Ni vizuri ukapeleka kwa Mungu kwa njia ya maombi kusudio la kutoa sadaka ya shukrani kisha Mungu atakusemesha kuhusu kiasi cha kutoa.

**Jinsi ya Kushiriki Katika Ibada ya Sadaka ya Shukrani**

Yapo mambo kadha wa kadha ambayo yanahusika katika kuifanya ibada ya sadaka ya shukrani iwe na ukamilifu. Baadhi ya mambo hayo ni kama yafuatayo:

a) **Uimbaji**: Kuimba ni moja ya sehemu ya ibada ya kumshukuru Mungu. Hii inatokana na ukweli kwamba wakati mwingine huwa tunashindwa kuelezea uzuri wa

Mungu wetu hivyo tunaimba ili mioyo yetu yenyewe ielezee uzuri huo (***Zaburi 107:22, 92:1; Kutoka 15:1; Nehemia 12:27-28, 40-42***)

b) **Kushuhudia matendo makuu ya Mungu kwa maneno ya kinywa chako**.

Katika ***1Wafalme 8:12-20,*** tunaona kuwa Mfalme Suleiman anashuhudia kwa kinywa chake mbele za wana wa Israel yale ambayo Mungu amemtendea. Tunaona pia katika ***Luka 17:12-19,*** yule mkoma aliyetakasika akirudi kwa furaha na kushuhudia ukuu wa Mungu. Kwa hiyo jiandae kueleza uzuri wa Bwana katika ibada ya shukrani kwani kwa kufanya hivyo utasababisha watu wengi kupona kupitia ushuhuda wako.

c) **Kuomba**: Maombi nayo ni sehemu ya ibada ya sadaka ya shukrani. Pamoja na kwamba wakati wa maandalizi ya utoaji wa sadaka ya shukrani ulienda katika maombi, hiyo haotoshi. Wakati wa ibada yenyewe inabidi uisogeze hiyo sadaka ya shukrani mbele za Mungu. Yaani unaunganisha moyo wako ulioibeba ile sadaka pamoja na Mungu (***1Wafalme 8:22-25***).

d) **Kutoa Sadaka**: Hitimisho la ibada ya shukrani ni utoaji wa sadaka yenyewe ***(1Wafalme8:62-66; Nehemia12:43-44; Yohana12:1-3).*** Katika ibada ya kumshukuru Mungu ni vizuri ukaambatanisha shukrani yako pamoja na sadaka ya upendo, kwa sababu sadaka yako lazime itaambatana na moyo wako.

## Faida ya Sadaka ya Shukrani

Watu wengi huwa wanapoteza baraka zao za ziada au majibu ya mahitaji yao kwa kushindwa kurudi kumpa Mungu utukufu kwa njia ya shukrani baada ya kuwatendea matendo makuu. Yaani huwa tunaacha sehemu kubwa ya majibu yetu baada ya kupokea sehemu ndogo tu ya majibu kwa kutokuwa waaminifu katika kushukuru **(*Luka 17:12-19*).**

Kumshukuru Mungu kunatupa nafasi ya kupewa Baraka za ziada kama tulivyoona hapo juu huyo mkoma aliyerudi kumshukuru Yesu baada ya kutakasika ukoma. Wale tisa ambao hawakurudi, waliondoka na Baraka ya kutakasika tu lakini huyo aliyerudi alipata Zaidi ya kutakasika. Ipo faida pia kwa wale wanaosikia ushuhuda wako, kwani kuna watu wanapitia changamoto kama zako hivyo unavyoshuhudia jinsi Mungu alivyokuvusha, huwatia moyo wengine nao kuvuka kwenye mapito yao.

**Ushuhuda:** Mwaka 2020 niliugua ugonjwa wa kujaa maji kifuani, lilikuwa ni tatizo kubwa sana ambalo liliogopesha watu wengi wa karibu na mimi. Namshukuru Mungu nilipona. Baada ya kupona, ilibidi nijiandae kwa ajili ya sadaka ya shukrani, nilifuata hatua zote za maandalizi ya kutoa sadaka ya shukrani kama zilivyoelezewa hapo juu.

Niliposimama kutoa sadaka ya shukrani nilianza na ushuhuda wa tatizo lilivyokuwa na jinsi ambavyo nilipata uponyaji kutoka kwa Mungu.

Huwezi amini, wakati nashuhudia, kumbe kuna mtu alikuwepo katika ile ibada akiwa na tatizo la kujaa maji tumboni na kifuani. Yeye alikuwa ameambiwa na daktari kuwa yale maji yalikuwa yamesababishwa na tatizo la saratani. Baada ya siku kadhaa kupita, yule mtu alienda kumshuhudia mshirika mwingine wa hapo kanisa jinsi alivyotiwa moyo na ushuhuda wangu na kwamba alipata nguvu ya Imani kuwa na yeye anaweza kupona. Anasema "alipata nguvu ya ajabu mno ya kuamini katika uponyaji wa tatizo lake".

Haukupita muda mrefu madaktari wakamwambia tatizo lake linaendelea viziru, na kweli baada ya miezi kadhaa ya matibabu, vipimo vilionyesha kuwa amepona kujaa maji pamoja na saratani. Hadi leo yupo mzima wa afya njema. *Nakusihi, usikae kimya na ushuhuda wa mambo makuu ambayo Mungu amekutendea.*

*Uponyaji wa watu wengine wanaopita katika changamoto kama zako, wanategemea ushuhuda wako ili nao wapone.*

**Baadhi ya Mifano ya Watu katika Biblia walioshiriki Katika Kutoa Sadaka ya Shukrani ni kama vile:**

1. Mfalme Sulemani baada ya ujenzi wa Hekalu **(*1Wafalme 8:62-66*)**
2. Nehemia baada ya ujenzi wa ukuta wa Yerusalem **(*Nehemia 12:43*)**
3. Familia ya Lazaro baada ya Lazaro kufufuliwa **(*Yohana 12:1-3*).**
4. Nuhu baada ya kutoka katika gharika **(*Mwanzo 8:21-22*)**
5. Wana wa Israel baada ya kuvuka bahari ya Shamu **(*Kutoka 15*)**

Hivyo utaona kuwa utoaji wa sadaka ya shukrani ni sehemu ya ukamilifu wetu katika kuthamini utendaji wa Mungu juu ya maisha yetu.

**Upinzani Katika Kutoa Sadaka ya Shukrani**

Utoaji wa sadaka yoyote ya kumpendeza Mungu ikiwemo sadaka ya shukrani, siyo jambo jepesi. Sadaka hii hukutana na upinzani sana kutoka kwa shetani kwa sababu sadaka ya shukrani hutangaza ushindi dhidi ya adui na ndiyo maana sadaka hii huwa inapata upinzani mkubwa sana kutoka kwa Ibilisi (***Yohana 12:4-8; Marko 14:4-8*).** Katika maandiko hayo tunaona kuwa Yuda pamoja na baadhi ya watu wengine wanachukia kutokana na sadaka aliyoitoa Mariamu, hizi roho za chuki juu ya watu wanaojitoa katika sadaka ya shukrani hazikukoma, zipo hata leo**.**

Watu wanapojitoa kumshukuru Mungu kwa sadaka nzuri, wapo watu ambao huwa wanaumia ndio maana utasikia wengine wanasema kwani ilikuwa lazima aje kututangazia mambo yake, si angeshukuru mwenyewe kimya kimya. Hizo roho zisikunyamazishe kusimama mbele ya madhabahu ya Bwana kushuhudia ukuu wa Bwana, tena simama ukiwa na sadaka nzuri iliyobeba moyo wako wa shukrani.

## *Sura Ya Nne*

## KAZI ZA SADAKA

---

Mungu aliweka msingi kwamba, sadaka inatakiwa itolewe ili kiwemo chakula katika nyumba yake kwa ajili ya kuujenga Ufalme wake (***Malaki 3:10*****).** Uhitaji wa uwepo wa chakula madhabahuni ni ili iwe sehemu ya ghala la chakula kwa ajili ya kushibisha watoa huduma wa Bwana pamoja na watu wenye mahitaji mbalimbali ***(Kumbukumbu la Torati 14:28-29; 26:12-15)***.

Yaani ni kusema kuwa zaka na sadaka zinapofika madhabahuni zinakuwa siyo mali ya mtu ama kundi la watu fulani tu bali ni sehemu ya kukusanya ili igawanywe katika kufanya kazi ya Mungu. **(not final destination, rather it is** a **center for destination)** Hii ni kusema kwamba zaka na sadaka zitumike kulisha wafuatao:

1. **Wanaotoa Huduma katika Madhabahu** (Wachungaji, Walimu, Wainjilisti, Waimbaji na wengine wote wanaotumika kwa namna moja ama nyingine katika kuujenga Ufalme wa Mungu)

Katika Torati ya Musa, Mungu alielekeza kuwa zaka na sadaka zote kwa pamoja zitumike kama ***riziki ya Walawi***. Hii ni kwa sababu Walawi walitumia muda wao wote kwa ajili ya kazi ya Mungu, hivyo hawakuwa na nafasi ya kujipatia kipato kwa njia ya kufanya kazi za kawaida (***Hesabu 18:21-24*****).** Hata hivyo,

Walawi nao baada ya kupokea zaka, walitakiwa kutoa fungu la kumi katika hizo zaka walizozipokea kutoka kwa Wanaisrael. Zaka yao ilikuwa ni riziki ya Makuhani **(*Hesabu 18:25-29*).**

Kama ilivyokuwa wakati wa Agano la Kale hata leo katika Agano Jipya watumishi wa Bwana (watu wanaojitoa katika huduma za Kristo) wanakula madhabahuni **(*1Korintho 9:13-14; Galatia 6:6; 2Korintho 8:1-7; Luka10:4-8*)**. Wapo watu ambao wanatumia muda wao wote kuwa kanisani kwa ajili ya kuhakikisha kuwa huduma ya Bwana inafanyika kama ilivyopangwa, watu hawa bila shaka watalishwa madhabahuni. Kutoa kwa ajili ya wainjilisti na kazi ya Injili kwa ujumla wake pia kunahusu wale watu ambao wameacha familia zao na wanatumia muda wao mwingi kwa ajili ya kupeleka injili **(*Wafilipi 4:14-16; 3Yohana 1:7-8*)**. Ikiwa wanaostahili kupokea posho za huduma zao wanaamua wenyewe kutupokea, fungu lao laweza kutumika kwa ajili ya makundi mengine ya uhitaji **(*2Korintho 11:8-9, 2Thesalonike 3:8-9*).**

Ni vyema pia ifahamike kuwa, siyo kila ukifanya kazi ya Bwana lazima ulipwe posho, kwa sababu wapo watu ambao Mungu amewabariki na kwamba wanaweza wenyewe kujihudumia bila kuhitaji sadaka ya ziada kutoka kwa hao uliowahudumia. Na wakati mwingine hekima itumike hasa unapotoa huduma kwenye makanisa machanga ambayo pengine wewe ndiye unahitajika kufanyika baraka kwao badala ya wao kutoa kwa ajili yako.

Pia, kuna huduma zingine ambazo hufanyika kwa muda mfupi tu kiasi kwamba hazichukui muda wa mtu kujitafutia kipato chake. Kwamba unaweza kufanya huduma ya Kristo bila kudai malipo kisha ukaendelea na kazi zako zinazokuingizia kipato. Hekima ya kweli na ujuzi wa Kiroho vinahitajika ili sadaka itumiwe na kugawanywa kwa utukufu wa Mungu**.**

***Wapo watu ambao huduma yao haiwalazimishi kuwepo katika huduma kila siku, wanakuwepo siku chache tu. Hawa haitakuwa rahisi kutegemea walishwe na madhabahu, lazima***

***wafanye kazi wagawanye muda wa kazi na huduma.*** Hivyo waimbaji na watoa huduma mbalimbali kanisani siyo lazima wahitaji kulipwa ili kutumika kwa kazi ya Mungu, ila kulingana na upatikanaji wa sadaka ya kusanyiko la mahali husika ulivyo. Waimbaji wanaweza kusaidiwa kulipiwa gharama za kunakili nyimbo zao, kulipiwa gharama za usafiri, chakula n.k hasa pale wanapokwenda kutoa huduma sehemu ya mbali.

***Endapo matoleo ya kusanyiko la mahali pamoja hayajitoshelezi, watoa huduma mbalimbali wanatakiwa kujua kwamba msingi mkuu wa huduma yao ni kutoa bure bila malipo na kwamba huduma ya kiroho huwa haiuzwi* (*Mathayo 10:8, 2Thesalonike 3:7-9*).** Mbali na sadaka hasa pale ambapo sadaka haitoshelezi, njia nyingine ya kusaidia kufanikisha huduma mbalimbali ni pamoja na kuitisha sadaka maalumu ya changizo inayolenga kuwatia moyo watoa huduma **(*Wafilipi 4:14-16; 3Yohana 1:6-8*)**.

2. **Wahitaji (**yatima, wajane, maskini, waliopungukiwa**)** (**2Korintho 9:9**)

Mbali na zaka na sadaka kutumika kwa ajili ya watoa huduma kanisani, vilevile Mungu alielekeza matoleo kugawanywa kwa wenye mahitaji mbalimbali kama vile yatima, wajane, maskini, wageni n.k ***(Kumbukumbu la Torati 14:28-29; 26:12-15).***Watu wa Mungu hawatakiwi kutoa michango yao katika matukio maalumu tu. Ila wanatakiwa kuwasaidia wenye uhitaji siku zote.

Toka enzi za agano la kale, kuwasaidia maskini ilikuwa ni njia ya kumtolea Mungu na ***ilitakiwa kufanyika bila kukoma wala kuhesabu imefanyika mara ngapi* (*Kumbukumbu la Torati 15:10-11; Mithali 14:31; 19:17*).** Hadi wakati huu kusaidia maskini ni sehemu ya ibada ya kweli na inayompendeza Mungu, hivyo inatakiwa kufanyika bila kukoma wala kuhesabu imefanyika mara ngapi **(*Matendo 10:1-2; Yakobo 1:27*).** Yaani tendo la kutoa kwa wahitaji linatakiwa kuwa endelevu kama

zilivyo ibada nyingine. ***Kanisa la mahali pamoja ama mtu binafsi ni vizuri katika bajeti zao waweke na sehemu ya fungu la kusaidia wahitaji*.**

*Kanisa la mahali pamoja (kusanyiko la mahali pamoja) linaposhindwa kuwa na kawaida ya kutoa kwa wahitaji linakuwa sawa kabisa na mtu ambaye hatoi sadaka na tunafahamu madhara ya mtu asiyetoa sadaka. Madhara ya kusanyiko la mahali pamoja kutokuwa na kawaida ya kutoa sadaka pengine ni makubwa kuliko mtu binafsi asiyetoa sadaka, kwa sababu madhara yake huanzia kwenye kusanyiko lenyewe mpaka kwa mshirika mmoja mmoja***.** Ipo hukumu ya milele kwa kutowasaidia wahitaji ***(Mathayo 25:31-46).***

3. **Ujenzi wa Hekalu la Bwana (*2Nyakati 31:10-12)***

Ni muhimu tujue kwamba, matoleo ni hitaji la madhabahuni kwa sababu kila kitu kanisani kama vile vyombo, umeme, viti n.k vinahitaji pesa. Ili kukidhi mahitaji yote haya, watu wa Mungu inawapasa kuzingatia kumtolea Mungu zaka na sadaka kamili. Kutokana na ufinyu wa sadaka zinazokusanywa siku za ibada, baadhi ya makusanyiko huitisha michango kwa washirika wake ili kusaidia kulipa gharama za umeme, maji, ukarabati wa vyombo, majengo n.k. Yote haya yanalenga kukamilisha kazi ya Mungu.

Wapo washirika ambao pengine kwa kutofahamu vizuri matumizi ya mapato ya kusanyiko huwa wanalalamika kwamba wanatoa zaka na sadaka lakini bado wanachangishwa michango mingine.

Hivyo basi, ni vyema viongozi wa kusanyiko la mahali pamoja kutoa ufafanuzi wa mapato na matumizi yao ili kuondoa hisia potofu zisizo za lazima ambazo mwisho wake huwa zinampa shetani nafasi ya kuvuruga kazi ya Mungu**.**

## *Sura Ya Tano*

# MSUKUMO WA KUTOA SADAKA

Siku za ibada waumini huchukua vitu vya aina mbalimbali vyenye thamani tofautitofauti kupeleka kanisani kwa lengo la kutoa sadaka. Hata hivyo, inaonekana kuwa dhamira inayowasukuma kuchukua sadaka hizo hutofautiana kutoka mtu mmoja hadi mwingine. Tofauti za dhamira zao zinaweza kuwa sahihi au siyo sahihi kutokana na sababu mbalimbali na hasa kutofautiana katika uelewa sahihi juu ya sababu za kutoa sadaka.

Baadhi ya sababu mbalimbali inayosababisha watu wengi makanisani kutoa sadaka ni kama ifuatayo:

a) Kwa sababu ni kawaida ya watu kwenda kanisani wakiwa na sadaka (**mazoea au utamaduni wa kutoa sadaka**). Hivyo utoaji wa watu wa jinsi hii huwa ni wa mazoea kwamba ni lazima kwenda kanisani ukiwa na sadaka. Ni kweli kwamba tunazuiwa kwenda kanisani tukiwa mikono mitupu lakini madhara ya kutoa sadaka kama mazoea ni kumfanya mtu kutoa chochote atakachokutana nacho siku ya ibada. Hivyo, hata kama akitoa mara nyingi anaweza asione matokeo yoyote ya kutoa kwake.

b) Kwa sababu Mchungaji wa kanisa anasisitiza sana juu ya matoleo kwa hiyo lazima nitoe ili asinielewe vibaya. Hivyo basi, mtu huyu anatoa sadaka ili kuwafurahisha viongozi wa kanisa.

c) Kwa sababu watu wengine wakisimama atabaki peke yake akiwa amekaa. Kwa hiyo, mtu anatoa sadaka kwa kufikiria watu wengine watamfikiriaje asipotoa. Anaogopa watu wasiseme pengine yeye ameishiwa au kuchukuliwa kwa hali ya umaskini pamoja na sababu kadha wa kadha ambazo mtu atazifikiria mbali na kufikiria upendo wa Mungu kwake (***Mathayo 6:1-4)***.
d) Kwa sababu mchungaji amepungukiwa mahitaji muhimu hivyo, anaona asipotoa familia ya mchungaji haitapata mahitaji hayo. Kwa hiyo, mtu huyu anatoa ili kumsaidia mchungaji. Ni kweli mara nyingine huwa tunatoa sadaka mahsusi kwa ajili ya mchungaji lakini haitakiwi tufikirie kwamba tusipotoa mchungaji atakufa na njaa kwani mtoaji mkuu kwetu sote ni Mungu ***(Mathayo 6:1-4)*** *na kwamba Mungu anaweza kumlisha mchungaji bila sadaka yako.*
e) Wengine wanatoa ili Mungu awabariki maishani mwao, yaani kutoa ili upate baraka kwa sababu pengine mambo yako hayaendi vizuri. Kwa sababu hii, sadaka inachukuliwa kama biashara na Mungu ya kutoa ili nawe upokee. Mara nyingi watu wengi walioenda mbele za Mungu na nia hii huishia kuvunjika moyo kwa sababu hawaendi na moyo wa kumjua na kumpenda Mungu, bali wanajiunganisha naye kwa sababu ya maslahi yao binafsi yasiyo na uelewa juu ya Mungu ndiyo maana mwisho wao unaweza usiwe mzuri.
f) Wengine wanatoa kwa sababu wameshuhudia watu ambao huwa wanatoa sadaka Mungu amewabariki sana katika maisha yao. Kwa hiyo, na yeye anatoa ili afanikiwe kama wengine walivyofanikiwa. Yaani pengine uliwahi kusikia mtu anatoa ushuhuda jinsi ambavyo Mungu amembariki kupitia utoaji, hivyo na wewe ukaanza kutoa kwa sababu hiyo tu. Kuiga jambo jema siyo vibaya lakini ni vizuri ufanye jambo kwa ufahamu mzuri. Siyo vyema kutoa kwa kuiga japo waliofanikiwa katika utoaji wanaweza kufanyika ushuhuda kwetu ili tukue katika viwango vya utoaji.

Hizo ni baadhi ya sababu na pengine na wewe una sababu zako zinazosababisha utoe sadaka. Baadhi ya sababu zipo sawa lakini ukiangalia kwa umakini unaona hakuna sababu pengine hata moja ambayo inahusiana na upendo wa moja kwa moja kwa Mungu, sababu nyingi zinaonekana kuwa ni za malengo binafsi tu.

**Kwa nini Tunatoa Sadaka?**

Ibada kamili hukamilishwa na sadaka, tunatoa sadaka kwa Mungu kama sehemu ya ibada yenye thamani mbele zake:

- Tunatoa ili tuoneshe upendo tulionao kwa Mungu.
- Tunatoa ili tuoneshe uhusiano wetu katika kumuabudu Mungu (**bila kuhesabu yale ambayo Mungu ametutendea, *Efeso 3:17-20***).
- Tunatoa ili kuonesha ushirika wetu na Mungu.

Ni kweli kuwa, ziko baraka tunapotoa sadaka, lakini jambo la muhimu ni wewe kuithaminisha sadaka yako iwe ibada kamili mbele za Mungu.

***Ili kuonesha kwamba sadaka yetu ni ishara ya kumpenda Mungu na wala siyo unafiki, Bwana Yesu alituagiza tutoe sadaka wakati Mioyo yetu ikiwa safi mbele za Mungu. Alisema, kama ukiwa unataka kutoa sadaka huku ukikumbuka kuwa huna mahusiano mazuri na ndugu yako ni heri usitoe sadaka****, kwanza ukapatane na ndugu yako ndipo uje kutoa sadaka* (***Mathayo 5:23-24*)**. Hii inamaanisha kuwa kutoa sadaka ni jambo la upendo wa juu sana mbele za Mungu, hivyo halitakiwi kufanyika ***kinafiki au kutizima agizo tu***.

Hebu fikiria, mume na mke wamegombana nyumbani, wala hawajaombana msamaha au mtoto hana heshima mbele za walezi wake (**wazazi, walimu, majirani n.k**) kisha wanaenda kanisani na wanatoa sadaka na zaka kwa mbwembwe kabisa. Je, kuna

upendo ndani ya mioyo ya watu kama hao? Bila shaka wanahitaji kutengeneza mambo yao kabla ya kutoa sadaka.

Tunapotoa sadaka ni muhimu sana kuelewa uhusiano wetu na Mungu yapoje. Kama mahusiano yetu na Mungu siyo mazuri lakini tunataka Mungu atujibu mahitaji yetu kwa kutoa sadaka tunapoteza hizo fedha ni bora tungalizitumia kwa matumizi binafsi **(1Samweli 15:22).** ***Jambo la muhimu kujua ni kwamba hata kama tukitoa sadaka ya namna gani haiwezi ikatufanya tufutiwe dhambi zetu (Isa 1:11-13; Amo 5:21-22; Mik 6:6-8).***

Wapo watu wanaolalamika kwamba, Mungu hajibu maombi yao, wamefunga pamoja na kuomba sana, wametoa sana sadaka kwa ajili ya jambo fulani lakini Mungu amekaa kimya**.** Inawezekana wakati wa Mungu kukujibu haujafika au hujibiwi kwa sababu haujatoa sawasawa na neno la Mungu, *yaani umetoa sadaka kama madai ya majibu ya matatizo yako***.**

**Maandiko matakatifu yanaonesha hali mbalimbali ambazo zinasababisha tumtolee Mungu sadaka:**

Kama ilivyoelezwa kwenye historia ya sadaka, utoaji ulianza kwa hiyari (tuliona kwa Habiri na Kaini) lakini baadaye jambo hili lilikuwa ni lazima wakati wa Torati ya Musa. ***Japokuwa suala la sadaka lilikuwa la lazima wakati wa Torati lakini lilitoa mwangaza wa kutuonesha Mungu anataka tumfanyie nini kupitia matoleo***. Kwa hiyo, itoshe kusema kuwa ni mapenzi ya Mungu tumtolee sadaka, Mungu anataka aone upendo wetu kwake kupitia mali zatu. Ndiyo maana anasema, ukimtolea sadaka iliyo nzuri unakuwa umemjaribu naye atakujibu kwa kukujaza kila kitu unachohitaji hata ukose mahali pa kuweka. ***Wakati huu wa Agano Jipya, sadaka inatolewa kwa hiyari na kwa upendo.***

Zifuatazo ni baadhi tu ya sababu kwa nini tunatoa sadaka:

1. **Ni Agizo la Mungu ambalo Linatekelezwa kwa Upendo (*Kumbukumbu la Torati 16:16-17*)**

**"***Katika sikukuu ya mikate isiyotiwa chachu na katika sikukuu ya majuma, na katika sikukuu ya vibanda; wala wasitokee mbele za Bwana mikono mitupu*" ***Kumbukumbu la torati 16:16b.*** Huu ni mfano wa agizo la Mungu la utoaji wa matoleo ya hiyari kwa kila mteule wa Mungu. Ambalo linatakiwa kutimizwa kwa upendo. Mungu anaagiza tusitoke mikono mitupu bali twende na vitu vya thamani sawasawa na alivyotubariki.

2. **Kama Ishara ya Kumpenda na Kumheshimu Mungu (*Mithali 3:9-10*)**

Heshima inaambatana na utii, Mungu ameamuru tumtolee zaka na sadaka kamili hekaluni mwake. Hivyo, tunapokuwa waaminifu kwenye matoleo, Mungu anaiona heshima yetu kwake kupitia kujitoa kwetu kwake kwa njia ya mali zetu. Pia, tunakuwa tunakamilisha heshima sahihi kwa Mungu bali tukitoa bila upendo mioyoni mwetu, tutakuwa tunatimiza wajibu tu. Hivyo basi, kama tunampenda Mungu na kumheshimu basi, hakika utoaji wa zaka na sadaka hautakuwa mzigo kwetu.

3. **Hitaji la Madhabahuni (*Malaki 3:8-11; 2Nyakati 31:10-12*)**

Muhimu kujua kwamba, matoleo ni hitaji la madhabahuni kwa sababu kila kitu kanisani kinahitaji pesa. Vyombo vya muziki, umeme, viti na kila kitu kinahitaji pesa. Wachungaji nao Mungu amewapa fungu lao kutokea madhabahuni kwa sababu ni agizo la Mungu kabisa (***2Nyakati 31:10; Luka 10:7-8***). Hivyo, tutambue kuwa mambo mengi kanisani yanahitaji tutoe sadaka nzuri ili huduma ya Mungu itendelee vizuri.

4. **Vyote ni Mali ya Mungu (*Zaburi 24:1*)**

Mwanadamu lazima ajue kwamba vitu vyote ni mali ya Mungu, hivyo hatuwezi kumzuilia Mungu kitu chochote. Mungu ametupatia mali ili tuwe mawakili wema wa mali zake, tuzitumie kwa upendo na kwa uaminifu. Mungu ana uwezo wa kuziondoa, kuziongeza au kuzifuta kabisa. Hitaji la matoleo lisiwe sababu ya kutoa sadaka kama kumlipa Mungu fadhila za kutupatia utajiri bali tumtolee sadaka kwa upendo (kama shukrani) wa jinsi alivyo mwema maishani mwetu.

**Baadhi ya Faida Zinazoambatana na Utoaji wa Sadaka**

1 **Hutengeneza Hazina zetu Mbinguni (*Luka 12:31-34)***

Matoleo yana faida nyingi sana kwa mtoaji, moja ya faida hizi ni kutengeneza hazina yako mbinguni ambapo hakuna wezi watakaoiharibu. Kazi ya hazina ni kukufaa wakati wa shida. Hivyo kwa kuweka hazina yako mbinguni humfanya Mungu kukufaa wakati wa shida.

*2* **Kutoa ni Chanzo cha Thawabu au Baraka za Mungu (*Malaki 3:8-11; Mwanzo 8;21-22, 22:12-18, 27:4; Luka 6:38)***

Matoleo ni chanzo kikuu cha baraka, unavyomtolea Mungu kwa usahihi na uaminifu hakika atakubariki sana kwa baraka zote za rohoni na za mwilini. Baraka za kiuchumi, kutamalaki, ndoa, uzao, afya n.k. Zote zitaambatana na wewe.

3 **Tunapata Ulinzi wa Mungu katika Maisha yetu (*Malaki 3:10-12)***

Kuna watu shetani huwapangia magonjwa mara kwa mara lakini hawaumwi kwa sababu Mungu anamkemea mharibifu wa afya zao kwa sababu tu ya utoaji wa sadaka kwa uaminifu. Mungu anataka tumjaribu kwa matoleo na ameahidi kufungua madirisha ya mbinguni.

Madirisha ya mbinguni yakifunguka kwako kwa sababu ya utoaji wako sahihi na wa kudumu hakika huko mbinguni zitatoka baraka nyingi na upendeleo katika kazi, uchumba, ndoa na chochote utakachokigusa.

Mungu anaposema atakubariki kwa sababu ya uaminifu wako siyo kwamba atakubariki pesa tu. Bali ni mambo mengi ya kukubariki. Mungu anaposema kwamba atamkemea yeye alaye ujue hakika ataondoa magonjwa, misiba, kuibiwa pamoja na mabalaa mbalimbali yanayoweza kusababisha pesa yako kutotumika kwenye mipango yako.

### *4* Utoaji unaweza kufufua baraka zako zilizokuwa zimekufa *(Matendo 9:36-41)*

Tujifunze kwa Dorkasi ambaye maisha yake yalikuwa yamejaa utoaji, yaani utoaji ulikuwa ni sehemu ya maisha yake na ndiyo ikawa sababu kufufuliwa kwake. Wajane walisimama na kuonesha mavazi ambayo walikuwa wanavalishwa na Dorkasi, walitoa machozi yao mbele za Mungu wakati ambapo Dorkasi alikuwa hawezi kujiombea na hatimaye Dorkasi akafufuliwa. Yapo mambo yetu mengi sana ambayo shetani anapambana kuyaua lakini sadaka zetu na nia yetu safi mbele za Mungu (Utakatifu) husimama na kututetea.

### 5 Kufungua Milango ya Majibu ya Maombi Yako

Katika ***2Wafalme 4:8-17,*** tunasoma utoaji wa Mwanamke wa huko Shunemu ambaye anatimiza wajibu wake kama mama anayemjua Mungu. Alichukua jukumu la kumtunza mtumishi wa Mungu Elisha. Huyu mwanamke hakuwa na mtoto, bila shaka alikuwa ameomba miaka mingi bila majibu lakini utoaji wake ukawa sababu ya maombi yake kujibiwa. Mungu hakubaki kimya katika kujitoa kwake na hivyo, ikawa sababu ya kufungua milango ya kupata mtoto**.**

***Mara nyingi huwa tunaomba tukitegemea majibu kupitia maombi yetu tu, lakini kuna wakati utoaji wetu unakuwa ni mlango wa majibu ya maombi yetu***. Katika ***Mathayo 10:42,*** tunasoma kuwa Yesu Kristo anatoa ahadi kwa yoyote atakayejitoa kwa ajili ya watumishi wa Mungu kwamba hatakosa thawabu yake**.** Hivyo, ndivyo ilivyotokea kwa huyo mama wa Shunemu baada ya kujitoa kwa ajili ya mtumishi wa Mungu**.**

***Haina maana kwamba, tutoe sadaka ili tujibiwe maombi yetu la hasha!! hilo lisiwe kusudi letu katika matoleo, bali maisha ya utoaji kwa upendo yanafungua milango ya majibu ya maombi yetu***. Huyu mama wa Shunemu hakutoa ili Mungu ajibu maombi yake ya kupata mtoto ila yeye alijitoa kwa moyo wa upendo kisha Mungu akakumbuka haja ya moyo wake.

> **Ushuhuda**: *Yupo mtu mmoja ambaye alifanikiwa kujenga nyumba kadhaa kwa ajili ya kuzipangisha, nyumba zilipokamilika zilikaa kwa kipindi cha zaidi ya miezi mitatu (3) bila wapangaji. Baadaye Mungu alimpa mzigo wa kufanya jambo fulani kanisani kwao anapoabudu. Alipotafakari aliona kama vile ile kazi ingemgharimu pesa nyingi, hivyo, akaamua kushirikisha baadhi ya watu pale kanisani ili wasaidiane katika gharama. Kila mtu alitoa sababu yake ya kutokuwa na pesa na wengine wakasema labda hilo jambo lifanyike miezi kadhaa ijayo.*
>
> *Yule mtu akaendelea kupata msukumo wa kufanya ile kazi hivyo, akaamua kutafuta pesa na kuanza kufanya ile kazi yeye mwenyewe. Siku kazi ilipokamilika anasema, wapangaji wa zile nyumba walipatikana siku hiyohiyo, anaendelea kusema kuwa, waliendelea kuja watu wengi wakihitaji kulipia ili waishi pale. Jambo lililomshangaza ni kwamba zile nyumba zilikuwa zimekaa muda mrefu sana bila wapangaji, iweje baada ya kufanya ile kazi kanisani watu waje kwa wingi kiasi kile?*

Yapo majibu ya maombi yako ambayo yanakuhitaji kusikia na kutii sauti ya Mungu kwa njia ya kutoa sadaka sawa sawa na mama mshunemu. Hata ushuhuda wa huyu ndugu hauoneshi kabisa kuwa alitoa ili apate wapangaji katika nyumba yake wala wakati anatoa wazo la kwamba kuna nyumba yake imekaa muda mrefu haijapata mpangaji halikuwepo kwake wakati huo. Bali yeye kilichokuwa mbele yake na kwenye mawazo ya moyo wake ni kufanya kile kilichowekwa na Mungu ndani yake. Ndugu huyu, alichofanya ni kutii sauti ya Mungu na pale alipotii basi, Mungu akakumbuka haja ya moyo wake.

## 6 Kukustahilisha Mambo yasiyo ya Kawaida

Tunaona habari za akida mmoja katika ***Luka 7:4-5*** ambaye mtumwa wake alikuwa anaumwa kiasi cha kufa. Akida yeye mwenyewe hakumwendea Yesu kumwelezea kwa nini alistahili kutendewa jambo lile. Bali watumishi wa yule akida walipomwendea Yesu walitumia sababu ya wema na utoaji wa yule akida kusisitizia ombi la yule akida kujibiwa na Yesu.

Tunaona kuwa sadaka yake yenyewe ilinena mbele za Yesu na hivyo kumstahilisha jambo ambalo hata yeye mwenyewe aliona kuwa alikuwa hastahili. Hii inatuonesha kuwa yapo mambo ambayo tunatendewa siyo kwa sababu sisi ni waombaji sana bali sadaka zetu zinasimama zenyewe mbele za Bwana kutuombea.

## 7 Sadaka yako Inakuwekea Ukumbusho mbele za Mungu

*Katika* ***Matendo 10:30-31,*** biblia inatuonesha namna ambavyo sadaka ya Kornelio ilivyosababisha kuwa ukumbusho mbele za Mungu. Kuweka kumbukumbu mbele za Mungu siyo jambo dogo, Mungu alimkumbuka

Kornelio akamtuma Malaika kumwelekeza Kornelio yampasayo kufanya ili apate wokovu kamili.

Naamini kuwa kila mtu angetamani kuona anakumbukwa na Mungu kwenye maisha yake ndiyo maana tukiwa kwenye maombi yetu binafsi huwa tunamwomba Mungu atukumbuke katika changamoto mbalimbali tunazopitia. ***Kumbe ipo njia rahisi tu ya kumfanya Mungu atukumbuke, nayo ni kuwa mwaminifu kwa kutoa sadaka kamili***. Ndiyo maana, ni vizuri kila mara uwe unajihoji mwenyewe je, mbele za Mungu kuna kitu (yamkini ni Sadaka zako, matendo yako mema, huduma yako au hata maombi) ambacho kinakunenea mbele za Mungu kwa ajili yako? Na Je kinanena nini kuhusu wewe?

Wakati Bwana anamtokea Kornelio anamwambia sala zako na sadaka zako zimefika juu na kuwa ukumbusho mbele za Mungu. Maana yake hizi sadaka na sala zilikuwa zinanena kitu mbele za Mungu juu ya Kornelio ndiyo maana ya ukumbusho yaani kumkumbusha kitu Mungu kuhusu Kornelio. Pia, tunaona kwa Dorkas kuhusu sadaka na matendo yake mema yalivyonena wakati wa kifo chake.

### 6. Kutengeneza Agano na Mungu

Ukitengeneza agano na Mungu ujue kuwa agano hilo litavunja maagano yote ya kipepo yaliyokufunga. Watu wengi wamefungwa na maagano ya mapepo ya ukoo amabayo yanafuata vizazi vyao. Na hivyo, kuharibu uchumi wa familia. Mungu anapofungua baraka zako kwa njia ya uaminifu wako katika sadaka, ni hakika kuwa na maagano ya kipepo hufungwa maana Mungu hukuzidisha na kukustawisha kwa kila namna, ikiwemo katika uchumi wako.

Baada ya Nuhu kumtolea Bwana sadaka ya shukrani, tunaona Mungu anaweka agano jipya la kutoiharibu dunia kwa gharika **(*Mwanzo 8:21-22*).** Pia, tunaona Ibrahimu baada ya kutii sauti ya Mungu na kuamua kumtolea sadaka ya kuteketeza ya mwanae Isaka, Mungu aliweka agano la kumbariki Ibrahimu pamoja na vizazi vyake vyote **(Mwanzo 22:15-18).**

## *Sura Ya Sita*

## KANUNI ZA UTOAJI SADAKA

### Kwa Nini Tunatoa Lakini Hatupokei?

Kuna nyakati tunapanda lakini hatuvuni na tunatoa lakini hatupokei; katika hali kama hiyo, wakati mwingine kunakuwa na maswali amabayo yanahitaji majibu. Kanuni ya Mungu ni kupokea baada ya kutoa (kupanda na kuvuna). Ni nini husababisha tupande bila kupokea mavuno?

Bila shaka hatuwezi kumlaumu Mungu kwamba amekatalia Baraka zetu kwa maana neno la Mungu linasema "***Mungu, si mwanadamu hata aseme uongo" Hesabu 23:19.*** Mungu ameahidi Baraka kupitia matoleo, kwa hiyo, ni sisi wapandaji au watoaji ndiyo tunaokosea masharti ya kupanda au kutoa. Mungu anasema katika ***Yakobo 4:3 "Hata mwaomba, wala hampati, kwasababu mwaomba vibaya".*** Basi ni lazima na kwa hakika, "tunatoa lakini hatupokei, ni kwa sababu tunatoa vibaya".

Yafuatayo ni baadhi tu ya mambo yanayosababisha tusipokee japo tunamtolea Mungu sadaka, hata hivyo zinaweza kuwepo sababu Zaidi ya hizi:

a) **Kutenda dhambi** (***Isaya 59:1-2, 11-20; Mith 21:27*****).** Kumpendeza Mungu kunaanzia na matendo yetu. Dhambi humtenga mwanadamu na Mungu. Katika ***Isaya 59:1-2*** tunaona kuwa siyo kwamba Mungu hasikii maombi yetu bali dhambi zetu zinatuweka mbali naye. Vivyo hivyo,

hata sadaka zetu hazitakuwa na matunda kama tunazitoa katika mazingira ya dhambi. Katika ***Mithali 21:27*** neno la Mungu linasema sadaka ya wasio haki inaleta chukizo mbele za Mungu. Katika **1Samweli 15:22,** Samweli anamwambia Mfalme Sauli kuwa Mungu anathamini sana utii wa sauti yake kuliko hata hiyo sadaka aliyokuwa ameitoa mbele za Bwana. Hivyo kama mtu atatoa sadaka bila kujali matendo yake kwa Mungu, sadaka hiyo inaweza isiwe na maana mbele za Mungu.

Hivyo, sadaka zetu ili zimpendeze Mungu lazima zitoke katika mioyo iliyo safi mbele za Mungu. Angalia mifano ya utoaji wa Kornelio **(Matendo 10:2)** na Dorkasi **(Matendo 9:36)** ambapo tunaona kuwa Mungu alipendezwa na matendo yao na pia utoaji wao.

Hapo mwanzo nimedokeza kwamba, sadaka zetu kwa Mungu ni ishara ya upendo tulionao kwake. Maandiko matakatifu yanaeleza kuwa ukimpenda Mungu utazishika amri zake **(Yohana 14:15, 21; 15:10).** Miongoni mwa amri za Mungu ni pamoja na utakatifu, kwa hiyo, upendo wetu kwa Mungu lazima uambatane na utakatifu.

b) **Kumwibia Mungu Zaka na Sadaka (*Malaki 3:7-12; 2Korintho 9:6-13)***

Kutoa zaka na sadaka zilizo pungufu mbele za Mungu zinaleta chukizo mbele za Bwana, hii itasababisha madirisha ya mbinguni kufungwa. Sadaka yako italeta mavuno mazuri endapo tu madirisha yako ya mbinguni yamefunguliwa kwa zaka kamili unayotoa. Nabii Malaki analiambia taifa la Israel kuwa zaka na sadaka zao walizokuwa wanapeleka mbele za Mungu hazikuwa kamili kulingana na Baraka ambazo Mungu alikuwa amewabariki. Ilifika wakati ambapo watu walikuwa wanatoa vitu dhaifu madhabahuni bila kuogopa.

Hali hii inaendelea mpaka kwenye kanisa la leo ambapo watu wanaweza kutoa chochote tu bila kujali. Upungufu katika utoaji wa fungu la kumi unasababishwa na: ***mtoaji kudhamiria kwa makusudi kupunguza kiasi kinachostahili kutolewa, kutoweka vizuri mahesabu au kumbukumbu za kipato chake na hivyo, kusababisha atoe zaka ya kukisia tu wakati upo uwezekano wa kujua kiwango sahihi cha fungu la kumi.***

Udhaifu wa sadaka ya upendo tunayotoa kila tuendapo kwenye ibada unaweza kusababishwa na sababu kadha wa kadha zikiwemo: ***kutoa kidogo sana ukilinganisha na baraka ambazo Mungu amekubariki au kupunguza sadaka ambayo tayari umedhamiria kuipeleka kanisani*** (***Matendo 5:1-5***). Punguzo hili hutokea labda kwa sababu ya kununua vitu njiani kama vile: pipi, vocha n.k kutoka kwenye pesa ambazo tayari umeshazitenga kwa ajili ya sadaka au kuona kuwa kiasi ulichotenga kwa ajili ya sadaka ni kikubwa sana hivyo unaamua kupunguza.

Ni vizuri utambue kuwa Mungu hutambua dhamira yako ya kutoa sadaka hata kabla hujaitoa, hivyo kanisani huwa tunaenda tu kukamilisha kile ambacho tayari Mungu anakijua kutoka mioyoni mwetu. Kwa muktadha huo ukipunguza sadaka unakuwa unamwibia Mungu. Japokuwa haina tatizo kama mtu akijitambua kuwa sadaka aliyopanga kumtolea Mungu ni ndogo na hivyo akaamua kuongeza kiasi cha sadaka wakati wa matoleo.

c) **Kutoa Sadaka bila Imani** (***Waebrania 10:38, 11:1, 6***)

“Imani ni kuwa na uhakika wa mambo yatarajiwayo” wengi hutoa sadaka lakini hawana uhakika kuwa ile sadaka itazaa mara 30 au mara 60 au mara 100 (***Mathayo 13:3, 8***).

- Kwa sababu wengi hutoa bila uhakika (imani) sadaka zao haziwi za kupendeza mbele za Mungu hivyo hazizai. Kwa sababu hiyo wanajikuta wanaamini kwamba wakitoa sadaka ni kama wamechanga pesa tu na wala haitazamiwi kuzaa, yaani ni kama imepotea. Hayo ni mawazo potofu ambayo shetani amewafanya wengi kufikiria hivyo.

- Lakini neno la Mungu linatupa uhakika (imani) kwa kuwa "***imani huja kwa kusikia … Neno la Kristo (Rumi 10:17).*** Mtu akiliamini neno la Mungu ya kwamba Mungu hawezi kusema uongo, moyo wake utapokea uhakika (imani). Ndani yake litajengeka tarajio la kupokea kila anapotoa wala hataona anapoteza mali zake atoapo sadaka, atajua kuwa kutoa sadaka si kupoteza bali ni kupanda kwa ajili ya mavuno (baraka) makubwa zaidi. Kuanzia sasa pokea uhakika kwamba ukitoa kwa imani ya kupokea utapokea. Ukitoa bila imani ya kupokea hautapokea bali utakuwa umechangia tu. Hiyo mbegu haiwezi kuzaa kwa maana "….kila tendo lisilotoka katika imani ni dhambi" (***Rumi 14:23*)**

- Hakuna mkulima anayeweza kutoa kidogo wakati anaamini mavuno ni mengi. Atoae kidogo hana imani ya kupokea kwa sababu moyoni mwake anaamini inapotea ndiyo maana anaona ni bora apoteze kidogo. Lakini mwenye imani ya kupokea hutoa kwa wingi kwa sababu anajua sadaka yake haipotei bali imepandwa na itazaa na kuongezeka.

- Ukipanga moyoni mwako kutoka nyumbani kumpa Mungu kiasi fulani cha sadaka, baada ya azma hiyo Mungu anakuwa ameipokea sadaka tayari, hivyo wakati wa utoaji usiipunguze kwani kwa kuipunguza utakuwa unamwibia Mungu (***Matendo 5:1-11; Mithali 21:27)***. Watu wengi hukosea kwa kufika ibadani wakiwa

wamepunguza sadaka ambayo mioyo yao ilishamkabidhi Mungu. Katika sadaka hiyo hiyo watanunua gazeti, pipi, au kulipa nauli. Kwa kufanya hivyo, hiyo sadaka inakuwa siyo kamili tena mbele za Mungu.

- Panga kutoa sadaka kwa maombi kabisa na uamue kiasi utakachomtolea Mungu kisha uwe mwaminifu kutokuipunguza hata iweje. Baadhi ya mikosi itupatayo ni matokeo ya kumwibia Mungu kama Anania na Safira walivyofanya. Habili alitoa sadaka yake kwa Imani na unyenyekevu na Mungu akaibariki.Usitoe sadaka wakati Imani yako imetindika mbele za Mungu **(*Mwazo 4:2-5, Waebrania11:4, 1Yohana 3:12*).**

d) **Kutoa Sadaka Kilema (*Malaki 1:13- 14; Walawi 22:20-22)***

Sadaka kilema ni ile ambayo hata wewe hauihitaji. Ni zile sadaka zitolewazo ili kupunguza mizigo au ili tuonekane tumeshiriki katika kutoa. Mungu hatabariki sadaka "*reject*" zilizokataliwa na wewe binafsi.Usitoe mabaki ya dukani, shambani, mfukoni n.k kuwa sadaka takatifu, utapata laana.

Mungu anapenda sadaka bora katika vitu akupavyo, sadaka nzuri inayotolewa kwa maandalizi. ***Haipendezi kwa watu unayemjua Mungu siku ya ibada ndipo uangalie kwenye pochi au mfukoni kuona kilichosalia kisha ndicho upeleke kama sadaka***. Sadaka inabidi iwe sehemu ya bajeti yako na pia iwe miongoni mwa fungu zuri.

Fikiria mtu anapopanga kupeleka zawadi kwa mtu anayempenda (mzazi, mwenza n.k) lazima ataandaa kitu cha thamani tena kwa upendo bila kulazimishwa ili amfurahishe mpendwa wake. Kwa Mungu inatubidi kufanya zaidi ya hapo. Matoleo yote ya sadaka yanapaswa kufanywa kwa moyo

mkunjufu mbele za uso wa Mungu katika ibada. "***Mheshimu Mungu kwa matoleo yako***" ***Mithali 3:9, kwa hiyo kutoa sadaka nzuri ni heshima mbele za Mungu***. Kumbuka kuwa Mungu ndiye anayekupa nguvu za kupata vyote ulivyonavyo hivyo inakubidi umkumbuke yeye kwanza kabla ya kitu chochote.

e) **Kutoa Sadaka Dhalimu au Haramu (*Malaki 1:13-14*)**
Sadaka haramu ni ile iliyopatikana kwa udhalimu, kwa mfano; biashara haramu (ukahaba, madawa ya kulevya n.k), dhuluma, rushwa, wizi, uuaji, utapeli n.k. Wewe ufanyaye mambo ya jinsi hii ni chukizo mbele za Mungu. Sadaka itokanayo na mapato ya jinsi hii haitabarikiwa ni haramu mbele za BWANA. Hivyo usifanye uovu kisha ukatumia hiyo pesa kutoa sadaka ukitaka iwe sehemu ya toba ya kukufutia makosa yako.

*f)* **Kutoa Sadaka bila Upendo wa Kristo Ndani Yako (*1Korintho 13:1-4*)**
Kama moyo wako unamchukia mtu, jirani, ndugu n.k, hufai kutoa sadaka. Maandiko matakatifu yanafundisha kuwa kama umekorofishana na mtu yakupasa kutengeneza uhusiano wenu kwanza kabla ya kutoa sadaka (***Mathayo 5:23-25*).** Hii ni kwa sababu utoaji ni ibada kamili. Unatakiwa utoe sadaka bila hila, kinyongo, chuki, hasira wala ugomvi au kwazo juu ya mtu, moyo wako uwe safi mbele za Mungu.

Kama una neno juu ya mtu maandiko matakatifu yanasema "***Ungamaneni dhambi zenu ninyi kwa ninyi mpate kuponywa." (Yakobo 5:16).*** Kama vile maandiko matakatifu yasemanvyo huwezi kumpenda Mungu usiyemwona huku ukimchukia jirani yako unayemwona, sadaka ni ishara ya kuonesha upendo wetu kwa Mungu hivyo huwezi kumpenda Mungu wakati ukiwa unamchukia jirani yako. Kwa sababu sadaka ni ishara ya upendo wetu kwa Mungu, hivyo hatuwezi kutoa katika hali ya unafiki.

**g) Kutoa Sadaka ili Uonekane Machoni pa Watu**

Utoaji wa baadhi ya watu huwa umelenga kupata sifa machoni pa watu. Utoaji wa jinsi hii hauleti thawabu kutoka kwa Mungu. Katika ***Mathayo 6:2-4,*** maana ya mandiko haya ni kwamba sio tatizo sadaka yako kuonekana kwa hali ya nje bali tatizo ni nia iliyo ndani ya moyo wa mtoaji. Haimaanishi jirani yako au mtu aliye karibu na wewe akiiona sadaka yako itakuwa batili, bali kama unaionesha au unaitaja ili usifiwe na kuonekana kwa watu hapo itakuwa batili mbele za Mungu.

Mungu hapendezwi na sadaka inayotolewa kwa njia ya kupata sifa kutoka kwa watu wakati moyo wa mtoaji upo mbali na Mungu. Katika ***Matendo 5:4* na *Luka 18:12*** tunaoneshwa dhahiri jinsi Mungu anavyochukizwa na sadaka za kutaka sifa au kuonekana mbele za watu. Anania na mkewe waliahidi kutoa sadaka yamkini ili wasifiwe na watu, baadaye hawakutoa kama walivyoahidi. Hii ilisababisha Mungu kuachilia hukumu ya mara moja juu yao **(Matendo 5:1-5).** Ndivyo hivyo Mungu anavyochukizwa hata leo pale tunapoahidi au kutoa ili tuonekane machoni pa watu lakini mioyo yetu ipo mbali na Mungu.

**H) Kutoa Sadaka bila Mwongozo wa Roho Mtakatifu (*Kumbukumbu la Torati 12:13-14*)**

Kila sadaka (mbegu) ina mahali pake maalum pa kupandwa. Ni muhimu kusikiliza mwongozo wa Roho Mtakatifu wakati wa kutoa sadaka. Kutoa ni ibada hivyo, lazima iongozwe kwa msaada wa Roho Mtakatifu. Yesu Kristo anasema atakapokuja huyo Roho Mtakatifu atawaongoza na kuwatia kwenye kweli yote (***Yohana 14:26; 16:13-14)***. Kwa hiyo, Roho Mtakatifu ndiye kiongozi wetu wa mambo yote ya rohoni ikiwa ni pamoja na matoleo. Watu wanaomtii Roho

Mtakatifu katika matoleo yao wanapata matokeo makubwa kuliko wale wanaotoa kwa akili zao tu (**kwa maelezo zaidi, rejelea kundi la kwanza la utoaji wa sadaka isiyo ya kawaida).**

Kama Mungu anataka sadaka yako uitoe kwa yatima au kwa watu wengine wenye mahitaji ipeleke hukohuko. Kama ukitoa mahali pengine utakuwa hujatii sauti ya Mungu, hivyo unaweza kupata mavuno haba. Ni muhimu umuulize Mungu, kumsikiliza na kutii vizuri sauti yake. Kama ambavyo haifai kumpenda Mungu huku ukichukia jirani yako ndivyo isivyofaa kutoa sadaka kanisani huku ukiwapita njiani watu wenye mahitaji maalumu bila kuwasaidia hasa kama Roho wa BWANA anakushuhudia kufanya hivyo.

Kutokana na ufinyu wa utajiri tulionao, bila shaka hatuwezi kuwasaidia watu wote wenye uhitaji tunaokutana nao njiani au wanaokuja nyumbani kwetu. Pia katikati ya watu wenye uhitaji, wengine siyo wahitaji sahihi, yaani wengine ni mawakala wa shetani na wengine ni matapeli tu. Hii inatukumbusha umuhimu wa kusikiliza mwongozo wa Roho Mtakatifu ili tufahamu vyema ni yupi kati ya wahitaji ambaye Mungu anataka ufanyike baraka kwake.

Bila msaada wa Roho Mtakatifu utatumia akili zako tu kuamua mahali pa kutoa sadaka yako na hatimaye unaweza usipate thawabu kwa Mungu. ***Siyo sahihi pia kwenda kanisani mikono mitupu kwa sababu ya kutoa sadaka kwa watu wenye uhitaji, pangilia sadaka yako kadri roho wa Bwana atakavyo kuongoza.*** Kuna sadaka za kutoa kwenye ibada na sadaka za sehemu nyingine nje ya ibada. Mfano, kwa yatima, wajane, masikini, mikutano ya injili, semina za neno la Mungu, safari za watumishi, nyumbani kwa watumishi n.k. *(**Matendo 4:3**,**10:1-4; Filipi 4:15-20; Galatia 6:6**; **Isaya 1:10-17**).* Hivyo, kutofuata mwongozo wa Roho Mtakatifu kutakufanya utoe sadaka nje ya mpango kamili wa

Mungu katika utoaji wako na hivyo kusababisha matokeo haba katika utoaji wako.

**i) Kutoa Sadaka ili Kukubaliwa na Mungu**

Watu wengine wanatumia sadaka kutafuta haki ya Mungu, mara zote sadaka za hivyo hazileti baraka. Haki ya Mungu inapatikana bure kwa toba ya kweli na wokovu kupitia Yesu Kristo (***Matendo 10:17-48; Efeso 2:8-9; Rumi 10:9-10, 13; Yohana 3:16****)*. Tunaona utoaji wa Kornelio ambao ulikuwa wa moyo wa ukamilifu mbele za Mungu. Kupitia utoaji ule, Mungu aliutazama uaminifu wa Kornelio na kumwonesha njia sahihi ya kuhesabiwa haki. Yaani wokovu kwa njia ya Yesu Kristo. Hivyo, usitoe sadaka kisha kudumu katika dhambi kwa matarajio kwamba sadaka yako itakuwa sababu yako kuhesabiwa haki. Sadaka yenyewe haiwezi kusababisha uhesabiwe haki mbele za Mungu bila matendo matakatifu.

**j) Kukosa Mifereji ya Baraka**

Waumini wengi wanatoa lakini Mungu anapotaka kuwabariki anakosa mahali pa kuwabariki. Ipo mifano mingi katika Biblia ya watu ambao waliwahi kukaa kwa watu maarufu na wenye fedha kabisa lakini walibaki kama walivyo mpaka hapo walipokuwa wameamua kupata kazi zao. Ni vyema tukumbuke kuwa Mungu ameahidi kubariki kazi za mikono yako, uingiapo na utokapo atapabariki (***Kumbukumbu la Torati 28:6, 12, 16:15****,).*

Hii inamaanisha kuwa kila unalogusa litabarikiwa na uwepo wako bila kujali hiyo kazi ni yako ama la. Wapendwa wengi tumekuwa visima vya baraka kwa watu au makampuni tunayofanyia kazi bila kujua au wanajua lakini hawachukui hatua. Ndiyo maana, unapokuwa unaomba kazi kwa muda mrefu bila kupata inabidi pia ufikirie kuwa yamkini Mungu anataka uwe na kazi yako binafsi ili amimine baraka zako hapo.

- ***Mwanzo 13:2*** tunasoma kuwa Ibrahimu alikuwa tajiri wa **mifugo, fedha** na **dhahabu** je, vilishuka kutoka mbinguni? Bila shaka jibu ni hapana, Ibrahimu alifanya kazi.

- Lakini pia tukisoma ***Luka 5:4-6*** Yesu aliwaambia wanafunzi wake wachukue nyavu zao ili wavue samaki, hatimaye wakaziona baraka za Bwana kwa kufanya kazi. Ni kweli Yesu alikuwa na uwezo wa kuwapa samaki bila ya wao kuvua lakini Mungu alishaweka kanuni ya kubarikiwa kupitia kufanya kazi.

- Mungu alipopanda bustani ya Eden alimuweka Adam akamwambia ailime na kuitunza **(*Mwanzo 2:15*).** Hivyo mpango wa Mungu toka mwanzo ni kufanya kazi kisha anabariki hizo kazi, ***tunapokuwa tunatumia muda wote kufanya kazi za wengine tujue baraka zetu zinatawaliwa na watu wengine***.

- **Maarifa katika kazi**: tunapofanya kazi lazima tufanye kwa bidii na maarifa, Mungu anapenda watu wanaofuata maarifa kwa sababu vitu vyote vinafuata kanuni zake (***Mithali 12:1, 19:20).*** Katika **Mathayo 7:24-27**, Bwana Yesu anatoa mfano wa kumsifia mtu mwenye akili na kumlaumu mtu mpumbavu. Hii inatuonesha kuwa huko mbimguni huwa tunatazamwa kuhusu ufanyajikazi wa mambo yetu na kwamba tunategemewa kuyafanya mambo yetu kwa akili. Katika **Luka 14: 28-31,** pia tunaona jinsi ambavyo kwa mara nyingine, Yesu anatoa mfano wa jinsi ambavyo mwanadamu anatakiwa kupangilia mambo yake kabla ya kuyatenda. Kwamba lazima tuwe na mipango katika kila jambo na siyo kufanya tu. ***Tena tunatakiwa kuyafanya kwa ufanisi ambao unampa Mungu utukufu***. Sote tunajua, kuwa wana wa Israel walipokuwa jangwani waliishi kwa miujiza ya Mungu

lakini walipofika Kanaani walitakiwa wafuate kanuni za kufanya kazi ili wabarikiwe.

- Yakobo alipokuwa katika nyumba ya Labani, nyumba hiyo ilibarikiwa sana lakini mpaka ulipofika wakati wa kutambua kwamba Mungu hakupanga aishi kwa Labani kwa kipindi hicho. Labani alitaka kumfanya Yakobo awe kitega uchumi kwake lakini Yakobo akajitambua, akasimama kwenye nafasi yake akakataa (***Mwanzo 30:27-31).***

- Tatizo la waumini wengi ni kuwa hawana kitu ambacho kwacho Mungu atakiona na kuwabariki. Wameweka akiba ya baraka zao kwa Mungu na hivyo Mungu amekosa mahali pa kuwabarikia na badala yake ameishia kubariki mahali wanapofanyia kazi bila kujali kuwa hizo ni kazi zao au za waajiri wao.

- **Kuwa na kitu chako:** Hakikisha unamiliki cha kwako huku ukiendelea na kazi nyingine ili umpe Mungu nafasi ya kukuzidisha na kukustawisha (***2Wafalme 4:1-7)***. Katika maandiko hayo tunaona jinsi ambavyo huyo mama mjane alivyoulizwa na Elisha kwamba ana kitu gani? Bila shaka swali hilo lilimanisha kuwa Baraka za huyo mama zingeanzia kwenye kitu alicho nacho. Tunaona kuwa vyombo vya kujaza mafuta vilipoishia ndipo mafuta yaliishia pia. ***Hivyo Baraka zetu zitategemea jinsi tunavyowaza na jinsi tunavyo thubutu. Tukiwaza katika udogo, tutavuna hivyo hivyo, tusipothubutu hatutavuna kamwe na tutabaki kuwa watu wa lawama na kuwaonea wivu wale waliofanikiwa***. Angalia mfano wa kubarikiwa kwa nyumba ya Potifa (***Mwanzo 39:1-5)*** kwa sababu ya uwepo wa Yusufu. Hapa simaanishi kupinga kuajiriwa au kufanya kazi chini ya mtu, la hasha!! Ninachotaka ni

kukupanua mawazo na uelewa wako juu ya kusudi la Mungu juu yako.

Kumbuka Mungu anawaagiza wanaofanya kazi za watu wengine kuzifanya kwa uaminifu kana kwamba unafanya kwa Yesu Kristo (***Efeso 6:5-8*****).** Ukweli ni kwamba, Mungu anaweza kukubariki kupitia mahali unapofanyia kazi hata kama ni kazi ya mtu mwingine. Baraka za jinsi hii huwezi kunufaika nazo kwa kiwango kikubwa kama kiwango kile ambacho ungebarikiwa kama ingekuwa kazi yako binafsi. Maana yake tafuta kufanya zaidi ya kile kiwango unachofanya leo, tamani kuona zaidi ya kile unachokiona wakati huu. Tafuta chaneli ambazo ni halali mbele za Mungu na jamii inayokuzunguka uzitumie kuanzisha vyanzo vya Mungu kukubarikia. Kuwepo  kwako mahali popote ni lazima kuwe sababu ya Mungu kupabariki mahali pale kwa sababu tu ya uwepo wako.

Taifa la Misri pamoja na nyumba ya Potifa hawakuwa wacha Mungu lakini kitendo cha Yusufu kuwa mahali pale ilikuwa sababu macho ya Mungu kuelekea pale na kusikia maombi yao na kubariki mahali pale.

Siyo Misri pekee yake hata Yakobo kule kwa mjomba wake Labani hawakuwa wacha Mungu bali kubarikiwa kwa Labani ni kwa sababu ya uwepo wa Yakobo mahali pale. Kwani mjomba wake Yakobo alikuwa muabudu miungu, hakuwa anamwabudu Mungu aliyekuwa ndani ya Yakobo, na kama alikuwa naye basi pembeni alikuwa na miungu mingine **(*Mwanzo 31:30-32)*.**

Sasa kama kuwepo kwa wacha Mungu mahali kunakuwa chanzo cha mahali pale kubarikiwa, ninaamini tukiamua kufunguka na kuanzisha vitu au

miradi yetu ya kutuingizia au kutuongezea vipato Baraka zake zitakuwa zaidi ya zile zinazoweza kupatikana kupitia wale tunaotumika chini yao au kuwatumikia.

- Mungu ameahidi kutufichulia hazina na mali zilizofichwa (***Isaya 45:2-3***), bila shaka ataleta hizo mali kupitia kazi za mikono yetu.

**Baadhi ya Njia za Utoaji Mzuri**

Ili mtu atoe sadaka ambayo Mungu ataipenda na kuikubali na sadaka hiyo kuendelea kunena mbele za Bwana ni lazima utoaji wa sadaka hiyo uendane na neno la Mungu linavyoelekeza. Watu wengi hutoa sadaka zinazonyamaza kwa sababu hawatoi sawasawa na neno la Mungu. Utoaji wa sadaka ni suala la kiroho hivyo, ni lazima liongozwe na Roho Mtakatifu. Yesu Kristo anasema atakapokuja huyo Roho Mtakatifu atawaongoza na kuwatia kwenye kweli yote ***(Yohana 14:26; 16:13-14).***

Unaweza ukawa mtoaji wa sadaka nyingi lakini kama hazitokani na mwongozo wa Roho Mtakatifu matokeo ya matoleo hayo yanaweza kuwa madogo ukilinganisha na yule anayetoa kwa msaada wa Roho Mtakatifu. Kazi zote za kiroho zinaongozwa na Roho Mtakatifu, nje ya hapo utakuwa unatumia akili zako na matokeo yake yanaweza kuwa haba. Ni muhimu kuwa msikivu sana wa sauti ya Mungu kupitia Roho Mtakatifu katika maisha yako ya kiroho.

Kama tunavyojua mwanadamu hawezi kumpangia Mungu kanuni za utendaji kazi wake, hivyo zifuatazo ni baadhi tu ya njia za utoaji unaofuata neno la Mungu:-

1. **Toa Kulingana na Jinsi Mungu Alivyokubariki (*Kumbukumbu la Torati 16:10, 2Korintho 9:7*; *1Korintho 16:2*)**.

Kama mtu anapata ujira wa shilingi 30,000 kwa mwezi, ni tofauti na mtu anayepata laki tano kwa mwezi n.k. Lakini mtu anaweza kutoa zaidi ya kawaida kulingana na jinsi ambavyo Mungu amemuongoza kutoa. Katika utoaji wa makanisa ya Makedonia ***2Korintho 8:1-15,*** mtume Paulo anaguswa na kujitoa kwa makanisa haya. Makanisa haya ya Makedonia ni moja ya makanisa yaliyokuwa na washirika masikini sana, lakini washirika wale pamoja na umaskini wao waliongoza katika kumtia moyo mtume Paulo katika huduma yake kwa njia ya kutoa sadaka zao. Makanisa haya Makedonia sio tu walitoa bali walitoa kwa moyo wa ukarimu.

Hawa wapendwa sio tu walikuwa maskini bali pia walikuwa wanapitia kipindi cha mateso au dhiki kwa sababu ya Imani au wokovu waliokuwa nao lakini hali hii haikuwafanya kuwa wagumu kumtumikia Kristo. Hawa wapendwa na washirika wa Makedonia walikuwa maskini kwa nje lakini ndani ya mioyo yao walikuwa ni matajiri wakubwa mbele za Mungu kwa sababu ya ile Neema ya Mungu kujaa kwa wingi ndani yao, umaskini, dhiki na mateso viliongeza ukarimu wao kuwa mwingi zaidi na vikafanya mioyo yao kuwa rahisi kumtolea Mungu. Hawa watu au washirika wa Makedonia walijitoa katika kiwango kikubwa bila kujali hali zao za kiuchumi.

Hii inatuonesha kuwa moyo wa utoaji hautazami mali ambazo mtoaji anazo, hali aliyonayo au anayopitia, wala haitegemei muda mtu aliokaa katika wokovu bali ni upendo katika kujitoa kwa kujua ukuu wa Mungu na inawezekana hata watumishi wa Mungu walijaribu kuwashauri kutoa kulingana na hali zao na wasipite mipaka ya hali walizokuwa nazo. Watu hawa hawakukubali bali waliwaomba na kuwasihi watumishi wa Mungu wawaruhusu waendelee kujitoa kwa ajili ya injili (***2Korintho 8:4***).

Mtu aliye na kipato kidogo asione aibu au akajihisi kwamba sadaka yake haina thamani mbele za Mungu kutokana na kuonekana kwa macho ya kimwili kuwa ni ndogo. Kumbuka

katika utoaji wa sadaka, moyo wa mtoaji ni wa muhimu sana kuzidi sadaka anayotoa. Muhimu ni kuzingatia kuwa sadaka hiyo inagusa moyo wa mtoaji mwenyewe kwa uhalisia wa kipato chake (***2Korintho 8:1-3)***.

2. **Toa kwa Hiyari bila Kulazimishwa** ***(2Korintho 9:7, 8:3; Kumbukumbu la Torati 16:7)***

Usitoe sadaka kwa kutegemea ushawishi wa watu kwa sababu utoaji wako lazima uanzie moyoni mwako. Usitoe kwa kulazimishwa au kujilazimisha wala kwa kusononeka moyoni mwako**.** Kushawishiwa ni tofauti na kufundishwa, kufundishwa hukufanya uwe na uelewa sahihi kuhusu utoaji wakati kushawishiwa ni kukufanya ufanye maamuzi sawasawa na makusudi ya anayekushawishi.

Wapo watu wengi ambao utoaji wao hutegemea kiwango ambacho wameshawishiwa au wamelazimishwa kutoa ndipo wanaamua kutoa. Hii ndiyo sababu makanisa ya injili potofu yanaota kila kuchao na yanatumia mbinu za kuwashawishi waumini ili watoe sadaka. Ukweli ni kwamba tunahitaji kutoa sadaka inayopendeza mbele za Mungu kwa hiyari ya kutoka mioyoni mwetu.

Toka mwanzo Mungu huwafurahia watu wanaotoa kwa upendo tena kwa hiyari yao wenyewe ndiyo maana inaitwa sadaka ya upendo mbele za Mungu. Mungu anamwelekeza Musa kuwa awambie wana wa Israel wenye moyo wa kupenda ndiyo wamtolee sadaka kwa ajili ya kazi yake (***Kutoka 25:1-8****)*. Hapo utaona lipo suala la upendo, hiari na kiasi ambacho mtu amebarikiwa ndicho atakachomtolea Mungu kwa ajili ya kazi yake.

3. **Usitoe Chochote tu (*Walawi 22:20-22*)**

Wapo watu ambao hawachagui sadaka za kutoa mbele za Bwana, wanatoa chochote tu. Hii siyo sawa hata kidogo kwa sababu sadaka huonesha upendo wetu kwa Mungu hivyo lazima tuchague kilicho kizuri cha kumtolea Mungu. Unaposhindwa kuchagua sadaka za kutoa mbele za Mungu ni ishara ya kushindwa kufanikiwa katika utoaji wako.

Kila mtu anapotaka kumpelekea mtu anayempenda zawadi anatamani ampelekee kitu kizuri ambacho atakifurahia mara baada ya kukipokea. Ndivyo hivyo, hata Mungu anataka tuchague vitu vizuri vya kumtolea. ***Baadhi ya watu huona aibu kutoa kitu kisicho cha thamani kwa wanadamu wenzao lakini hawaoni tatizo kutoa kitu hichohicho madhabahuni pa Bwana***.

Fikiria katika hali ya kawaida umekutana na rafiki yako na unataka kumpatia pesa ya kula au ya kwendea njiani, kuna kiasi fulani cha pesa ambacho utaona aibu kumpatia ni lazima utampatia kiasi ambacho kinalingana na hadhi yako na ya kwake pia. Sasa swali la kujiuliza ni kwamba pesa ambayo unaona aibu kumpa mwanadamu mwenzako unapata wapi ujasiri wa kuitoa madhabahuni? Je, tunawaheshimu wanadamu kuliko Mungu?

Hapa ndipo mahali tunapopishana na uweza na Baraka za Mungu wetu. Kuna msemo wa vijana wa kisasa kusema “amepishana na gari la mshahara” huwezi kamwe ukapata mshahara mbele ya safari kama gari lililobeba mshahara wako umepishana nalo wakati linakufuata uliko na inawezekana ulipishana nalo kwa sababu ya kutolijua vizuri gari hilo. Maana yake ni kwamba, kwa kushindwa kumuelewa Mungu wetu kama wakristo wa Makedonia tumejikuta tunatoa sadaka chini ya kiwango ambacho Mungu anastahili. Matokeo yake tumezikosa Baraka zetu ambazo Mungu aliagiza zitufuate kupitia uelewa wetu juu yake na upendo wetu kwake kwa njia ya sadaka. Upendo huu kwake ndiyo unaopelekea kuamua kiasi cha sadaka cha kumtolea Mungu.

**Mfano:** S*iku moja nilikuwa nafundisha somo la utoaji pahali fulani nikawaambia leo kila mtu arudi nyumbani na sadaka yake ajinunulie zawadi yake yeye mwenyewe. Wengi waliona kuwa sadaka waliyokuwa wameleta mbele za Bwana haikufaa chochote hata kwa wao wenyewe.* Hii inaonesha kuwa watu wengi huwa tunaenda kanisani na sadaka ya kitu chochote tu ambacho hata sisi wenyewe tukipewa hatutakipenda kabisa.

4. **Toa kwa Furaha (kwa moyo wa ukarimu) (*2Korintho 9:6; 8:2)***

Ipo mitazamo kwamba unatakiwa kutoa kile kinachouma moyo wako ndipo Mungu atapokubariki. ***Hii siyo kweli hata kidogo, unatakiwa kutoa kile kinachogusa moyo wako siyo kinachouma (2Korintho 9:7)***. Hali ya kutoa kinachouma moyo wako inasababisha baadhi ya watu kutoa huku wakiwa wamejawa na huzuni mioyoni mwao. Hivyo, badala ya kupata Baraka, wanaishia kupata laana. Hawana furaha mioyoni mwao na wanatoa kwa masononeko makubwa ili tu kutimiza wajibu wa kutoa.

Huu sio utoaji wa upendo ambao Mungu anatuelekeza bali ni unyanga'anyi. Utoaji wa jinsi hii huonekana kuwa ni mzigo mkubwa kwa watoaji hata kufikia hatua ya kusababisha baadhi ya watu kuchukia kipindi cha matoleo. Baadhi ya watu huchukia kipindi cha matoleo na kuamua kutoka nje wakati wa matoleo. Ukweli ni kwamba wakati wa kutoa sadaka ni wakati wa kupanda mbegu, hivyo ni wakati wa shangwe na furaha kuu. Huu ni wakati wa kuonesha upendo wetu kwa Mungu kwa wema wa baraka zake za kila namna anazotubariki. Mungu anatuonesha kuwa yeye aliupenda ulimwengu kisha akamtoa mwanaye **(*Yohana 3:16*).** Utoaji wa upendo utaambatana na furaha na siyo huzuni moyoni mwa mtoaji **(*2Korintho 8:2, 7*)**.

5. **Toa kwa Imani (*Waebrania 11:4)***

“Imani ni kuwa na uhakika wa mambo yatarajiwayo” Chochote kile unachokitoa mbele za Mungu unahitaji kukitoa kwa imani kwamba kimepokelewa na Mungu na pia ujue kwamba katika kupanda kwako utavuna kwa wakati wake usipozimia moyo wako (***Waebrania 11:1, 6; Waebrania 10:38***). Utoapo sadaka kwa moyo wa upendo uwe na uhakika kuwa ile sadaka itazaa mara 30 au mara 60 au mara 100 (***Mathayo 13:3, 8***).

Sadaka bora ni kama mbegu iliyopandwa kwenye udongo mzuri, lazima izae na kuongezeka sana **(*Luka 6:38*)**. Lakini Neno la Mungu linatupa uhakika (imani) kuwa “***imani huja kwa kusikia … Neno la Kristo (Rumi 10:17).*** Mtu akiliamini neno la Mungu, kwamba Mungu hawezi kusema uongo, moyo wake utapokea uhakika (imani). Ndani yake litajengeka tarajio la kupokea kila anapotoa wala hataona anapoteza mali zake atoapo sadaka. Atajua kuwa kutoa sadaka si kupoteza bali ni kupanda kwa ajili ya mavuno (baraka) kubwa zaidi. Kila tendo lisilotoka katika imani ni dhambi (***Rumi 14:23*). Hakuna mkulima anayeweza kutoa kidogo wakati anaamini mavuno ni mengi. Atoaye kidogo hana imani ya kupokea, anaamini mbegu yake inapotea na ndiyo maana anaona ni bora apoteze kidogo.

Lakini mwenye imani ya kupokea, hutoa kwa wingi kwa sababu anajua sadaka yake haipotei bali imepandwa na itazaa sana. Kwa imani Habili alitoa sadaka iliyobora ukilinganisha na Kaini na Mungu akaizidisha ile sadaka, japokuwa Habili amekufa lakini sadaka yake ingali hai lakini Kaini alitoa sadaka yake kwa moyo usio na upendo mbele za Mungu ndio maana sadaka yake ikakataliwa **(*Mwanzo 4:2-5, Waebrania 11:4).***

6. **Toa Mara kwa Mara**

Watu wengine hufikiria kwamba utoaji una mwisho wake, jibu ni hapana. Mwisho wa utoaji kwako ni mwisho wa baraka zako,

hivyo usihesabu umejitoa mara ngapi, endelea kujitoa bila kukoma. Utoaji ni ibada, ibada yako kwa Mungu haina kikomo. ***Tunahitaji baraka nyingi sana kutoka kwa Mungu, hivyo utoaji wetu pia hautakiwi kuwa na kipimo***.

Ni vizuri viongozi wa kusanyiko la mahali pamoja waweke taratibu zisizokuwa na kikwazo kwa waumini kuhusu matoleo na michango mbalimbali. Ni vyema zifahamike aina ya sadaka zinazotolewa kila mnapokutana. Mfano, washirika wengine kila wakikutana huwa na matoleo ya sadaka ya upendo ya kila wakutanapo pamoja na machangizo ya ujenzi, uinjilisti, vyombo vya mziki n.k. Kila watu wamejiwekea utaratibu wao wa matoleo lakini suala la muhimu ni kuona kuwa sadaka zinatolewa katika utaratibu unaofahamika.

Yapo makusanyiko ambayo mpangilio wao katika utoaji wa sadaka na machangizo mbalimbali haupo vizuri kabisa. Yaani mchungaji au kiongozi akijisikia kuitisha changizo fulani anafanya hivyo bila hata kutoa taarifa kwa washirika. Utaratibu wa jinsi hiyo unakwaza watoaji. Kuna wakati ambapo dharura hutokea lakini ionekane kweli ilikuwa ni dharura kufanya hivyo, vinginevyo watu wapewe taarifa mapema juu ya changizo hilo ili wajiandae.

Angalia mfano huu: Siku moja nilishiriki katika ibada mahali fulani, ikaitishwa sadaka ya upendo na mafungu ya kumi, baada ya hapo mchungaji akatangaza changizo la ukarabati wa choo, baada ya hapo mchungaji akaitisha changizo la kusaidia ndugu fulani pale kanisani na baadaye tena akaitisha changizo la kusaidia ndugu fulani alikuwa anasafiri lakini nauli haijitoshelezi. Kwa utaratibu kama huo ni rahisi kukwaza washirika. Ni vyema dharura isiwe zaidi ya changizo moja. Vinginevyo watu wapewe taarifa mapema ili wajiandae kwamba siku tutakayokusanyika kutakuwa na sadaka ya upendo pamoja na machangizo kadha wa kadha. Pamoja na mapungufu ya

kibinadamu bado kujitoa kwetu mbele za Mungu kwa njia ya matoleo hakutakiwi kuwa na kipimo na tutoe bila lawama.

7. **Toa Sadaka na Kuipa Jina**

Kila sadaka ina jina lake ndiyo maana katika Biblia kuna sadaka ya amani, malimbuko, zaka, shukrani, nadhiri (***Hesabu 15:1-10*****)** n.k. Hivyo, ni vizuri kuipa jina sadaka yako, kwamba je, ni sadaka ya shukrani? au ni sadaka ya malimbuko? n.k. Hii ni kusema kuwa kabla hujapeleka sadaka yako madhabahuni au mahali popote ambapo Roho wa Bwana amekuongoza ni vizuri ukaiombea na kuikabidhi mikononi mwa Bwana kwa kumweleza Mungu kusudi la kutoa hiyo sadaka. Kuwepo na maandalizi mahsusi ya sadaka kabla haijatolewa.

8. **Usitoe ili Uonekane na Watu (*Mathayo 6:1-4)***

Unapoenda kutoa sadaka iwe ni madhabahuni au kwa makundi mbalimbaili ya wahitaji, bila shaka kuna watu watakuona au hata huyo unayemsaidia lazima atakuona. Hivyo, kuonekana kwa macho ya mwili siyo tatizo na hakuzuiliwi, kuonekana umebeba kuku au nguo au bahasha ya fungu la kumi kuelekea madhabahuni siyo tatizo. Kinachokatazwa hapa ni utoaji ambao moyoni mwa mtoaji anakuwa anatazamia kutukuzwa kwa jinsi ya kuchukua nafasi ya utukufu ambao Mungu anastahili, kuonesha kwamba kama asingekuwa yeye hilo jambo lisingefanyika na kwamba imekuwa hivyo kwa uwezo wake.

Hivyo, kuonekana kwako ni jinsi unavyojiona au unavyokusudia wewe mwenyewe moyoni mwako. Kwamba kama moyoni mwako unatoa ili watu wakuone, wakusifu, wakushangilie na kukulipa sawasawa na utoaji wako basi ujue unatoa ili uonekane machoni pa watu. Huu ndiyo utoaji ambao thawabu yake unaipata kwa wanadamu. Ni vizuri ifahamike kuwa kila utoaji una thawabu yake, tofauti na utoaji wa rohoni thawabu yake inatoka kwa Mungu wakati utoaji wa kimwili (wa kuonekana machoni pa

watu) thawabu yake inapatikana kwa wanadamu. Mara nyingi mtoaji wa jinsi hii huwa anakusudia moyoni mwake kupata kitu fulani kutoka kwa yule anayesaidiwa.

Mfano, baadhi ya wanasiasa hutoa misaada fulani kwa makundi ya watu huku mioyoni mwao wakikusudia kupata kura au waungwe mkono kwenye mambo yao ya siasa. Baadhi ya watu hutoa ufadhili wa masomo kwa watoto wasiojiweza lakini mioyoni mwao wanakusudia kupata uhusiano wa kimapenzi. Baadhi ya wafanyabiashara hutoa misaada ili kutangaza biashara zao. Wengine hutoa misaada ili wasifiwe na kupata umaarufu tu. Mifano ni mingi sana nimekutolea baadhi tu ili ikufunue katika suala la utoaji wa kuonekana machoni pa wanadamu. Watu wengine hawawezi kutoa sadaka zao wakiwa peke yao bila kutangazwa pamoja na kusifiwa, Wanapenda utoaji wao uonekane kwa watu jinsi walivyotoa, kiroho huo sio utoaji mzuri! Utoaji wa kiroho haufanywi kwa matangazo. Kusudia Mungu akuone katika utoaji wako badala ya wanadamu.

Yesu Kristo anasema mtu akitoa huku moyoni mwake anafikiria kutazamwa na wanadamu, basi thawabu yake ataipata kwa wanadamu. Yaani jinsi watu watakavyo mshukuru na kumpa utukufu anaotaka au jinsi watakavyomlipa kwa namna aliyokusudia moyoni mwake. Huyo hapati thawabu kutoka mbinguni.

Hii haina maana, kuwa mtu akitoa msaada basi asipewe shukrani au heshima anayostahili. Kushukuru ni jambo la kiroho, hivyo ni vyema kutoa shukrani kwa mtu aliyetenda wema kwako au hata kwa mtu mwingine. Jambo la shukrani linatia moyo kwa mtoaji kujitoa kwa wengine pia. Angalia jinsi ambavyo mtume Paulo anavyoshukuru juu ya kujitoa kwa watu wa makanisa ya Makedonia kwa ajili yake (***2Korintho 8:1-15***). Jambo hili liliwatia moyo watu wale na hivyo, pamoja na dhiki mbalimbali walizokuwa wanapitia lakini walikaza moyo wakaendelea kujitoa kwa ajili ya kazi ya Mungu.

# HITIMISHO

Natumai umebarikiwa sana kwa kusoma kitabu hiki. Naamini pia utoaji wako utapata hatua na wala hutabaki kama ulivyokuwa kwa kadri Roho Mtakatifu atakavyokuponya. Katika kitabu hiki, umesoma shuhuda zangu binafsi na za watu wengine pia ambazo Mungu kwa nyakati tofauti aliwatendea watu wake ili iwe ushuhuda na kwako pia. Nakuomba usisite kutoa ushuhuda kwa watu wengine ili nao wapone kupitia usomaji wa kitabu hiki.

Ndani ya kitabu hiki umesoma utoaji wa sadaka **Isiyo ya Kawaida** pamoja na nguvu iliyomo ndani ya sadaka ya aina hiyo. Roho Mtakatifu alinisukuma kuandika habari za sadaka isiyo ya kawaida ili kuponya watu waliozoea kutoa sadaka ya kawaida ambayo haijaleta matokeo kwao. Utoaji kamili unaongozwa na Roho Mtakatifu hivyo, natumai umeelewa nafasi ya Roho Mtakatifu katika utoaji wa sadaka.

Utoaji wa sadaka isiyo ya kawaida utakutoa mahali ulipo na ***kukupeleka mahali ambapo utapata matokeo halisi ya utoaji wa sadaka.*** Mungu ameahidi kutubariki kupitia sadaka lakini watu wengi bado hawajaona matunda ya utoaji wao kwa sababu wengi wao hutoa sadaka ya kawaida tu. Naamini kupitia usomaji wa kitabu hiki umepata uelewa mpana juu ya utoaji wa sadaka isiyo ya kawaida na matokeo ya utoaji wa aina hiyo. Mbali na sadaka isiyo ya kawaida, ndani ya kitabu hiki pia umeelewa aina mbalimbali za sadaka na utaratibu unaofaa katika utoaji wa sadaka hizo. ***Nakusihi uendelee kumtumikia Mungu kwa njia ya mali zako, kamwe hautapungukiwa wala watoto wako hawataomba mkate barabarani.***

Kumbuka kuwa kitabu hiki pamoja na vingine tofautitofauti vinapatikana kwenye Tovuti yetu ya **www.nguvuyasadaka.com**.